

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Saba – Tarehe 23 Juni, 2021

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2020.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2021 *(The Finance Bill, 2021)*.

**MHE. MARIAMU M. NYOKA - K.n.y MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2021 *(The Finance Bill, 2021)*

MWENYEKITI: Ahsante.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tunaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete.

Na. 475

Ujenzi wa Kituo cha Afya Ikuwo – Makete

MHE. FESTO R. SANGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Ikuwo?

MWENYEKITI: Hili ndiyo swali la Kibunge, swali *short and clear*. Mtu anauliza swali *page* nane? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Makete, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Makete shilingi milioni 400 katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ipelele. Ujenzi wa Kituo hicho umekamilika na kinatoa huduma zikiwemo huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Makete shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati za Usungilo, Nungu na Matenga. Vilevile, Mei 2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Makete shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kitulo. Aidha, ombi la Kituo cha Afya Ikuwo limepokelewa na linafanyiwa tathimini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaipitia na kuiboresha Sera ya Ujenzi wa Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata ili ujenzi ufanyike kimkakati na kwa tija zaidi badala ya kila Kijiji na kila Kata. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pia niipongeze Serikali kwa fedha zote ambazo imetuletea kwa ajili ya maendeleo ya Makete. Niseme wazi kwamba sitakuwa na haja ya kuwa na maswali ya nyongeza ila niiombe tu Serikali inavyofanya tathmini kwa ajili ya kituo hiki ikumbuke pia usafiri wa *ambulance* kwa sababu ni kilometa 70 kutoka pale kwenda Makete Mjini kwa ajili ya wananchi wangu. Ahsante. (*Makoff*)

MWENYEKITI: Ahsante na mabilion ya hela jana Waziri wa Fedha ameyatoa. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

Na. 476

Kujenga Vituo vya Afya – Ikungi

MHE. MIRAJI J. MTATURU aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Afya vya Issuna, Ikungi, Makiungu, Ntuntu na Misughaa ili kurahisisha huduma za dharura Wilayani Ikungi kwa kuwa Wilaya hii inapitiwa na Barabara ya Dodoma – Mwanza ambayo imekuwa na ajali za mara kwa mara?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa ili kuwahisha majeruhi na wagonjwa katika Hospitali za Rufaa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi iliyoanza kujengwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo hadi mwezi Mei 2021 ilikuwa imepatiwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo. Hospitali hiyo itasaidia kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali zitakazotokea eneo la Ikungi katika barabara ya Dodoma hadi Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Mei 2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi shilingi milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya Ihanja na Sepuka. Ujenzi wa Vituo hivyo umekamilika na vinatoa huduma ikiwemo huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapitia Sera ya Zahanati katika kila Kijiji na Kituo cha Afya katika kila Kata na itafanyiwa maboresho yenye tija zaidi ili ujenzi uwe wa kimkakati badala ya kila Kijiji au kila Kata.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya Ikungi ina magari matatu ya kubebea wagonjwa ambayo yapo katika Vituo vya Afya Ikungi, Sepuka na Ihanja ambayo yote yanaendelea kutoa huduma za rufaa za dharura ndani na nje ya wilaya ya Ikungi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtaturu.

MHE. MIRAJI J MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini katika swali langu la msingi mpango wa Serikali ni kujenga Kituo cha Afya kila Kata na katika Jimbo la Singida Mashariki tuna Kata 13 na tunacho Kituo cha Afya kimoja tu ambacho pia hakina huduma nzuri. Kwa sababu Kata hizi hazina Kituo cha Afya, naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Kata zingine ikiwemo Kata za Makiungu na Ntuntu ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan wakati wa kampeni? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, namshukuru sana Mheshimiwa, ni kweli ametuletea fedha kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya. Fedha hizo zilirudishwa kama ambavyo tulisema baada ya kuwa mwaka wa fedha umepita. Hivi tunavyoongea zaidi ya miezi sita, fedha hizo hazipo na ujenzi umesimama. Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha hizo ikiwemo kuleta vifaa tiba katika hospitali hiyo ili iweze kuanza kutoa huduma? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimetangulia kutoa ufafanuzi katika majibu yangu ya msingi kwamba Sera ya Maendeleo ya Afya ya Msingi inakwenda kuboreshwa ili iwe na tija na uhalisia na ufanisi mkubwa zaidi kwa sababu tuna vijiji karibu 12,000 na mitaa karibu 16,000 na tuna kata 3,956. Kwa hivyo, tunataka kwenda kimkakati zaidi kujenga vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati ambavyo vitakuwa *fully equipped* na vitatoa tija zaidi badala ya kujenga kila kata na kila Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika jimbo lake, vituo hivi vya afya ikiwemo kituo hiki ambacho ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini na vituo vile vingine vyote tutafanya tathmini na kama tutaona tija ya kuvijenga vitakwenda kujengwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba mpango huo utaendelea kutekelezwa kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fedha za hospitali ya halmashauri zilirejeshwa, kwa kipindi hicho zilirejeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 lakini Serikali imeshafanya maboresho. Waheshimiwa Wabunge wote tumesikia hapa wakati wa bajeti ya Wizara ya Fedha kwamba kuanzia Mwaka ujao wa Fedha, fedha zinazopelekwa kwenye miradi ya maendeleo hazitarejeshwa baada ya tarehe 30 Juni. Kufuatia hilo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizo tutafanya utaratibu kuzipeleka ili kuendelea na ujenzi wa hospitali kama ulivyopangwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASK. JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la Singida Mashariki linafanana kabisa na tatizo la Kata ya Mabwepande katika Jimbo la Kawe, ni lini sasa Serikali itamalizia ile Hospitali ya Jimbo la Kawe katika Kata ya Mabwepande?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Bulaya.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inajenga Hospitali ya Manispaa katika eneo la Mabwepande na mwezi wa tatu

tulifanya ziara pale, tulishirikiana na Mheshimiwa Mbunge, iko hatua za mwisho za ukamilishaji na tulishatoa maelekezo kupitia mapato ya ndani wahakikishe hospitali ile inaanza kufanya kazi ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya vifaatiba lakini pia kwa ajili ya kumalizia baadhi ya shughuli za ujenzi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za Manispaa ya Kinondoni. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Sera ya Afya mbali ya ujenzi wa zahanati pamoja na vituo vya afya lakini pia kuna kupandisha hadhi vituo vya afya. Hospitali ya Manyamanyama imepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya wilaya lakini bado inapata mgao kama kituo cha afya. Ni lini sasa itapatwa mgao wa vifaatiba na dawa kama hospitali ya wilaya kwa sababu ipo barabarani na inatoa huduma si tu kwa Wilaya ya Bunda, hata kwenye mikoa Jirani? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali ni kwamba vituo vile vyote ambavyo vimepandishwa hadhi kutoka kituo cha afya kwenda kuwa hospitali kama ilivyo Hospitali ya Manyamanyama vinastahili kuwekewa bajeti kwa ngazi ya hospitali na vifaatiba lakini pia hata ikama ya

watumishi. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutalifanyia kazi hilo kwa haraka iwezekanavyo ili iingie kwenye mgao wa hospitali. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna malalamiko kwenye hospitali wanalazimishwa kutumia walenzi maalum ambao gharama yao ni zaidi ya Sh.500,000 kwa mtu mmoja. Hizi hospitali haziwezi kulipa Sh.500,000 lakini wanakuwa *imposed*, lazima wawaajiri hawa watu. *Normally* wao wakipata mgambo wanalipa *less than that*. Kwa hiyo, mlitazame na hilo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

Na. 477

**Barabara ya Himo - Kilema, Pofo - Mandaka,
Uchira - Kisomachi na Mabogini - Kahe - Chekereni**

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia Wananchi wa Moshi Vijijini kuwa barabara za Himo – Kilema, Pofo – Mandaka, Uchira – Kisomachi na Mabogini – Kahe - Chekereni zitawekwa kwenye Bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Pofo – Mandaka – Kilema, Uchira – Kisomachi – Kolarie, Fongagate

– Mabogini – Kahe na Chekereni – Kyomu – Kahe zina jumla ya urefu wa kilometa 57.28. Serikali imeendelea kujenga na kukarabati barabara hizi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali ilijenga barabara ya Uchira – Kisomachi - Kolarie kipande chenye urefu wa kilometa 1.4 kwa kiwango cha lami kwa shilingi milioni 694, ujenzi wa barabara ya Chekereni – Kyomu - Kahe kipande cha kilometa 11 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 230.01 na kufanya matengenezo ya barabara za Fongagate – Mabogini - Kahe kipande cha kilometa 3 kwa gharama ya shilingi milioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali inatekeleza kazi za matengenezo ya kawaida katika barabara ya Pofo – Mandaka – Kilema kilometa tisa kwa gharama ya shilingi milioni 13.5, matengenezo ya barabara ya Uchira – Kisomachi – Kolarie kilometa 2.5 kwa gharama ya shilingi milioni 15, matengenezo ya barabara ya Fongagate – Mabogini – Kahe kilometa mbili kwa gharama ya shilingi milioni 60 na matengenezo ya barabara ya Chekereni – Kyomu – Kahe kilometa 3 kwa gharama ya shilingi milioni 4.5. Matengenezo ya barabara hizi yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 33 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Pofo – Mandaka – Kilema kilometa 11, matengenezo ya barabara ya Uchira – Kisomachi – Kolarie kilometa 4 kwa gharama ya shilingi milioni 11 na matengenezo ya barabara ya Fongagate – Mabogini – Kahe kilometa 42.25 kwa gharama ya shilingi milioni 540.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara hizi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kimezi, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa lakini kusema ukweli matengenezo yanayofanyika hayatoshelezi kitu. Unafanya matengenezo mwezi huu, mwezi ujao mvua kubwa ikinyesha unarudia tena matengenezo. Kusema kweli ahadi ambazo zilitupa ushindi sisi wana-CCM ni ahadi hii ya barabara ya Mandaka – Kilema ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni lini au anafanya *commitment* gani kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna taswira kwamba kule Kilimanjaro kuna barabara nzuri. Nataka niwahakikishie wananchi kwamba Kilimanjaro hatuna barabara nzuri, barabara zilizokuwepo ni zile za zamani zilizojengwa na Ushirika na zingine zinaenda mpakani. Sasa namuomba Mheshimiwa anayehusika, Waziri wa TAMISEMI, hajawahi kufika kwenye jimbo langu akaona hali ya usafiri ilivyo ngumu, najua kwamba tumeshapewa hela lakini hazitoshi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kimei uliza swali lako.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Je, Waziri atakubali kuongozana nami nikamtembeze aone hali ya barabara za Vunjo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza Mheshimiwa Mbunge amesema anataka kujua *commitment* ya Serikali juu ya ahadi ya barabara ya Mandaka – Kilema itaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami. Niseme tu kwamba tumelipokea kwa sababu moja ya wajibu wetu

ambao tulikuwa tunaufanya hapo awali ilikuwa ni kuchukua ahadi zote za viongozi ili tuziweke katika Mpango. Kwa sababu jana tumepitisha Bajeti Kuu na kuna ongezeko la fedha ambalo limetokea, naamini katika Mpango unaofuata tutakuwa tumeingiza na tutafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili kufika katika Jimbo lake, nimwambie tu hapa katika Bunge lako Tukufu kwamba niko tayari kwa sababu mara baada ya Bunge nitakuwa na ziara ya kuzunguka katika maeneo mbalimbali ikiwemo zile ahadi ambazo nimezitoa hapa kwa Wabunge mbalimbali kufika katika maeneo yao. Kwa hiyo, moja ya eneo ambalo nitafika ni pamoja na Vunjo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini barabara ya Mzumbe – Mgeta itajengwa kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Awamu ya Nne? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, alichozungumza hapa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ya utekelezaji wa Barabara ya Mzumbe mpaka Mgeta, niseme tu kama nilivyojibu katika jibu la msingi na la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kimei kwamba, na yenyewe tunalingiza katika mpango, tutaizingatia. Barabara nyingi tutazingezea katika

mpango baada ya kupata ongezeko la fedha hii ambayo jana Bunge lako Tukufu lilipitisha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage.

Na. 478

Huduma ya Mazoezi Tiba na Utengamao Katika Vituo vya Afya

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto iliyopo katika vituo vya kutolea huduma za afya ya kukosekana kwa Idara ya Huduma ya Mazoezi Tiba na Utengamao ukilinganisha na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji aina hiyo ya tiba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna ongezeko kubwa la uhitaji wa huduma ya mazoezi tiba na utengamao kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, huku kukiwa na changamoto ya uwepo wa miundombinu stahiki, vifaa na wataalam kwenye vituo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefanya tathmini ya mahitaji wa huduma ya mazoezi tiba na utengamao kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na inaendelea kukamilisha mpango mkakati ambao utatoa mwongozo katika kutatua

uhitaji wa huduma hizo. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itatekeleza kikamilifu mpango utakaotolewa ili kuboresha huduma ya mazoezi tiba na utengamao katika vituo vya afya. Ahsante.

MWENYEKITI: Dkt. Kaijage.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kutokana na uhitaji mkubwa na ukuaji wa tatizo hili la *stroke*, kwa maana ya kupooza na uhitaji wa mazoezi tiba na utengamao:-

Je, Serikali sasa ina mpango gani kuhakikisha kwamba inaboresha vitita vya Bima ya Afya ya Taifa na Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa ili tiba hii iwe jumishi katika bima hizi kwa ajili ya ustawi wa wananchi wetu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukiza ambalo linasababisha uhitaji mkubwa sana wa tiba mazoezi pamoja na huduma za utengamao. Serikali inaendelea kuboresha mpango mkakati ambao utakuja na mbinu; kwanza za kuhakikisha tunaweka mipango madhubuti ya kuzuia magonjwa yasiyoambukiza; pili, kuwa na vifaa tiba vya kutosha na wataalam katika maeneo ya magonjwa yasiyoambukiza na pia utengamao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tutakwenda kuona wazo zuri la Mheshimiwa Mbunge tuone namna gani tunakwenda kuboresha eneo la bima ya afya, lakini na *CHF* na huduma nyingine kuweza ku-cover huduma hizi za mazoezi tiba na utengamao. Kwa hiyo, tumelichukua wazo hilo, ni zuri sana na kwa kipindi hiki ni wakati muafaka, tutakwenda kuoifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo.

Na. 479

Ujenzi wa Soko la Kimkakati Lusahunga Katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kimkakati la Rusahunga Wilayani Biharamulo litakalogharimu shilingi bilioni 3.5 kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko nchini kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo ndani na nje ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha masoko yanaanzishwa, kuboreshwa na kuendelezwa ili kutoa fursa kwa wakulima wadogo pamoja na wafanyabishara kuuza mazao na bidhaa zao katika masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilitenga eneo la uwekezaji katika Kata ya Lusahunga lenye ukubwa wa ekari 65 ambalo lina thamani ya shilingi bilioni 3.5. Eneo hili limetengwa kwa ajili ya kujenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, kujenga maghala ya kuhifadhia

mazao, miundombinu ya majengo ya kibiashara kama mahoteli, ujenzi wa soko la kimkakati, kituo cha afya, viwanja vya makazi, na kituo cha mafunzo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*) imeendelea kusisitiza Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kutenga fedha katika bajeti yake ili kufanikisha ujenzi wa soko hilo. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta wadau mbalimbali ikiwemo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili iweze kufanikisha ujenzi wa soko hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer*.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali, lakini pia labda nieleze kidogo; mnamo tarehe 1 mwezi wa Kumi mwaka jana 2020 tukiwa katika kampeni Waziri Mkuu aliahidi ujenzi wa soko hili pale Nyakanazi na tarehe 11 mwezi wa Pili wakati akijibu Maswali ya Papo kwa Papo, swali lililoulizwa na Mheshimiwa Neema Lugangira aliahidi pia ujenzi wa soko hili na akataja kabisa ni soko la kimkakati na akataja *value* yake kama ni *3.5 billion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majibu ya Serikali wanasema wanahamasisha Halmashauri ya Biharamulo ili iweze kufanya ujenzi wa soko hili; hili soko limetamkwa, ukisema *3.5 billion* kwa Halmashauri ya Biharamulo wajenge soko hili, labda litakaa zaidi ya miaka kumi, kwa sababu uwezo huo hatuna; na ilitamkwa humu ndani ya Bunge:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate *commitment* ya Serikali kwanza nijue *financing* ya soko hili itafanyika vipi? Sisi uwezo huo hatuna. Kwa hiyo, nipate majibu ya Serikali kama Serikali kuu itafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu soko hili ni muhimu kwa ajili ya kufungua ukanda wetu na ni soko la kikanda litakalohudumia nchi za Kongo, Burundi, Rwanda na

nchi nyingine zote za Jirani: nipate majibu ya Serikali, ni lini ujenzi wa soko hili utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ina mkakati na mipango mbalimbali ya kuhakikisha inatekeleza ahadi ambazo viongozi wa Serikali wanaahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Chiwelesa kwa ufuatiliaji mkubwa anaofanya kwa ajili ya maendeleo katika Jimbo lake la Biharamulo Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli masoko haya ya kimkakati na hasa masoko ya pembezoni ambayo yako katika mipaka ya nchi za jirani na hasa hizi za Kongo, Rwanda na Burundi ni masoko ambayo yana umuhimu sana kuyaendeleza ili yaweze kuleta maendeleo ya nchi, lakini kuwapatia kipato wananchi wanaokaa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kupitia programu ya *ASDP II* ambayo pia imeweka ule mfumo wa *O and OD* ambao ni fursa na vikwazo kupitia utaratibu huo, Halmashauri zinahamasishwa kuangalia vyanzo mbalimbali vya ku-*finance* mipango yao, mikakati yao katika kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na TAMISEMI tuna mikakati mbalimbali ambayo pia kupitia humo tunaweza kujenga masoko haya kulingana na fedha zinavyopatikana. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

Na. 480

**Hitaji la Majisafi Kata za Mwamala, Samuye, Busanda,
Usule, Bukene na Imesela**

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Kata za Mwamala, Samuye, Busanda, Usule, Bukene na Imesela?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Kata ya Mwamala, Samuye, Busanda, Usule, Bukene na Imesela kupitia mpango wa muda wa kati na muda mrefu. Kwa mwaka wa 2020/2021, kazi zilizofanyika ni pamoja na kufanya usanifu wa matanki mawili yenye lita 100,000 na lita 200,000, mtandao wa kusambaza maji wa urefu wa kilometa 44.8 na vituo vya kuchotea maji 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, ujenzi wa miundombinu ambayo itatumia maji kutoka mradi wa maji wa Masangwa, Ilobashi, Bubale utafanyika ili kuongeza upatikanaji wa maji katika Kata za Mwamala na Samuye.

Aidha, kwa mpango wa muda mrefu ni kutumia maji ya bomba kuu la kutoka Ziwa Victoria kupeleka maji Tinde, Shelui, ambapo kata zote sita zitapata huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwezi Desemba, 2022.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Christina.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amesema kwamba mradi wa muda mrefu wa Shelui – Tinde utaweza kukidhi mahitaji ya wananchi wa Shinyanga: Je, ni lini sasa Mradi wa Shelui – Tinde utanza kwa kuwa mkataba umeshasainiwa toka tarehe 25 mwezi wa Pili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tunajua Sera ya Maji ni kuhakikisha kwamba inasambaza maji katika vijiji vyote ambavyo vinapitiwa na bomba kuu la Ziwa Viktoria.

Je, ni lini Serikali itanza kusambaza maji katika Kata za Lyabukande, Lyamidati, Nindo, Imesela na Didia?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Swali zuri sana, fupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mradi huu kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi tunatarajia kutoa maji Ziwa Victoria na Shelui – Tinde pia itakuwa ni moja ya wanufaika mwaka ujao wa fedha, kadiri fedha tunavyozipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais, tumesikia jana wakati Bajeti ya Serikali Mheshimiwa Waziri akihitimisha pale, Mheshimiwa Rais ametuongezea fedha ambazo zitatusaidia kuongeza maeneo mengi katika nchi hii kuhakikisha maji ya uhakika yanakwenda kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la usambazaji maji katika miradi yetu hii ni lazima ifanyike. Lengo ni kuona kwamba, wananchi wanapelekewa maji karibu na makazi yao na kupunguziwa umbali mrefu wa kutembea. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kisangi na Mheshimiwa Bilakwate ajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali lini itakamilisha mradi wa maji wa visima vya Kimbiji na Mpera kuwasaidia wananchi wa Halmashauri ya Kigamboni waweze kupata maji safi na salama; na pia katika Kata za Tuangoma, Chamazi, Mbande, Mianzini, Kibondemaji na Charambe wote hawa waweze kunufaika na mradi huo?

MWENYEKITI: Ongezea na Majimatitu. Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Visima hivi vya maji vya maeneo ya Kimbiji, Kigamboni na maeneo haya yote ya ukanda ule vinatarajiwa kuhakikishwa vinakamilika mwaka ujao wa fedha, kadiri fedha ambavyo tutakuwa tukiendelea kuzipokea ndani ya Wizara yetu. Maeneo ya Tuangoma, Majimatitu, kote huko Wizara inatupia jicho la kipekee kabisa. Tunafahamu ongezeko la wakazi ni kubwa, hivyo na sisi tutahakikisha tunafanya kazi usiku na mchana ili maji yaweze kuwafikia wananchi wa maeneo haya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate, halafu jandae Mheshimiwa Anatropia.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye Wilaya ya Kyerwa, Kata ya Bugomora, Kata ya Mlongo, Kata ya Kimuli na Kata ya Kyerwa Kagenyi, kuna miradi ambayo usanifu wake umekamilika, lakini mpaka sasa hivi Serikali bado haijatoa fedha ili miradi hii ianze. Lini Serikali itatoa fedha miradi hii ianze? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Waziri anapendeza na maji yapo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa hiyo *compliment*. Kwa swali la Mheshimiwa

Mbunge kutoka Jimbo la Kyerwa, eneo hili pia Serikali tumeendelea kulipa jicho la kipekee. Wizara kupitia *RUWASA* na mamlaka pale Mji wa Kyerwa wataendelea kushirikiana kuhakikisha miradi hii yote ambayo haijakamilika iweze kukamilika kwa wakati ili wananchi waweze kunufaika na Serikali ya Awamu ya Sita.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Changamoto ya maji katika Kata za Murongo, Kibale, Bugomora ambazo ni kata za mpakani mwa Mto Kagera zinaweza kumalizwa kama kukianzishwa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Kagera kuja kuhudumia wakazi. Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha tunapata maji ya kutosha kutoka Mto Kagera kuhudumia hizi kata ambazo ziko pembezoni mwa huo mto? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Anatropia, hakika akina mama tunasemeana vema. Tunafahmu mwanamama ndiye anayepata shida ya kubeba maji kichwani na sisi kama Wizara tumesema lazima tumtue mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kutoka Mto Kagera sisi kama Wizara ni moja ya vipaumbele vyetu kutumia mito na maziwa makuu kuhakikisha maji yanapatikana. Kama nilivyomjibu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Anatropia tutakuja pamoja na Mheshimiwa wa Jimbo tutaweka mambo sawa, Kyerwa maji yatapatikana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Kitandula.

Na. 481

**JWTZ Kuwalipa Fidia Wananchi wa Kata ya
Mwakijembe – Mkinga**

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Mwakijembe ambao mashamba yao yalitwaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) watalipwa fidia?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. Jiandae Mheshimiwa Ridhiwani.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilianzisha Kituo cha Ulinzi mwaka 2017, eneo la Kata ya Mwakijembe. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga iliona umuhimu wa kutenga eneo hilo kwa matumizi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya mpakani. Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilitembelea eneo husika mwaka 2017 kujionea hali halisi. Eneo husika awali lilikuwa ni la mradi wa Serikali wa umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Mwakijembe wanaombwa wawe na subira pindi taratibu za kisheria za utwaaji wa eneo zikikamilika. Serikali italipa fidia kwa wananchi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia sababu zilizotolewa hadi Jeshi kukabidhiwa eneo hilo, Jeshi litaendelea kutumia eneo hilo wakati taratibu za ulipwaji wa fidia zinaendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dunstan.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kata ya Mwakijembe tuna changamoto kubwa sana ya ukame. Kwa hiyo, eneo hili lililotwaliwa ndilo eneo pekee linalofaa kwa kilimo; na kwa sababu, wananchi hawa wameondolewa kwenye eneo lile. Je, Serikali iko tayari kufanya mchakato wa haraka wa kuwafidia watu hawa ili waondokane na madhila wanayoyapata sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili. Kwa kuwa imebainika wazi kwamba eneo hili ni hatarishi; kwa miaka miwili mfululizo yametokea mafuriko makubwa na tumewahatarisha Askari wetu kwenye eneo lile: Je, Serikali ipo tayari kuwahamisha Askari hawa kwenda kwenye eneo la awali ambalo Kamati ya Bunge iliona ili Askari hawa wakae kwenye eneo ambalo ni salama? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, ni dhamira ya Serikali kupitia Wizara yangu kuwalipa fidia wananchi wa maeneo yote ambayo yametwaliwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiulinzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kitandula kama tulivyowahi pia kuzungumza, ni kwamba tunashirikiana na wenzetu Wizara ya Ardhi na Wizara ya Fedha, na yako maeneo mengi ambayo tayari tumeshalipa fidia; pia uko mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Fedha kutupatia fedha na taratibu zikikamilika wananchi hawa nawahakikishia kwamba watalipwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kuona umuhimu wa eneo hili kutumika tena kwa wananchi, niseme tu kwamba, labda kutokana na changamoto za mvua nyingi tulizozipata hivi karibuni, umevutiwa pia kuona uko umuhimu wa wananchi kuendelea kufanya umwagiliaji

katika eneo hili; niseme tu kwamba zile sababu za kupewa eneo hili bado zipo. Hata hivyo tunaweza tukalitazama kutokana na maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, iko kamati maalum ambayo inaendelea kuyapitia maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, naelekeza wafanye pia marejeo katika eneo hili kwa kushirikiana na Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na pia kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuone kama pia tunaweza tuka-*reallocate*, tukapata eneo lingine bila kuondoa sababu muhimu za kufanya vijana wetu waendeleo kufanya shughuli zao muhimu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tutaendelea kushirikiana ili kuona tunaweza kutenda vema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kuona umuhimu wa eneo hili kutumiwa tena na wananchi, labda kutokana na changamoto ya mvua nyingi tulizozipata hivi karibuni, Mbunge amevutiwa kuona kwamba upo umuhimu wa wananchi kuendelea kufanya umwagiliaji katika eneo hili. Niseme tu kwamba, zile sababu za kupewa eneo hili bado zipo, lakini tunaweza tukalitazama kutokana na maoni ya Mbunge kwa sababu ipo Kamati Maalum ambayo inaendelea kuyapitia maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimhakikishie tu Mbunge kwamba naelekeza wafanye pia marejeo katika eneo hili kwa kushirikiana na Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya lakini kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuone kama tunaweza tuka-*reallocate*, tukapata eneo lingine bila kuondosha sababu muhimu za kufanya vijana wetu waendeleo kufanya shughuli zao muhimu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tutaendelea kushirikiana ili kuona tunaweza kutenda vema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Mbunge ameshakuelewa. Mheshimiwa Ridhiwani.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niunge katika swali alilouliza ndugu yangu Mheshimiwa Dunstan Kitandula, kwamba kumekuwa na utaratibu au zoezi ambalo linaendelea kule Msata katika maeneo ya Kihangaiko na Pongwe Msungura wakipima maeneo ya wananchi katika maana ya kulipa fidia, lakini kwa taarifa nilizozipata za juzi ni kwamba zoezi lile limesimama kwa sababu ya Mkataba ambao walikuwa wamepeana baina ya Wizara na yule mpima kuhusiana na eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika spirit ya kuondoa migogoro iliyoko baina ya Jeshi na wananchi...

MWENYEKITI: Sasa uliza swali.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, maarufu kama Baba Aziza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira yetu kupima maeneo yote yanayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo huo ni utaratibu unaoendelea na nimhakikishie tu Mheshimiwa Ridhiwani, sio kwamba zoezi limesitishwa, zoezi la upimaji maeneo yote linaendelea lina hatua zake. Kwa hiyo niwatoe wasiwasi tu wananchi wa eneo la Msata Kihangaiko, wanavyoona wale wapimaji hawapo wanafikiri labda shughuli imesita, hapana.

Nimtoe wasiwasi pia Mheshimiwa Ridhiwani zoezi linaendelea, tutahakikisha maeneo yote tunamaliza kufanya upimaji na wananchi wanapata haki zao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo aulize swali lake.

Na. 482

Umeme wa Gridi ya Taifa - Mkoani Katavi

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa umeme wa *Grid* ya Taifa Mkoani Katavi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme wa Gridi ya Taifa wa msongo wa kilovolti 132, yenye urefu wa kilometa 381 kutoka Tabora hadi Katavi. Mradi huu unahusisha pia ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza umeme vya msongo wa kilovoti 132 kwenda 33 vya Ipole, Inyonga na Mpanda. Ujenzi wa Mradi unatarajia kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2023. Gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 64.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa mradi mwingine wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Iringa - Mbeya – Sumbawanga – Mpanda hadi Kigoma yenye urefu wa kilometa 1,232, unatarajiwa kuanza Novemba na kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 470.42.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa mradi. Swali la kwanza; Kata za Kasansa, Mamba, Maji Moto, Mbede Mwamapuli, Chamalendi, Usevya na Kibaoni zinatumia umeme wa kutoka nchi ya jirani ya Zambia, umeme ambao hautoshi ni *kilowatt* 100. Tuliomba kupata umeme wenye *kilowatt* 500. Je ni lini Serikali itatuletea *transformer* zenye *kilowatt* 500?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye Mji ya Nyonga ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele umeme hautoshi kwa sababu umeme uliopo wakati unawekwa ulikuwa umewekwa kwa mahitaji madogo, mji umeongezeka, wananchi wanafanya biashara, wamefungua miradi ya ujasiriamali, ambayo ni mashine za kusaga na vitu vingine. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutuongeza umeme wenye *megawatt* zaidi ya nne?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa kutambua juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba gridi ya Taifa inafika katika Mkoa wetu wa Katavi. Mkoa wa Katavi haujafikiwa na gridi lakini unapata umeme kutoka katika vyanzo viwili, Wilaya ya Tanganyika na Wilaya ya Mpanda Mjini wanatumia *generator* mbili ambazo ziko pale Mpanda mjini na mpaka sasa zinazalisha *megawatt* kama 5.87 hivi na umeme ule unatosha maeneo yale kwa sababu matumizi ya Mkoa wa Katavi kwa sasa kwenye yale maeneo ya mjini ni *megawatt* kama 5.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini chanzo cha pili cha umeme kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni umeme

ule unaotoka Zambia unapita Sumbawanga unapita Namanyere unakuja kuingia sehemu ya karibu na Mpanda Mjini unakuja kuingia kwenye Wilaya ya Mlele kwenye hayo maeneo ya Mwamapuli, Maeneo ya Majimoto, Maeneo ya Kibaoni aliyoyataja ambayo sasa ndio umeme unaingia pale kutokea Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachokifanya kwa sasa cha kwanza kabisa inahakikisha kufikia 2023 imefikisha gridi ya Taifa katika Mkoa wetu wa Mpanda kutokea Tabora. Jambo la pili ambalo inalifanya ni kuhakikisha kwamba inaongeza uwezo wa hizo *transformer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita *transformer* yenye uwezo wa *kilowatt* 400 imeongezwa katika Wilaya ya Mlele ili kuongeza nguvu kwenye hayo maeneo ya Kata za Mlele ambazo amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge afanye mawasiliano, atataarifiwa kwamba sasa hali ya umeme imetulia na sasa Katavi inaweza kuendelea vizuri wakati tukiwa tunahakikisha kwamba gridi inafika kwenye Mkoa wetu wa Katavi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilave.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya ambazo zilichelewa sana kupata umeme wa *REA*. Kwa bahati nzuri kwa sasa Serikali inatekeleza mradi huo. Kwenye Mradi wa *REA phase II* vipi vijiji vilisahaulika kuingizwa kwenye mradi. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha vijiji vilivyosahaulika katika mradi wa *phase II*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika swali la msingi na swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Mbogo. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Kakoso pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Katavi pamoja na Mpanda wanavyofuatilia masuala ya umeme vijijini katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yapo maeneo nchi nzima ambayo yalisahaulika na yalikuwa yanafikia takriban maeneo ama vijiji 610.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Kakoso vijiji vyote 610 ambavyo vilisahaulika tumefanya marejeo na vijiji vyote vimeingia kwenye mpango na vimekabidhiwa wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Kakoso kwa sababu ni kweli hata kata kubwa ya Mishamo pamoja na Mwese pamoja na Utamata vilisahaulika lakini vyote vimeingia kwenye mpango na wananchi wote watapata umeme kwa uhakika ndani ya miezi 18 kutoka sasa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kilave halafu Mheshimiwa Mayenga.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza, je, ni lini Serikali itaweza kutuongezea *transformer* nyingine kwenye Jimbo la Temeke kwani tuna mahitaji ya *megawatt* 117, lakini sasa hivi tunatumia megawatt 32. Je, tutapata lini *transformer* hii nyingine? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Jimbo la Temeke pamoja na Mbagala na Mkuranga tumelazimika kuongeza vituo vitatu katika kila wilaya kwa ajili ya kuongeza *transformer* za *megawatt* 48 kila mahali, kwa hiyo Temeke, Mbagala pamoja na Mkuranga tunaongezea *transformer* ya *megawatt* 48 kila eneo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Mayenga.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Shinyanga Mjini licha ya kuwepo kwa umeme wa kutosha kutoka kwenye gridi ya Taifa, lakini kumekuwa na tatizo kubwa sana la kukatikatika kwa umeme. Je, Serikali ipo tayari sasa kuja na hasa Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kule Shinyanga Mjini kusikiliza wananchi jinsi wanavyoathirika kibiashara pamoja na kijamii?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mayenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kufuatana naye katika Jimbo lake kwa siku alizotaja. Hata hivyo, tatizo la kukatika kwa umeme katika Mkoa wa Shinyanga inatokana na matengenezo yanayofanyika kwa sasa katika *line* ya Segese ya umbali wa kilometa 12. Kwa hiyo mara nyingi tunataoa matangazo kurejesha hali ya umeme katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Shinyanga unapata umeme kutoka *substation* ya lbadakuli yenye *megawatt* 182 ambapo mahitaji ya Mkoa wa Shinyanga ni *Megawatt* 123. Kwa hiyo umeme wa Mkoa wa Shinyanga unatosha, isipokuwa kwa sasa wananchi tunaomba radhi katika maeneo yote yanayopitiwa ikiwemo Ngokoro na maeneo mengine kwa sababu ya matengenezo ya *line* ya Segese.

Ndani ya 14 matengenezo yatakamilika na umeme utarejea katika hali yake ya kawaida.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Njombe tunapitiwa na gridi inayotoka Makambako kwenda Songea, lakini bado tumekuwa na tatizo kubwa sana la ukatikaji wa umeme ambao sisi tunaamini pamoja na maelezo ambayo Waziri ameyatoa siku ya nyuma, tunaamini kutokana na *grid stability*, ni lini sasa swala la ukatikaji wa umeme usioisha wa Mkoa wa Njombe na Mji ya Njombe utafikia tamati? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hasa katika eneo la Njombe pamoja na Ludewa umeme unakatika kwa kiasi kikubwa kwa sababu kuna matengenezo ya kufunga *auto recloser* ambayo inaimarika ndani ya siku 28. Pia katika maeneo ya Njombe na Ludewa ipo *line* ambayo tunaongezea, tumetenga shilingi bilioni 270 katika mikoa miwili na bilioni 100 kila mkoa kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa mitambo na kuimarisha umeme katika Mkoa wa Makambako, Njombe pamoja na Ludewa. Kwa hiyo niwahakikishie wananchi wa Ludewa pamoja na Njombe kwamba ndani ya muda unaokuja ambao nimeutaja hali ya umeme itaimarika kwa kiasi kikubwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilitupa orodha ya makandarasi ambao wanafanya kazi katika wilaya zetu na majimbo yetu. Sasa, je, Serikali inaweza

ikatupatia orodha ya awamu hii ya REA ya tatu, mzunguko wa pili, ni vijiji vipi na vitongoji vipi vitakavyofanyiwa kazi ili iwe rahisi kwa Waheshimiwa Wabunge kufuatilia na kutoa taarifa Serikalini?

MWENYEKITI: Wabunge wanaume mbona hamwombi kwenda ziara pamoja na Mawaziri.

Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotoa yale mawasiliano ya mkandarasi na baadaye tukatoa mawasiliano ya Mbunge kwa Mkandarasi, tuliamini kwamba kwenye mawasiliano hayo masuala yote yanayohusiana na upelekaji wa umeme kwenye maeneo yetu yatafanyika. Aidha, sisi kama Wizara tuko tayari kuendelea kutoa ushirikiano na kutoa taarifa sahihi kabisa na kubwa kabisa za maeneo yapi yatakatayofikiwa na umeme ili Waheshimiwa Wabunge sasa watuambie yale ambayo yanaonekana yamebaki kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, vile vijiji 600 tayari tumevichukua ili sasa kwa wigo mpana tuweze kushirikiana pamoja kuhakikisha maeneo yote yanachukuliwa.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Jesca.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa majimbo ya mijini mitaa ndio kama vijiji. Swali, je, ni lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye mitaa yetu kwa mfano Jimbo la Iringa Mjini kata ya Isakalilo, Mtaa wa Kitasengwa Mkonga, Majengo Mapya; Kata ya Mkwawa, Mtaa wa Wahe na Hoho, Kata ya Igumbilo Mtaa wa Ulonge...

MWENYEKITI: Sio zote tena wewe taja moja tu, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia umeme katika mitaa. Sasa naomba nijibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumetenga mitaa 637 kwa nchi nzima ikiwemo mitaa kwa Mheshimiwa Jesca na mitaa yote itaanza kupelekewa umeme kuanzia mwezi Novemba mwaka huu ndani ya miezi 18. Tumetenga fedha hizo kwa awamu tunaanza na mitaa yote ambayo inafanana na hali ya kivijiji, lakini na mitaa mingine ambayo ipo katika majiji makubwa pamoja na manispaa kwa nchi nzima. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, swali litaulizwa na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu.

Na. 483

Mashamba Yasiyoendelezwa Karatu – Bendhu

MHE. DANIEL A. TLEMAI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza mashamba ya Karatu –Bendhu pamoja na kuwalipa wafanyakazi wa mashamba hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ina jumla ya mashamba 33 yanayomilikiwa na wawekezaji katika tasnia ya mazao ya biashara na chakula. Kati ya mashamba hayo 33 mojawapo ni Shamba la Bendhu

lililopo Kata ya Oldeani lenye ukubwa wa hekta 472, Mwekezaji wa shamba hilo aliyemilikishwa kwa miaka 99 kuanzia 1948 hadi 2047, ameliendeleza kwa asilimia 49 kwa kilimo cha mazao ya ngano na kahawa. Aidha asilimia 45 ya shamba linalimwa na wafanyakazi kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mashamba yote 33, Shamba la Bendhu ndiyo lenye mgogoro wa mirathi iliyotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na.6 la tarehe 5 Februari, 2021 katika ukurasa wa 13. Kutokana na mgogoro huo uzalishaji wa mazao katika shamba hilo uliyumba na kusababisha malipo kwa wafanyakazi kutofanyika kwa wakati. Aidha, wafanyakazi wa shamba hilo walifungua kesi Na.8 ya mwaka 2015 katika Kamisheni ya Usuluhishi na Maamuzi (CMA) Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majadiliano ya kesi hiyo, mwezi Desemba, 2020 yalifikwa makubaliano kwamba wafanyakazi wataendelea kulipwa kadri ya mapato yatakavyokuwa yanapatikana kutokana na uzalishaji katika shamba hilo. Pia, utekelezaji wa makubaliano hayo unasimamiwa na Chama cha Wafanyakazi. Aidha, nia ya Serikali ni kuona utekelezaji wa makubaliano hayo unafanyika bila changamoto yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na shauri la mirathi kuwa mahakamani, Serikali inasubiri maamuzi ya Mahakama juu ya shauri hilo. Aidha, hakuna migogoro iliyopo katika mashamba mengine 32 ya Karatu. Hata hivyo mkakati wa Serikali ni kuendelea kufuatilia mashamba yote ya uwekezaji yaliyopo Wilayani Karatu na kwingineko nchini ili kuhakikisha mashamba hayo yanaendelezwa na kuzalisha kwa maslahi ya nchi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Daniel.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ilituma Wizarani mara nyingi kwamba kuna

mashamba hayo aliyoyataja Mheshimiwa Naibu Waziri, kati ya mashamba 33 yanayoendelezwa kwa robo moja tu katika mashamba yale yote 33; lakini kwa kuwa shamba hili la Bendhu mmiliki wake alifariki na akamwachia mwanee ambayo yupo nchini Zimbabwe na baadaye wafanyakazi wale hawajaweza kulipwa muda wote tokea mmiliki yule aliyefariki namba moja na yule aliyeachiwa shamba hilo hajaweza kuonekana mpaka muda huu. Sasa ni lini majibu ya Serikali kwamba hili shamba la Bendhu wafanyakazi wale wote wanaweza kupata haki yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Waziri atakubaliana nami kwenda katika Jimbo la Karatu kuona mashamba haya 33 yote, ajionee kwamba haya mashamba hayaendelezwi. Kwa mfano katika Kata ya Oldeani hata mahali pa kuzika mtu hakuna kwa sababu mashamba yale yote yapo chini ya uwekezaji na wakati huo kutoka *Fireland* Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekuwa msitu mwingine baada ya *Fireland* ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro. Je, ni lini Waziri atafuatana na mimi kwenda katika Jimbo la Karatu kujionea mashamba haya hayaendelezwi katika majibu aliyotoa kwamba anaona mashamba haya yanaendelezwa? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Daniel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwenda karatu mimi na yeye tumeshakuwa na maongezi tutakwenda na tutapanga tarehe pamoja ambayo tutakwenda kutembelea, kwenda kuangalia hayo mashamba na matatizo ya wakulima wa vitunguu ambao wanakabiliana nayo. Pia kuhusu Shamba la Bendhu nimeshajibu kwenye swali la msingi Serikali sasa hivi hatuwezi kusema jambo lolote kwasababu jambo hili lipo mahakamani tunasubiri shauri hili liishe mahakamani *then* tunaweza kufanya *intervention*.

MWENYEKITI: Swali letu la mwisho na kwa Wizara ya Ujenzi, litaulizwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda.

Na. 484

Ujenzi wa Barabara ya Mkwiti - Amkeni

MHE. MAIMUNA S. MTANDA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mkwiti – Amkeni inayounganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara kupitia Mtama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mkwiti – Amkeni yenye urefu wa kilometa 74.23 inayounganisha Wilaya ya Tandahimba na Newala katika Mkoa wa Mtwara na Wilaya ya Lindi Vijijini mkoa wa Lindi unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi milioni 1,807.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa tatu ambapo jumla ya kilometa 2.8 zimekamilika kujengwa na kazi za ujenzi zinaendelea kwenye kipande chenye urefu wa mita 200. Wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukiendelea kutekelezwa kwa awamu, Wizara yangu itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maimuna.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante barabara ya kutoka Amkeni – Kitangali hadi Mtama yenye kilomita 74 ndiyo barabara pekee inayofungua mji wa Newala na maeneo mengine kuelekea Dar es Salaam hadi kuja huku Dodoma. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba fedha zitatengwa kwa awamu lakini ikumbukwe kwamba wilaya hii ni ya muda mrefu tangu 1952 hadi leo haina barabara ya uhakika. Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili barabara hii iweze kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na changamoto za ubovu wa hii barabara wafanyabiashara wengi wa usafirishaji wanakwama kupeleka vyombo vyao vya usafiri kwa hofu ya uharibifu wa vyombo vyao na wananchi wanateseka na usafiri kwa sababu ya ubovu wa barabara. Je, Serikali haioni kwamba inarudisha nyuma jitihada zake za ajira kupitia sekta zisizo rasmi hasa usafirishaji? Ahsante

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi barabara hii ni kweli ni ya muhimu sana kwa mkoa wa Mtwara ambayo inaunganisha mkoa wa Lindi. Lakini kwa kulitambua hilo Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD* inajenga maeneo korofi yote kwa kiwango cha lami na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba maeneo mengi korofi yamejengwa kwa kiwango cha lami na hata katika mwaka huu wa fedha tunaoendea kuna fedha imetengwa kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami yale maeneo yote korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, ambalo linafanana hili jibu la kwanza kwa sababu ya kutambua ule ubovu kwenye hii barabara ndiyo maana sasa *TANROAD*

mkoa wa Mtwara unafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika muda wote na kuhakikisha kwamba maeneo korofi yote yanawekewa lami ili barabara hii iweze kupitika muda wote wa mwaka ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika mwaka wa fedha huu 2021 Serikali ilisema imetenga bilioni 5 kwa ajili ya kujenga barabara ya kutoka Same Kisiwani mpaka Mkomazi kwa kiwango cha lami. Je, fedha hiyo itatolewa lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, jiandae Mheshimiwa Mtinga.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaboyoka Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema fedha hii kwa kujenga kwa kuanza kwa kiwango cha lami Same hadi Mkomazi ambapo tumetenga bilioni 5 fedha itaanza kutoka mara bajeti itakapoanza kutumika ya mwaka 2021/2022, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mtinga jiandae Mheshimiwa Sendeka.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa barabara hii ya Mkwiti – Amkeni inayounganisha mkoa wa Lindi na Mtwara tatizo lake linafanana kabisa na barabara ya Singida Simiyu inayoanzia Iguguno na kwa kuwa Serikali imevunja nyumba za wananchi wa Iguguno hivi karibuni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi barabara hii hasa kuanzia Iguguno mpaka Nduguti?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni barabara ambazo zitajengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano na itategemea na upatikanaji wa fedha hatuwezi leo tukaahidi kwamba itaanza mwaka ujao kwa sababu haijaingia kwenye mpango. Lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miaka inayokuja ya bajeti itaingizwa kwenye mpango ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami ikiwa ni kuanzia na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na hatimaye kujenga kwa kiwango cha lami ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sendeka, jiandae Mheshimiwa Hussein.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara inayotoka Arusha, Simanjiro, Kiteto, Kongwa umekamilika na ni ahadi ya muda mrefu ya ilani za uchaguzi kadhaa. Je, ni lini Serikali Sikivu ya CCM itaanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa?

MWENYEKITI: Ahsante maswali yale mafupi Mheshimiwa Waziri, jiandae Hussein jiandae Mulugo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sendeka Mbunge wa Simanjiro kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii aliyoitaja ni barabara muhimu sana hasa kwa mikoa ya Arusha Manyara na Dodoma na nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kati ya barabara ambazo ziko kwenye mpango na kwa

kuwa usanifu umeshakamilika Serikali inatafuta fedha ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami katika awamu ambayo ime...

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa barabara inajengwa Mheshimiwa Waziri kaa hapo, Mheshimiwa Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa barabara ya kutoka Busisi Nyang'wale kwenda Kahama imeahidiwa na viongozi wakuu wa nchi kujengwa kwa kiwango cha lami. Ni lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu na ujenzi wa barabara hiyo kuanza mara moja?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri majibu, jandae Mulugo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar Mbunge wa Nyang'wale kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni barabara ambayo katika ilani ya chama itafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika kipindi hiki. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute Subira fedha ikipatikana ya Serikali tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kama fedha itaruhusu basi tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mulugo, Mheshimiwa Chumi.

MHE. PHILIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, swali langu la nyongeza, barabara ya kutoka Mbalizi mpaka Mkwajuni sasa ni miaka 15 imekuwa ikiahidiwa na Waheshimiwa Marais wanaokuja kupiga kampeni kule Mheshimiwa Dkt. Kikwete alituhidi miaka 10 ikapita bila kujenga, Mheshimiwa Rais marehemu Mungu

amlaze mahali pema peponi Mheshimiwa JPM naye aliahidi...

MWENYEKITI: Usilete ufundi kwenye swali uliza swali moja kwa moja. (*Kicheko*)

MHE. PHILIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Waziri ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kutoka Mbalizi mpaka Mkwajuni kwa sababu nimekuwa nikiahidiwa miaka mingi? Na upembuzi yakinifu tayari umeshaiha kabisa naomba majibu.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Phillipa Mulugo Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa Mkoa wa Songwe lakini pia kwa wilaya ya Chunya na wilaya ya Songwe. Barabara hii imeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami lakini bado nimpe pole sana Mheshimiwa kwa sababu katika kipindi chote hiki ilikuwa haipitiki kwa sababu ya mvua lakini *TANROADS* mkoa wa Songwe ilifanya jitihada kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mulugo kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano kama ilivyoahidiwa na tunavyotekeleza ilani za viongozi wakuu wa Serikali barabara hii nayo itafanyiwa kazi kwa maana ya kujengwa kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyopatikana, ahsante.

MWENYEKITI: Ameshakuelewa Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi barabara ya Mafinga Mgololo ambayo ni kiungo muhimu sana cha uchumi katika uchumi wa Mufindi na Iringa imeahidiwa toka ilani ya uchaguzi 2005 ninauliza Serikali. Je, wakati jitihada za kujenga kwa kiwango

cha lami zinaendelea Serikali iko tayari kushughulikia na maeneo korofi kama vile Itulavanu, Mtili na pale mlima wa Kalinga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chami Mbunge wa Mafinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge hili nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Iringa aende akaangalie maeneo hayo korofi aweze kufanya tathmini ili yale maeneo korofi tuweze kutafuta fedha ili barabara hiyo iweze kutengenezwa maeneo korofi yaweze kupitika muda wote wa mwaka ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri barabara ya Kablu ya Yanga inashuka Jangwani mpaka Kawawa *Road* umeiona hali yake ilivyo sasa hivi hii barabara ya *TANROADS*? Ni barabara ya kwenu ya *TANROADS* kutoka Klabu ya Yanga unashuka Jangwani mpaka unakuja *Kawawa road*. Agiza mtu aende akatizame. (*Kicheko*)

Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha wageni waliopo jukwaa la Spika wageni 22 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni *Winners Group* kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na ndugu Suma Lwena na ndugu Faraja Mkini, karibuni Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wageni 17 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni kikundi cha sala na wanakwaya kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege ya Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Carlos Kidiru, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambao ni wanafunzi wa

Chuo Kikuu cha Dodoma UDOM wanaotoka Jimbo la Ushetu wakiongozwa na ndugu Mathias Maziku karibuni.

Wageni 30 wa Mheshimiwa Joyce Ndalichako ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimboni Kasulu mkoani Kigoma wakiongozwa na ndugu William Feketeke karibuni. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi Naibu Waziri wa Maji ambao ni wafanyabiashara na waandishi wa Habari kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na ndugu Michael Mbuza karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Deo Sangu ambao ni wafanyakazi wa *Uchumi Commercial Bank* kutoka mkoani Kilimanjaro ndugu Samwel Wado, ndugu Gasper Mlingi na ndugu Zakharia Dodo. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Deo Sanga ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha UDOM wanaotoka Jimbo la Kwela mkoani Rukwa wakiongozwa na ndugu Paul Kazimoto. Wageni 70 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango cha jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Salome Komba karibuni. *(Makofi)*

Wageni 6 wa Mheshimiwa Exaud Kigahe Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na mke wake ndugu Rehema Mponzi. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Francis Mtinga Mbunge ambao wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi na walimu kutoka Iramba mkoani Singida, wakiongozwa na ndugu Mohamed Imbele karibuni. Wageni 25 wa Mheshimiwa Deo Mwanyika ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka mkoani Njombe wakiongozwa na ndugu Lucas Mlote. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni Watoto wake kutoka Buchosa Mkoa wa Mwanza ndugu

Butongwa Shigongo, ndugu Tanzania Asteria na ndugu Kahabi Shigongo karibuni. Wageni 34 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanakwaya wa kwaya Sauti ya Jangwani kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato la Mkoani Shinyanga wakiongozwa na Mchungaji Stephano Bomani. *(Makofi)*

Wageni 48 wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Babati Mkoa wa Manyara wakiongozwa na ndugu Muye Tumaini karibuni. Wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Tadayo ambao ni wapiga kura wake kutoka Mwanga Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na ndugu Puyo Nzalayemisi. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Vwawa Mkoani Songwe wakiongozwa na Ndugu Justin Halinga. Wageni wanne wa Mheshimiwa Kabula Shitobela ambao ni familia yake kutoka Jiji la Dar es Salaam wakiongozwa na mtoto wake ndugu Cristell Maganga. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambaye ni Mpwa wake kutoka Benki ya NMB ya Jijini Arusha ndugu Faraja Luoga. Wageni wawili wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli Mbunge ambao ni viongozi wa CCM kutoka Segerea Jijini Dar es Salaam ndugu Nuru Chalamila na ndugu Fatma Selega. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Siligas Ngura ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Emmanuel Mathias, (MC Pilipili). Wageni watano wa Mheshimiwa *Engineer* Samuel Hhayuma Mbunge ambao ni wafanyabiashara kutoka Hanang Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Clementini Fisoo. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Alfred Kimea ambao ni wanafunzi wa Chuo cha CBE kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Neema Issangaya. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo mgeni kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye amekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake ndugu Aisha Nassoro.

Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kama mlivyotangaziwa hapo awali kutakuwa na punguzo (*offer*) maalum ya kutembelea eneo la hifadhi ya Ngorongoro kuanzia tarehe 30 Juni baada ya kumaliza Bunge hadi tarehe 2 Julai kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani.

Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kwenda kutembelea eneo la hifadhi ya Ngorongoro mnaombwa mkajiandikishe na kupata utaratibu wa malipo kwenye banda la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro lililopo viwanja vya Bunge eneo la maonesho.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kutakuwa na semina na uzinduzi kwa Wabunge wote kama ifuatavyo. Semina *Sports betting* siku ya Alhamisi tarehe 24 Juni saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa.

Semina ya Mfuko wa Barabara na umuhimu wa matengenezo ya barabara nchini siku ya Ijumaa tarehe 25 saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa.

Semina ya Mkakati wa utekelezaji anuani za makazi *post code* nchini tarehe 28 Juni katika ukumbi wa Msekwa saa saba mchana. Uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 siku ya Jumanne tarehe 29 Juni saa 4 katika ukumbi wa Mkutano wa Jakaya Kikwete Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnaombwa kwa leo kutakuwa na *caucus* kwenye ukumbi wa Msekwa saa moja jioni ni muhimu sana wote muhudhurie.

Meneja *Bunge Sports* Seif Gulamali anapenda kuwatangazia Bunge kuwa Bonanza la *NMB* lililokuwa lifanyike

Jumamosi tarehe 26 Juni halitafanyika tena hivyo mtataarifiwa pindi litapokamilika.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021
(The Finance Bill, 2021)

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 *(The Finance Act, 2021)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati yako ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Kamati ya Bunge kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili kuuboresha Muswada huu. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni tarehe 22 Juni, 2021.

Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na *TRA* kwa kuandaa Muswada huu pamoja na

marekebisho yake, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 niliyowasilisha Bungeni tarehe 10 Juni mwaka huu. Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho sheria 22 zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kurekebisha viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali ili kuboresha taratibu za ulipaji na ukusanyaji wa kodi, kuongeza udhibiti wa mapato na matumizi ya baadhi ya taasisi za Serikali, kupunguza kodi kwenye mapato ya ajira na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zifuatazo ni sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho:-

- (i) Sheria ya Makampuni, Sura 212;
- (ii) Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306;
- (iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
- (iv) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134;
- (v) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41;
- (vi) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura 178;
- (vii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- (viii) Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289;
- (ix) Sheria ya Kodi ya Usajili wa Magari, Sura 124;
- (x) Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura 437;
- (xi) Sheria ya Udhibiti wa Ajira kwa Raia wa Kigeni, Sura 436;
- (xii) Sheria ya Bandari, Sura 166;
- (xiii) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano, Sura 306;
- (xiv) Sheria ya Wakala wa Meli, Sura 415;
- (xv) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418;
- (xvi) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220;
- (xvii) Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 189;
- (xviii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438;

- (xix) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399;
- (xx) Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura 408;
- (xxi) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; na
- (xxii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya Muswada. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Ishirini na Tano, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambayo ni tarehe 1 Julai, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Makampuni, Sura 212 ili kuweka masharti ya mpito kwa ajili ya hisa fichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, kama ilivyorekebisha inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306 kwa kuongeza kifungu cha 164A ili kuanzisha tozo kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Lengo la hatua hii ni kupata fedha za kugharamia maeneo mahsusikiwemo maji, barabara, umeme, bima ya afya kwa wote na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebisha, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kama ifuatavyo: -

(i) Kurekebisha kifungu cha 124 ili kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye pikipiki zilizotumika kwa zaidi ya miaka mitatu zinazoingizwa nchini zinazotambuliwa kwa *HS Heading* 87.11. Lengo la hatua hii ni kudhibiti uingizaji wa pikipiki chakavu ili kulinda mazingira.

(ii) Kurekebisha Jedwali la Nne ili:-

(a) kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini kutoka Sh.765 kwa lita za sasa hadi Sh.620 kwa lita. Lengo la hatua hii ni kuchochea kilimo cha shayiri hapa nchini.

(b) Kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa kwa asilimia 20 kwenye vinywaji vikali kwa kuwa vina kiwango kikubwa cha kilevi ili kuwa na uwiano na viwango vya kodi kati ya vinywaji vikali na bia. Jambo hili liliongelewa na Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo tulimsikia Mheshimiwa Reuben, Mbunge wa Handeni pamoja na Wabunge wengine Mheshimiwa King na Santiel Kirumba waliokuwa wamechangia kwa nyakati tofauti.

(c) Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nyuzi na kamba za plastiki zinazoingizwa kutoka nje ya nchi au kuzalishwa hapa nchini zinazotambuliwa kwa *Heading* 55.11 na 56.07 isipokuwa zile zinazotumika kwenye uvuvi zinazotambulika kwa *HS Code* 5607.50.00. Lengo la marekebisho haya ni kulinda mazingira na kuchochea uzalishaji na matumizi ya bidhaa za katani zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 13 cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kwa kuongeza kifungu kipya cha 13B, ili kuruhusu Serikali kudhamini kampuni au taasisi yoyote kukopa kiasi kisichozidi thamani ya Hisa za Serikali kwenye kampuni/taasisi inayotekeleza mradi husika baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41 kama ifuatavyo: -

(i) Kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (*Gaming tax on winnings*) kutoka asilimia 20 hadi 15 kwenye michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (*sports betting*).

(ii) Kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha kwa asilimia 10 ya mapato ghafi kwenye michezo ya kubahatisha inayoendesha kwa kompyuta na michezo ya kubahatisha iliyo chini ya majaribio.

(iii) Kupitia Jedwali la Marekebisho, napendekeza kufuta pendekezo nililowasilisha kupitia Hotuba ya Bajeti la kuongeza kiwango cha Kodi katika michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (*GGR*) kutoka asilimia 25 ya mauzo ghafi hadi asilimia 30 ya mauzo ghafi. Hata hivyo, pamoja na mapendekezo haya, bado asilimia 5 kwenye kodi hii itawasilishwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa ajili ya kuendeleza michezo nchini kama Waziri mwenye sekta Mheshimiwa Innocent Bashungwa alivyokuwa amependekeza na Wabunge wengi kulipendekeza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebisha inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 7 cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura 178 ili kuweka masharti kwa Bodi ya mikopo kutoweka ada au tozo yoyote ikiwemo *Value Retention Fee* kwenye mikopo ya wanafunzi kabla ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Elimu baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha. Hatua hii ina lengo la kuzuia utozaji holela wa ada kwenye mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na ili kuwapunguzia mzigo wa ulipaji wa mikopo kwa wanafunzi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane kama ilivyorekebisha pamoja na mambo mengine inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo: -

(i) Kurekebisha kifungu cha 10 ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutoa msamaha wa kodi kwa kutoa tangazo la *GN* bila sharti la kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwa miradi inayotekelezwa na wafadhili (fedha za misaada) kupitia mikataba ya misaada na mikopo iliyoingwiwa baina ya nchi hizo na Serikali yenye kifungu

kinachoruhusu msamaha wa kodi ya mapato. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa kwa misaada na mikopo ambayo utekelezaji wake umekuwa ukichelewa kusubiri ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

(ii) Kurekebisha kifungu cha 65N ili kuwezesha ukokotoaji wa gharama za uchakavu kwa kiwango maalum cha asilimia tano kwenye gharama za mali za ujenzi wa bomba la mafuta (*EACOP*).

(iii) Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yanayohusisha mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji na ununuzi wa mazao.

Aidha, pendekezo hili halitahusisha wakulima wadogo na wale wanaouza mazao yao kwenye masoko ya msingi (*AMCOS*) na vyama vya ushirika vya wakulima.

(iv) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza Kodi ya Mapato ya Ajira (*Pay As You Earn*) kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8.

(v) Kurekebisha Jedwali la Pili ili kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwenye hatifungani za Serikali zenye miaka isiyopungua mitatu zilizoordheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam kuanzia tarehe 1 Julai, 2021.

Aidha, kufuatia mashauriano baina ya Serikali na Kamati ya Bunge ya Bajeti, Serikali imeondoa pendekezo la kutoza Kodi ya Mapato kwa asilimia 3 ya mapato ghafi kwa wachimbaji wa madini wadogo, ili kutoa fursa ya kufanya utafiti zaidi kuhusu namna bora ya kuwatoza kodi wachimbaji hawa bila kuathiri ukusanyaji wa mapato mengine. Jambo hili liliongelewa vizuri na Mheshimiwa Waziri mwenye sekta katika vikao ambavyo tulikutana Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Fedha na kama ambavyo lilienda likakubalika kwenye mashauriano ya Kamati ya Bajeti pamoja na Wizara hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289 kama ifuatavyo: -

(i) Kurekebisha kifungu cha 16 ili kutoza Kodi ya Majengo kwa kiwango cha Sh.1,000/= kwa mwezi kwenye nyumba za kawaida zenye mita moja. Aidha, kiwango cha Sh.5,000/= kwa mwezi kitatozwa kwa kila ghorofa au *apartment* zenye mita moja. Ukusanyaji wa kodi hii utafanywa na *TANESCO* kupitia ununuzi wa umeme. Aidha, kwa nyumba ambazo hazitumii umeme wa *TANESCO*, kodi hiyo itakusanywa kwa utaratibu unaotumika hivi sasa kwa kutumia Ofisi zetu za Serikali za Mitaa.

(ii) Kuweka utaratibu wa kurejesha asilimia 15 ya makusanyo ya Kodi ya Majengo kwa Halmashauri na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hoja kutoka kwa Wabunge mbalimbali, Serikali imeondoa Sehemu ya Kumi ya Muswada inayohusu marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 yaliyokuwa yanapendekeza kubainisha mazingira ambayo kampuni inayolipa tozo ya huduma haitawajibika kulipa tozo ya uzalishaji. Jambo hili lilisemwa kwa hisia kali na Mbunge wa Korogwe Mheshimiwa Mnzava pamoja na Mheshimiwa Chumi pamoja na Wabunge wengine wanaotoka kwenye maeneo ambayo yalikuwa yanaathiriwa na mapendekezo yale. Lengo la hatua hii ni kutoa fursa ya kufanya utafiti zaidi kuhusu namna bora ya ukusanyaji wa mapato hayo na kuondoa uwezekano wa kampuni kulipa tozo mara mbili na pia kuondoa uwezekano wa baadhi ya Halmashauri kupoteza mapato ya kugharamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao ambayo tayari walikuwa wameshaindaa na imepita kwenye taratibu zote za uandaaji wa bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Moja kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Usajili wa Magari, Sura Na.124 ili kupunguza ada ya usajili wa magari kwa namba

binafsi kutoka Sh.10,000,000 hadi Sh.5,000,000 kila baada ya miaka mitatu. Jambo hili liliongewa kwa hisia kali na Wabunge na wengine walipendekeza uwezekano wa kuweka namba maalum kwa ajili ya Wabunge. Nikuahidi wewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba jambo hili litafanyiwa kazi katika marekebisho mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Mbili kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura 437 kwa kuongeza kifungu kipya 46A ili kuweka tozo katika kila muamala wa kutuma au kutoa fedha kwa kiasi kitakachotofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha itakayotumwa au kutolewa. Aidha, pendekezo hili linalenga kutoza tozo ya Sh.10 hadi Sh.10,000 katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa. Kiasi cha tozo kinatofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha unaotumwa au kutolewa. Aidha, Waziri mwenye dhamana kwa kushauriana na Waziri wa Mawasiliano atatunga Kanuni zitakazoweka utaratibu wa utozaji na ukusanyaji wa tozo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nilihakikishie Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania kwamba jambo hili halitaathiri shughuli ya utumiaji wa simu zetu kwa masuala haya ya kifedha ambayo imewaweka wananchi wengi kwa sababu Serikali imepanga kutumia fedha nyingi kwenye shughuli za maendeleo kwa maana hiyo kutakuwepo na ukwasi mwingi mtaani na hivyo wananchi wataweza kutumiana fedha bila kupunguza matumizi ya simu katika shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Tatu kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 16 katika Sheria ya Udhibiti wa Ajira kwa Raia wa Kigeni, Sura Na. 436 ili kuweka adhabu ya kiasi cha Sh.500,000/ = kwa kila mwezi kwa mwajiri aliyeajiri raia wa kigeni na kuchelewa au kushindwa kuwasilisha ritani za kila mwezi, zenye taarifa za raia wa kigeni aliyeajiriwa ikiwemo taarifa zao za mishahara kwa Kamishna wa Kazi. Lengo la pendekezo hili ni kuhimiza uwajibikaji wa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Nne, Kumi na Tisa na Ishirini kama zilivyorekebishwa, zinapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Bandari, Sura Na. 166, Sheria ya Wakala wa Meli, Sura Na. 415 na Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura Na. 172 ili kuweka sharti kwa mapato ya Mamlaka ya Bandari, TCRA na TASAC kuingizwa kwenye akaunti maalum zitakazofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, taasisi hizi zitapatiwa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na baada ya kupata ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kama tulivyosema, haya yatafanyika taasisi hizi zikiwa zimeshapata fedha za mkupuo za miezi miwili na kuanza kupata kwa mwezi mmoja mmoja ili kutokuathiri shughuli zao za kila siku na kutokukwamisha shughuli zao ambazo ni za dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Tano kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura Na. 418 kama ifuatavyo:-

(i) Kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na uwezo wa kisheria wa kukagua mashirika yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni na ambayo Serikali ina umiliki wa hisa wa zaidi ya asilimia hamsini.

(ii) Kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha Bungeni majibu kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye kikao kinachofuata cha Bunge baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa yake badala ya utaratibu wa sasa ambapo taarifa zote huwasilishwa kwa pamoja katika kikao kimoja cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Sita kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Na. 220 kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha kifungu cha 4A(a) ili kuelekeza fedha zitakazokusanywa kutokana na ongezeko la ushuru wa barabara na mafuta la Sh.100 kwa aina zote za mafuta kwa

ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara zilizo chini ya *TARURA*. Kwa hiyo, fedha hizi zitakazopatikana zile za nyongeza hazigawanywi, zenyewe zinakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA* kwa sababu chanzo hiki kilikuja baada ya mjadala na hisia kubwa za Waheshimiwa Wabunge kutaka *TARURA* iongezewe fedha ili kuweza kutekeleza miradi ya barabara na kufungua vijiji na maeneo yetu ambayo hayapitiki kwa kukosa barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbili kuongeza Ushuru wa Barabara kwa shilingi 100/= kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli kwa maelezo hayo niliyoyatoa kwamba itakwenda kwenye kutunisha Mfuko wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, natoa ridhaa kwa Waziri anayehusika na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoa kanuni ambayo itapunguza tozo zilizokuwa zinatozwa kwa ajili ya masuala ya Zimamoto kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Ilala, Mwenyekiti makini kabisa wa Bunge alivyolipigania jambo hili katika hotuba yake na kuwatetea wananchi wake ambao walikuwa wanatozwa gharama kubwa ambazo pia zilikuwa hazikusanyiki. Kwa kuwa mamlaka ya kupunguza yako ndani ya Waziri mwenye dhamana kwa kupitia Kanuni, Wizara ya Fedha inaridhia Waziri mwenye dhamana kuweza kufanya Kanuni hizo sambamba na Waziri wa Kilimo pamoja na Mifugo kwenye maeneo yao ambayo wataona yanahitaji marekebisho ya kanuni ili kuweza kuboresha uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi na Saba kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho kwenye Jedwali la Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 189 ili kuhuisha viwango vilivyopo vya sasa sambamba na mfumuko wa bei kwani viwango vilivyopo ni vya muda mrefu tangu mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mashauriano baina ya Serikali na Kamati ya Bajeti, Sehemu ya Kumi na Nane inayohusu marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 yamefutwa ili kutoa fursa kwa Serikali kukamilisha

mchakato wa marekebisho ya Sheria hii kwa ujumla wake. Jambo hili limekubalika pia na Wizara zinazo husika tukiwa tumekaa na Mheshimiwa Mwambe anayesimamia Wizara hiyo, pamoja na Naibu Wake ili tuweze kuikamilisha sheria yote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Ishirini na Moja pamoja na mambo mengine inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Kodi, kurahisisha taratibu za ukusanyaji kodi na faini na kuondoa sharti kwa mlipa kodi kulipa sehemu ya kodi kwanza ili aweze kuwasilisha pingamizi dhidi ya uamuzi wa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na makadirio ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili pia liliongelewa kwa kiwango kikubwa na Waheshimiwa Wabunge na Serikali imeshauriana na Kamati na kuona jambo hili linaweza kuboreshwa likafanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Ishirini na Mbili inapendekeza marekebisho kwenye Kifungu cha 10 katika Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399 ili kuhuisha orodha ya wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato wanaowakilisha Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Ishirini na Tatu inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 22 katika Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura 408 ili kuanzisha utaratibu wa kufanya usuluhishi wa migogoro ya kikodi nje ya Mahakama. Lengo ni kuongeza kasi ya utatuzi wa migogoro ya kodi na kupunguza mlundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fedha nyingi sana zimepaki katika maeneo haya na inapotokea mashauri haya hayafanyiki, tunaendelea kukosa fedha na tunafanya kichaka, mwingine anaona kama hataki kulipa hiyo fedha ni bora akaipaki kule halafu kadri inavyochelewa kusikilizwa maisha mengine huku yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Ishirini na Nne kama ilivyorekebisha pamoja na mambo mengine, inapendekeza marekebisha ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

(i) Kurudisha utaratibu wa kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kutumika Tanzania Zanzibar. Lengo la hatua hii ni kuwa na ufanisi wa marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Jambo hili limeongelewa na Wabunge kwa hisia kali Wabunge wanaotoka upande wa pili wa Muungano, yaani Tanzania Zanzibar pamoja na kuungwa mkono na Wabunge wenzao ambao wako katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara pamoja na Serikali imesikiliza mapendekezo yao na ufanisi wake utakuwa mkubwa kwa sababu tutautekeleza kama ilivyopendekezwa.

(ii) Kuwezesha miradi inayogharamiwa na fedha za Serikali na fedha za wafadhili; kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kupitia kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania badala ya utaratibu wa awali wa kuwasilisha kwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya kupata ridhaa ya kutoa Tangazo la Serikali (GN) kwa kila mradi. Lengo la hatua hii ni kurahisisha na kuharakisha utoaji wa misamaha badala ya utaratibu wa sasa unavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limeongelewa sana na Wabunge na Mheshimiwa Waziri wa Maji muda mwingi sana alikuwa akifika Wizarani kwa ajili ya kufuatilia GN jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa shughuli hizo.

(iii) Kuzitambua bidhaa za mtaji zilizomo kwenye Sura ya 84, 85 na 89 katika Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kwa bidhaa za mtaji zinazostahili kupata vivutio au ahirisho la mapato ya Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(iv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa na huduma zitakazoingizwa au kununuliwa hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Bomba la kusafirisha

mafuta ghafi; kutoa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe ya kubebea maziwa inayotambulika kwa *H.S Code* 7310.29.90, 7310.10.00 na 7612.90.90;

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ghafi yanayotambulika kwa *H.S Code* 2709.00.00 kwa lengo la kutoa unafuu kwa mlaji ikiwemo Kampuni ya uendeshaji wa bomba la mafuta;

(vi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini na makinikia yatakayolingizwa nchini kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuongezewa thamani au kuuzwa kwenye masoko ya madini yanayotambulika hapa nchini. Lengo la pendekezo hili ni kuviwezesha viwanda vyetu vya uchenjuaji vilivyoanzishwa hapa nchini kupata malighafi ya kutosha kwa ajili ya uchakataji na hatimaye kuongeza ajira na mapato ya Serikalini;

(vii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyumba vya ubaridi (*cold rooms*) vinavyotambuliwa kwa *H.S Code* 9406.10.10 na 9406.9010. Lengo la msamaha huu ni kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mboga mboga na maua nchini ili kuchochea kilimo;

(viii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Nyasi Bandia zinazotambulika kwa *HS Code* 5703.30.00 na 5703.20.00 kwa ajili ya Viwanja vya Mpira vilivyoko kwenye Manispaa na Majiji. Msamaha huo utahusisha ridhaa kutoka Baraza la Michezo la Taifa kama Waheshimiwa Wabunge walivyoshauri kama wakiongozwa na Mheshimiwa Chumi;

(ix) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja za mkononi zenye *HS Code* kama nilivyozorodhesha, 8471.30.00 au 8517.12.00 na *modems (HS Code* 8517.62.00 au 8517.69.00); na

(x) Kuondoa sharti la kuwataka wenye viwanda vya kutengeneza madawa ya binadamu au mifugo kuchapisha majina ya viwanda husika kwenye vifungashio vya madawa

vinavyonunuliwa au kuingizwa nchini ili kuwawezesha wazalishaji husika kupata msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani. Aidha, wazalishaji husika watalazimika kupata ridhaa ya Wizara ya Afya au Taasisi inayohusika na udhibiti wa uzalishaji wa madawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Ishirini na Tano inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82 kama ifuatavyo:-

(i) Kupandisha kiwango cha chini cha idadi ya waajiriwa wanaostahili kulipiwa kodi kutoka 4% ya sasa hadi 10%;

(ii) Ibara ya 88 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19 ili kufuta tozo ya Elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi kwa hospitali zinazomilikiwa na taasisi za kidini kwa kuwa taasisi hizi zimekuwa zikiisaidiana sana na Serikali katika kufikisha huduma za afya hata kwenye maeneo ambayo Serikali haijaweza kupeleka huduma kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika Hotuba ya Bajeti ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021, zitatekelezwa na Mawaziri husika kwa kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali kama nilivyosema (*Government Notices*) kwa mujibu wa matakwa ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hoja ambazo zilitolewa na Wabunge ambazo hatukuweza kuzitaja katika majibu tutaenda kutekeleza; tumepokea kama ushauri na nyingine ni hoja ambazo zinahitaji utekelezaji na nyingine zinahitaji kufanyiwa kazi zaidi, tutaendelea kuzifanyia kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba tunatekeleza haya tuliyoyapokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine tutaendelea kutoa miongozo kwa mujibu wa sheria zetu za nchi ili kuweza kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unafanyika kama ilivyokuwa imekusudiwa. Rai yangu kwa Waheshimiwa

Wabunge, tutakapomaliza Bunge fedha hizi tunazotarajia kuzipeleka kule kwenye Serikali za Mitaa ni nyingi, basi pawe na uwazi, wataalam wetu wawashirikishe Wabunge kwa uwazi, kama Mheshimiwa Mama Malecela alivyokuwa ameshauri wakati anachangia ili Wabunge waweze kushiriki kwenye vipaumbele vya miradi ambayo wanataka fedha hizo zitumike, lakini pia waweze kufuatilia kikamilifu jinsi fedha hizo zinatavyotumika kwa sababu wao ni Wawakilishi wa wananchi na wameshiriki katika kupangilia fedha hizi hapa tukiwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaongea na Wizara zote tuweze kutoa miongozo hiyo kwa wataalam wetu ili isiwe jambo la hisani kwa Mbunge kujua fedha zilizokuja kwa ajili kutekeleza miradi jimboni kwake, iwe ni jambo ambalo ni la lazima, fedha zikishafika Wabunge wote wajulishwe kwamba fedha mlizokuwa mnapigania kule zimeshakuja, Wabunge wote wa Majimbo na wa Viti Maalum wajue ili waweze kufuatilia miradi imeshatekelezwa katika mikoa yao na katika wilaya ili tunavyokuja huku tuweze kufanya tathmini ya hiki tulichokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa wenzenu huko Wizarani, tutasimamia uwazi huo na tutamtuma Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kufuatilia siyo tu kwa kalenda ya kawaida, hata kwa wakati wowote ambapo ataona kuna fedha anatakiwa kuzifuatilia aweze kuona matumizi yake yamefanyika kama ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hizi fedha ambazo tunazisemea hapa ni zenu, na wawakilishi wenu ni hawa, kwa hiyo, na ninyi wote fuatilieni ili fedha ziweze kutumika kama ilivyokusudiwa na tuweze kuona thamani halisi ya fedha ambazo tumezitoa kwa walipa kodi na kuweza kuona faida kwenye miradi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisha ninayopendekeza ni utekelezaji wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kwa hiyo, naomba

Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri *wind-up*.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kulwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake kama ilivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, alipokuja Mheshimiwa Rais Samia kuhutubia Bunge, alizungumzia namna ya kuilea *ATCL* na kuondoa tozo ambazo *ATCL* zinalipa sasa hivi, humu hamna.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe nilipokee hilo kwa sababu ndiyo mjadala huu utaendelea ili tuweze kushauriana Serikalini pamoja na Kamati husika na tutakapokuwa tunajibu michango itakayotolewa...

MWENYEKITI: Eee, maana yake Mheshimiwa Waziri, *National Career* zote duniani hazilipi *local taxes*. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipokea.

MWENYEKITI: ...na *landing fees, navigation fees, parking fees* zote wanalipa *ATCL*; na kwenye *contingent liability* wanapata matatizo. Haya nashukuru Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipokea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, toa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2021 (THE FINANCE BILL, 2021) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 (**The Finance Act, 2021**) pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili**.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini** kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili kuuboresha Muswada huu.
3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni tarehe 22 Juni, 2021. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango na TRA kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.
4. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Muswada huu ni kufazinyia marekebisho sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa

mwaka wa fedha 2021/2022 niliyowasilisha Bungeni tarehe 10 Juni mwaka huu.

5. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria **Ishirini na mbili** zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kurekebisha viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali ili kuboresha taratibu za ulipaji na ukusanyaji kodi, kuongeza udhibiti wa mapato na matumizi ya baadhi ya Taasisi za Serikali, kupunguza kodi kwenye mapato ya ajira na kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

6. **Mheshimiwa Spika**, zifuatazo ni Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho:-

- i. Sheria ya Makampuni, Sura 212;
- ii. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306;
- iii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
Part XI of the Bill proposes to amend the Motor Vehicle (Tax on Registration and Transfer) Act, Cap 124, whereby the First Schedule to the Act is amended by reducing motor vehicle registration tax for personalised identification from ten million shillings to five million shillings in order to reduce cost for personalised registration and increase Government revenue.

Part XII of the Bill proposes to amend the National Payment Systems Act, Cap. 437 by imposing a levy on mobile money transfer transactions depending on the value of the money sent or withdrawn in order to raise funds for implementation of development and strategic projects.

Part XIII of the Bill proposes to amend the Non-Citizens (Employment Regulation) Act, Cap. 436, whereby sections 16 and 20 are proposed to be amended in order to impose penalty to employers for late submission or failure to submit to the Labor Commissioner returns on employment of non-citizens. The objective of the amendment is to encourage timely submission of returns by employers and deter non-compliance.

Part XIV, Part XIX and Part XX of the Bill propose to amend the Ports Act, Cap. 166, the Tanzania Communications Regulatory Authority Act, Cap. 172 and the Tanzania Shipping Agencies Act, Cap. 415 so as to require all funds and revenues of the Tanzania Ports Authority, the Tanzania Communications Regulatory Authority and the Tanzania Shipping Agencies Corporation to be collected through GePG and deposited at the Bank of Tanzania.

Part XV of the Bill proposes to amend the Public Audit Act, Cap. 418 for the purpose of mandating the Controller and Auditor General to audit corporations in which the Government has shares, irrespective of the amount of shares. Further, section 38 is amended to enable the Minister to submit to the National Assembly responses to the Controller and Auditor General's report after the Controller and Auditor General has laid his report before the National Assembly.

Part XVI of the Bill proposes to amend the Road and Fuel Tolls Act, Cap. 220, whereby section 4A and the Second Schedule are amended with a view to increase fuel levy to support the construction and maintenance of rural roads.

Part XVII of the Bill proposes to amend the Stamp Duty Act, Cap. 89 by amending the Schedule in order to review the prescribed rates to reflect the current value of Tanzania shillings.

Part XVIII of the Bill proposes to amend the Tanzania Investment Act, Cap. 38 by introducing an advisory committee of the National Investment Steering Committee for purposes of enhancing effective implementation of the responsibilities of the Committee.

Part XXI of the Bill proposes to amend the Tax Administration Act, Cap. 438, whereby section 22 and the Third Schedule are amended in order to introduce a requirement to employees to apply for a Taxpayer Identification Number so as to facilitate proper accounting of tax on employment income. Further, sections 28A, 28B, 28C and 28D are amended in order to enhance effective implementation of the functions of the Tax Ombudsman's office.

It is further proposed to amend sections 29 and 85 to impose a requirement for submission of official translation of documents by taxpayers which are not in official language. Section 35 is amended in order to require every taxpayer who maintains data in electronic form to maintain a primary data server within the United Republic for effective accessibility of the information.

The Bill further proposes to amend sections 44, 51 and 74 to expand the scope of persons from whom the Commissioner General may access information, to enable objection of non assessment tax decision without payment of tax deposit and empower the Commissioner to demand a tax which was erroneously refunded. Section 56 is amended to enable payment of property rate at the time of payment for electricity with a view to simplify collection of property rate and reduce compliance cost.

Part XXII of the Bill proposes to amend the Tanzania Revenue Authority Act, Cap. 399 whereby section 10 is amended to review the list of Board members representing the Ministry responsible for finance.

Part XXIII of the Bill proposes to amend the Tax Revenue Appeals Act, Cap. 408 whereby section 22 is amended in order to introduce mediation procedure at any stage of the proceedings of the tax dispute resolution with the aim of speeding up resolution of tax dispute and reducing backlog of cases.

Part XXIV of the Bill proposes to amend the Value Added Tax Act, Cap. 148, whereby sections 3 and 55A are amended in order to enable the refund of VAT between Mainland Tanzania and Tanzania Zanzibar for goods purchased in one part of the Union by persons registered for VAT and consumed in another part of the Union. The object of the amendment is to increase efficiency of the refund of VAT between the two parts of the Union.

Section 6 is proposed to be amended to empower the Commissioner General to grant Value Added Tax exemption on importation or supply of goods and services for implementation of strategic projects with a view to increase efficiency in administration and monitoring of VAT exemptions. Section 6 is further amended to exempt VAT on importation by or supply of goods or services to a non-governmental organisation on implementation of projects through agreement with the Government of the United Republic which provides for exemption.

Section 11 is proposed to be amended to harmonise the definition of capital goods available in various tax laws for the purpose of preventing loss of Government revenue. Section 59 is proposed to be amended to allow zero rating of transportation of crude oil through an international pipeline and incidental services.

The Schedule is amended to exempt VAT on importation of smart phones, tablets, modems, aluminium and stainless-steel milk cans, crude oil, minerals and mineral concentrates, Contactless Smart Cards and Consumables, cold rooms and artificial grass for football pitches located in city council and to remove VAT exemption on solar lights.

Part XXV of the Bill proposes to amend the Vocational Education and Training Act, Cap. 82, whereby section 14 is amended by introducing a rate of 0.4 percent to individual employers engaged in small scale mining operations and increase the number of employees for the purpose of payment of service development levy in order to reduce the burden of levy for employers with fewer employees. Further, section 19 is amended to exempt religious health institution from paying levy with a view to reduce operational cost.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Ishirini ambapo Sehemu ya Kwanza inajumuisha jina la Muswada na tarehe ambayo Sheria itaanza kutumika.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Makampuni, Sura 212. Vifungu vya 85, 86 na 117 vinapendekezwa kurekebisha ili kuondoa dhana ya hisa fichi. Vifungu hivi vimerekebisha ili kuzuia utoaji wa hisa fichi na kuweka masharti ya mpito kwa ajili ya hisa fichi ambazo zimekwishatolewa. Lengo la marekebisho haya ni kuweka uwazi wa wanufaika wa hisa fichi na kudhibiti utoaji na uhamishaji wa hisa fichi.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306 kwa kuweka tozo kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji ili kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na miradi ya kimkakati.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Jedwali la Nne linarekebisha ili kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia kumi kwenye kamba na nyuzi za plastiki zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazolingizwa kutoka nje ya nchi isipokuwa kamba zinazotumika kwenye uvuvi kwa lengo la kutunza mazingira na kuchochea matumizi ya kamba za mkonge zinazozalishwa hapa nchini. Jedwali la Nne linarekebisha kwa kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali kwa asilimia 30 ili kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, marekebisho haya yanakusudia kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri inayozalishwa hapa nchini kwa lengo la kuchochea kilimo cha shayiri.

Kifungu cha 124 kinapendekezwa kurekebisha kwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye pikipiki zilizotumika zenye umri wa zaidi ya miaka mitatu zinazolingizwa nchini kwa lengo la kudhibiti uingizaji wa pikipiki chakavu na kulinda mazingira. Vilevile, kifungu hiki kinarekebisha ili kuwajumuisha watoa huduma wa malipo ya miamala ya simu waliosajiliwa chini ya Sheria ya Mifumo ya Malipo.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kwa kurekebisha kifungu cha 13 ili kuruhusu Serikali kudhamini kampuni au taasisi yoyote kukopa kiasi kisichozidi thamani ya hisa za Serikali ya Tanzania kwenye kampuni au taasisi inayotekeleza mradi baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41 ambapo kifungu cha 31A kinarekebisha ili kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi kwa lengo la kuhamasisha wachezaji kucheza michezo ya ndani badala ya michezo ya nje. Pia, Jedwali la Pili linarekebisha ili kuongeza kiwango cha kodi katika michezo ya ubashiri kwa mapato ghafi na kuweka kiwango cha kodi cha asilimia 10 kwa michezo ya kubahatisha inayochezesha kwa njia ya kompyuta na bidhaa za michezo ya kubahatisha zinazotolewa leseni kwa mujibu wa kifungu cha 51 ili kuongeza mapato ya Serikali.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178, ambapo kifungu cha 7 kinarekebishwa kwa kuweka masharti ya kupata idhini ya Waziri na utangazaji katika Gazeti la Serikali pale ambapo Bodi ya Mikopo itatumia mamlaka yake ya kuweka vigezo na masharti ya utoaji wa mikopo na misaada kwa wanafunzi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usimamizi wa mamlaka ya Bodi kuweka masharti ya utoaji wa mikopo.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 ambapo kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi bila kuhitaji ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwenye miradi inayotekelezwa na wafadhili wa maendeleo kwa lengo la kuharakisha utekelezaji wa miradi husika. Vilevile, vifungu vya 4, 79 na 84 vinarekebishwa ili kuweka utaratibu maalum wa utozaji wa kodi ya mapato kwa walipa kodi binafsi wadogo ambao wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini. Aidha, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 65A ili kuwezesha ukototaji wa gharama za uchakavu kwenye gharama za mali za ujenzi wa bomba la mafuta. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha gharama za uchakavu na muda wa matumizi wa bomba la mafuta.

Vilevile, inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 83B ili kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 2 kwa taasisi na makampuni ya nchini yanayojishughulisha na ununuzi na usindikaji wa mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi yatakapokuwa yanafanya malipo kwa wauzaji wa mazao husika. Aidha, pendekezo hili halitahusisha wakulima wadogo na wale wanaouza mazao yao kwenye masoko ya msingi (AMCOS) kwa lengo la kuweka usawa katika utozaji wa kodi za mazo ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Aidha, Jedwali la Kwanza linarekebishwa ili kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya ajira kwa wafanyakazi wenye kima cha chini cha mshahara kutoka asilimia 9 mpaka asilimia 8 kwa lengo la kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inakusudia kurekebisha Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289, ambapo kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebisha kwa kuongeza kodi ya majengo ili kuendana na mfumo wa makusanyo unaopendekezwa. Aidha, kifungu cha 31A kinarekebishwa ili kuweka utaratibu wa kurejesha 15% ya makusanyo ya kodi ya majengo kwenda mamlaka za serikali za mitaa.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inakusudia kurekebisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kwa lengo la kubainisha mazingira ambayo kampuni iliyolipa tozo ya huduma haitawajibika kulipa tozo ya uzalishaji ili kutatua mgongano uliojitokeza katika tafsiri ya kifungu hicho.

Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Usajili wa Magari, Sura 124, ambapo Jedwali la Kwanza linarekebishwa kwa kupunguza ada ya usajili wa magari kwa namba binafsi hadi shilingi 5,000,000 ili kupunguza gharama ya usajili wa namba binafsi na kuongeza mapato ya Serikali.

Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura 437 kwa kuweka tozo katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa kwa kiasi kitakachotofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha

itakayotumwa au kutolewa ili kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na miradi ya kimkakati.

Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Uthibiti wa Ajira kwa Raia wa Kigeni, Sura 436, ambapo kifungu cha 16 kinarekebishwa ili kuweka adhabu kwa waajiri watakaochelewa kuwasilisha taarifa za waajiriwa wenye uraia wa kigeni kwa Kamishna wa Kazi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha uwasilishaji wa taarifa kwa wakati.

Sehemu ya Kumi na Nne, Sehemu ya Kumi na Tisa na Sehemu ya Ishirini zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bandari, Sura 166, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano, Sura 172 na Sheria ya Wakala wa Meli, Sura 415 kwa lengo la kuweka matakwa kwa Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano na Shirika la Wakala wa Meli kukusanya mapato yao kwa mfumo wa GePG na kuwasilisha mapato hayo kwenye akaunti maalumu itakayofungulia Benki Kuu ya Tanzania.

Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada inakusudia kurekebisha sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418 ili kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua makampuni ambayo Serikali inamiliki hisa. Aidha, Sheria hii inarekebishwa ili kumuwezesha Waziri mwenye dhamana na fedha kuwasilisha Bungeni majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa amewasilisha taarifa yake.

Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 ambapo kifungu cha 4 kinarekebishwa kwa kuongeza ushuru wa barabara kwa shilingi 100 kwa kila lita ya petroli na dizeli kwa ajili ya kugharamia ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini.

Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 89 ili kuhuisha viwango vya ushuru kulingana na thamani ya sasa ya shilingi.

Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji, Sura 38 kwa kuanzisha Kamati ya Ushauri ya Kitaalam kwa ajili ya Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu yake.

Sehemu ya Ishirini na Moja ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 kwa kurekebisha kifungu cha 22 na Jedwali la Tatu ili kuweka takwa kwa waajiriwa kufanya maombi ya Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi (TIN) kwa lengo la kuwezesha utunzaji wa hesabu za kodi ya mapato itokananyo na ajira. Vilevile, vifungu vya 28A,28B,28C and 28D vinarekebishwa ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Kodi.

Kurekebisha vifungu vya 29 na 85 ili kuweka sharti kwa walipakodi waweze kuwasilisha nyaraka zilizotafsiriwa katika lugha rasmi. Vilevile, kurekebisha kifungu cha 35 ili kumtaka

mlipakodi yeyote anayehifadhi taarifa zake kwa njia ya kielektroniki kuwa na “server” ndani ya Jamhuri ya Muungano ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo.

Muswada pia unapendekeza kurekebisha vifungu vya 44, 51 na 74 ili kuongeza wigo wa watu ambao Kamishna Mkuu anaweza kupata taarifa kutoka kwao, kumuwezesha mlipakodi kuweka pingamizi kwa maamuzi ya Kamishna yasiyotokana na makadirio ya kodi pasipo kuweka amana ya kodi na kumuwezesha Kamishna Mkuu kudai kodi ambayo imerudishwa kwa mlipakodi kimakosa. Kifungu cha 56 kinarekebisha ili kuwezesha kodi ya majengo kulipwa wakati wa kulipia ankara za umeme kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa kodi na kupunguza gharama za kulipa kodi hiyo.

Sehemu ya Ishirini na Mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisha kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399. Kurekebisha Kifungu cha 10 ili kuhuisha wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato wanaowakilisha Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha.

Sehemu ya Ishirini na Tatu ya Muswada inakusudia kurekebisha Sheria ya Rufaa za Kodi Sura 408 ambapo kifungu cha 22 kinarekebisha kwa lengo la kuanzisha utaratibu wa kufanya usuluhishi wa migogoro ya kikodi nje ya Mahakama ili kuongeza kasi ya utatuzi wa migogoro ya kodi na kupunguza mlundikano wa mashauri.

Sehemu ya Ishirini na Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisha kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148, ambapo vifungu vya 3 na 55A vinarekebisha ili kuwezesha marejesho ya kodi ya Ongezeko la Thamani kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa bidhaa zinazonunuliwa na walipakodi waliosajiliwa katika upande mmoja wa Muungano na kutumika katika upande mwingine wa Muungano kwa lengo la kuongeza ufanisi wa marejesho ya kodi baina ya pande zote mbili za Muungano.

Kifungu cha 6 kinarekebisha ili kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa msamaha wa kodi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa usimamizi na ufuatiliaji wa misamaha. Vilevile, kurekebisha kifungu cha 6 ili kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa na huduma zitakazoingizwa au kununuliwa hapa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mkakati au yenye maslahi kwa umma kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebisha ili kuwianisha tafsiri ya bidhaa za mtaji kwenye Sheria za kodi na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 59 ili kutoza kodi kwa kiwango cha sifuri kwa huduma za usafirishaji na huduma nyingine zinazohusiana na usafirishaji wa mafuta ghafi kupitia bomba la mafuta linalopita Tanzania kutoka nchi nyingine.

Jedwali linapendekezwa kurekebisha ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja za mkononi, vishikwambi (tablets), modemu, mikebe ya kuhifadhia maziwa, mafuta ghafi, madini ya vito na makinikia, kadi na malighafi nyingine za kutengeneza vitambulisho vya taifa, vyumba vya ubaridi na nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vya mpira vilivyoko kwenye majiji na kuondoa msamaha kwenye taa zinazotumia umeme wa jua.

Sehemu ya Ishirini na Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82, ambapo kifungu cha 14 kinarekebishwa ili kuanzisha tozo ya asimilia 0.4 kwa waajiri binafsi wanaojishughulisha na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini ili kutatua changamoto za ulipaji wa tozo hiyo kwa wachimbaji wadogo na kuongeza wigo wa idadi ya wafanyakazi kwa ajili ya utozaji wa tozo ya maendeleo ya huduma kwa lengo la kutoa unafuu kwa waajiri wenye idadi ndogo ya waajiriwa. Aidha, kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kusamehe tozo ya maendeleo ya huduma kwa taasisi za afya za kidini ili kuzipunguza gharama za uendeshaji.

Dodoma
9th June, 2021

MWIGULU L. NCHEMBA
Minister for Finance and Planning

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY THE HON. MWIGULU L. NCHEMBA THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED “THE FINANCE ACT 2021”

(Made under S.O 99(10))

The Bill entitled “The Finance Act 2021” is amended generally as follows:

- A:** In Clause 8 by deleting the proposed section 164A(1) and substituting for it the following:
 “164A.-(1) There is established a levy to be charged on airtime at a rate ranging from 5 to 222.70 Tanzanian Shillings.”;
- B:** In Clause 11 by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:
 “(c) deleting the whole of Heading 22.08 and substituting for it the following:

Heading	H.S. Code No.	Description	Unit	Old Rate	New Rate
22.08		Undenatured ethyl alcohol of an alcoholic strength by volume of less than 80% vol; spirits, liqueurs and other spirituous beverages.			
	2208.20.00	- Spirits obtained by distilling grape wine or grape marc from locally produced grapes.	l	Tshs. 450.00 per litre	Tshs. 540.00 per litre
		Other locally produced spirits under this heading.		Tshs. 3,315.00 per litre	Tshs. 3,978.00 per litre
		Imported spirits under this heading:			
	2208.20.00	- Spirits obtained by distilling grape wine or grape marc	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.30.00	- Whiskies	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.40.00	- Rum and other spirits obtained by distilling fermented sugar – cane products	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.50.00	- Gin and Geneva	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.60.00	- Vodka	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.70.00	- Liqueurs and cordials	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre

		- Other:			
	2208.90.10	--- Distilled Spirits (e.g. Konyagi, Uganda Waragi)	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre
	2208.90.90	--- Other	l	Tshs. 3,655.05 per litre	Tshs. 4,386.06 per litre

- C:** In Clause 16(a) by deleting the word “thirty” appearing in the third column and substituting for it the word “twenty five”;
- D:** In Clause 18, by-
- inserting the figure “7” between the words “section” and “by”;
 - deleting the proposed subsection (2) and substituting for it the following:
“(2) Notwithstanding the provisions of this section, the Board shall not impose retention fee or any other fee, charges, penalty or payments on repayment of loan owed by former student loan beneficiary without approval of the Minister in consultation with Minister responsible for finance.”;
- E:** In Clause 20 by deleting paragraph (a);
- F:** By deleting Clause 21;
- G:** In Clause 22 by inserting a “comma” and the words “non-concessional” between the words “agreement” and “or” appearing in subsection (4)(b);
- H:** By deleting Clause 24;
- I:** In Clause 27 by deleting the proposed paragraph (b);
- J:** In Clause 28 by deleting the proposed paragraph (x) and substituting for it the following:
“(x) interest derived by a person from government bonds of not less than three years issued and listed on the Dar es Salaam Stock Exchange from 1st July 2021.”;
- K:** By adding immediately after Clause 29 the following:
“Amendment of section 3 **30.** The principal Act is amended in section 3 in the definition of the term “rateable property” by deleting paragraph (b)(ii) and substituting for it the following:
“(ii) in the case of a plot with more than one building, all buildings in actual occupation in that plot including improvements on, in or under such buildings.”;
- L:** In Clause 30 by adding immediately after the proposed paragraph (b) the following:
“(c) by deleting subsection (2A) and substituting for it the following:

(2A) The Minister responsible for finance shall cause fifteen percent of the monies collected under subsection (1) to be remitted to the Ministry responsible for local government authorities.”;

- M:** By deleting Clause 31;
- N:** By deleting the whole of Part X;
- O:** In Clause 38 by deleting the proposed subsection (1) and substituting for it the following:
“(1) There is established a levy to be charged on mobile money transfer transaction at a rate ranging from 10 to 10,000 Tanzanian Shillings.”;
- P:** In Clause 40 by deleting Clause 40(3) and substituting for it the following:
“(3) A person who fails to submit a return to the Labour Commissioner on or before the prescribed period under subsection (1), shall be liable to a penalty of five hundred thousand shillings for each month or part of a month during which the delay continues.”;
- Q:** In Clause 42 by the proposed subsection (3) and substituting for it the following:
“(3) All funds of the Authority shall be deposited into a bank account opened at the Bank of Tanzania and Authority’s expenditure shall be disbursed according to the approved budget of the Authority and upon approval of the Paymaster General.”
- R:** In Clause 44 by deleting the proposed definition of the term “public authority” and substituting for it the following:
““Public authority” or “body” means a body of persons, whether or not corporate, established under any written law, whose functions are of public nature and are exercised in furtherance of the public policy, and shall include authority or bodies-
- (a) which is in receipt of a contribution from, or the operations of which may, under the law or instrument relating thereto, impose or create a liability upon, public funds;
 - (b) where the government controls more than fifty per cent of the shares in that body or authority;
 - (c) whose accounts are, by or under any written law, required to be audited or are open to inspection, by the Controller and Auditor-General; or
 - (d) which has, in any of its financial year, received more than half of its income from public funds.”;
- S:** In Clause 47 by inserting the words “and Urban” between the words “Rural” and “Roads” appearing in the proposed proviso to paragraph (a);
- T:** In Clause 50 by deleting figure “4” appearing in the third column of item 22 and substituting for it figure “1”;

U: By deleting the whole of Part XVIII;

V: In Clause 54 by deleting the proposed subsection (8) and substituting for it the following:
“(8) All funds of the Authority shall be deposited into a bank account opened at the Bank of Tanzania and Authority’s expenditure shall be disbursed according to the approved budget of the Authority and upon approval of the Paymaster General.”;

W: By deleting Clause 56 and substituting for it the following:
“Amendment of section 35 **56.** The principal Act is amended in section 35(2) by deleting the words “the bank account of the Corporation” and substituting for them the words “a bank account opened at the Bank of Tanzania and the Corporation’s expenditure shall be disbursed according to the budget of the Corporation and upon approval of the Paymaster General”;

X: In Clause 68(a)(i) by adding a proviso immediately after the proposed paragraph (d) as follows:
“Provided that, the property rate in respect of rateable properties not connected with electricity, shall be paid in accordance with subsection (1)(a), (b) or (c) of this section.”;

Y: In Clause 79(4) by deleting the phrase “on behalf of the Zanzibar Revenue Board and remit it to the Tanzania Zanzibar Treasury” and substituting for it the phrase “and remit it to the Zanzibar Revenue Board.”;

Z: In Clause 85, by-
(a) adding immediately after item (ii) of the proposed paragraph (a) the following:
(iii) in item 7 by deleting the phrase “and printed for use by a local manufacturer whose name appears on the packing material” appearing immediately after the word “products” in sub item (1).”;

(b) deleting items 25 and 28 of the proposed paragraph (b) and substituting for them the following:

25	An import of precious minerals, tin, tungsten, tantalum, mineral concentrates and loaded carbon by any person for processing, smelting, refining or sale in the Mineral and Gem Houses or buying stations designated by the Mining Commission.
28	An import of artificial grass of HS Code 5703.30.00 and 5703.20.00 for football pitches located in City or Municipal Council approved by the National Sports Council of Tanzania.

AA: In Clause 87 by deleting the proposed paragraph s (b) and (c);

BB: By renumbering Parts I to XXV as Parts I to XXIII respectively;

CC: By renumbering Clauses 22 to 88 as Clauses 21 to 83 respectively;

Dodoma,
....., 2021

MWIGULU L. NCHEMBA
Minister for Finance and Planning

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY THE HON.
MWIGULU L. NCHEMBA THE MINISTER FOR FINANCE AND PLANNING AT THE
SECOND READING OF THE BILL ENTITLED “THE FINANCE ACT 2021”**

(Made under S.O 88(6))

The Bill entitled “The Finance Act 2021” is further amended as follows:

- A:** By adding immediately after paragraph X of the Schedule of Amendments the following:
“Amendment of section 79 **71.** The principal Act is amended in section 79-
(a) in subsection (1), by adding immediately after paragraph (b) the following:
 “(c) entered into controlled transactions or series of controlled transactions and fails to determine the income and expenditure resulting from the transaction in a manner that is inconsistent with arms length principle; and
(b) in subsection (2), by adding immediately after paragraph (b) the following:
 “(c) for a person who has contravened subsection (1)(c), one hundred percent of the tax shortfall.
- B:** By renaming paragraphs “Y” to “CC” of the Schedule of Amendments as paragraphs “Z” to “DD” respectively.
- C:** Deleting paragraph “CC” of the Schedule and substituting for it the following:
“CC: By renumbering Clauses 22 to 88 as Clauses 22 to 84 respectively.”

Dodoma,
....., 2021

MWIGULU L. NCHEMBA
Minister for Finance and Planning

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bajeti. Mheshimiwa Mwenyekiti una dakika 30. *(Makofi)*

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2021 *(The Finance Bill, 2021)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na amedhihirisha uongozi wake kwa kutuletea Muswada wa Sheria ya Fedha ambao unaenda kutatua changamoto za wananchi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango, Makamu wa Rais kwa kuendelea kumshauri vyema Mheshimiwa Rais. Vilevile Kamati inampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuendelea kusimamia shughuli zote za Serikali kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa ya Kamati iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 10 Juni, 2021, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na kueleza hatua mbalimbali za kikodi na kiutawala zinazochukuliwa na Serikali kwa mwaka

huu wa fedha. Hatua husika zina lengo la kuchochea uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kufuatia hatua hiyo, tarehe 15 Juni, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha Na. 5 wa mwaka 2021 kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza. Baada ya hatua hiyo na kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Bunge, ulielekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuujadili Muswada na kutoa maoni kuhusu mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Muswada; Kamati ya Bajeti ilifanya vikao mbalimbali kwa ajili ya kuufanyia kazi Muswada huu ikiwa ni pamoja na kupokea maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu maudhui, madhumuni na malengo ya Muswada huu. Pia, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na masuala mengine ya kikodi, baadhi ya wadau waliofika mbele ya Kamati ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maoni ya wadau, Kamati ilichambua maoni hayo na kuupitia Muswada kifungu kwa kifungu, kwa madhumuni ya kujiridhisha na ubora, tija na athari za kiuchumi zitakazopatikana kutokana na utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huu. Hatua hii iliwezesha Kamati kubaini maeneo yanayohitaji marekebisho katika Muswada kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali bila kuathiri mwenendo wa uchumi na kuvutia zaidi uwekezaji na uzalishaji mali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, siku ya Jumapili tarehe 20 Juni, 2021 Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango na kufanya majadiliano ya kina kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria 25 zilizopo kwenye Muswada huu. Aidha, majadiliano hayo yalikusishia pia Wizara na Taasisi zote za

Serikali ambazo zimeguswa na Muswada huu kama zilivyooneshwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021; kutokana uchambuzi uliofanywa na Kamati na baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Kodi ya Makampuni, Sura 212; Serikali inapendekeza kufuta utaratibu wa kutoa hisa fiche kwa madhumuni ya kuongeza uwazi kwenye umiliki wa hisa za kampuni. Aidha, Serikali imeeleza kuwa lengo la pendekezo hili ni kukabiliana na vitendo vya kihalifu kama vile utakatishaji wa fedha na ufadhili wa shughuli za kigaidi. Vie vile mapendekezo hayo ni kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa *Global Forum on Transparency and Exchange of Information for Tax Purposes* hivyo inatakiwa kutekeleza masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa pendekezo la usajili wa hisa *fiche* liliwasilishwa na Serikali katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 ambapo lilifanyiwa mabadiliko na kuwekwa kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020. Aidha, kwa wakati huo Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati ya kuweka utaratibu wa kusajili hisa *fiche* na kuzuia utoaji na uhamishaji wa hisa fiche bila idhini ya Msajili wa Makampuni. Katika utekelezaji wa Mabadiliko ya mwaka 2020, Serikali imeishauri Kamati kukubali mapendekezo ya Muswada huu kama yalivyokuwa yamewasilishwa mwaka 2020 na Kamati imeridhia mapendekezo hayo kutokana na changamoto zilizojitokeza kwenye mapendekezo ya Kamati ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura 306; Kamati inakubaliana

na Serikali juu ya mapendekezo ya kuanzisha ushuru utakaotozwa kwenye muda wa maongezi pamoja na miamala ya kutuma na kutolea fedha kwa njia ya simu. Ushuru huu utaongeza mapato ya Serikali na kupanua wigo wa kodi. Kamati iliishauri Serikali kuweka ukomo wa chini na kiwango cha juu kama ilivyokuwa imebainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya kutoka shilingi 10/= hadi shilingi 10,000/=. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. Ikumbukwe pendekezo hili litaongeza mapato ya Serikali kwa shilingi trilioni 1.254.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Kifungu cha 124 (2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kinatoa fursa kwa Serikali kufanya mabadiliko kwenye viwango vya ushuru wa bidhaa kwa kuangalia matarajio ya mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi. Takwa hili lina lengo la kulinda thamani ya shilingi dhidi ya mfumuko wa bei na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha hali ya uchumi utaona kwamba mfumuko wa bei uko kati ya 3% hadi 5%. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mabadiliko katika ushuru wa bidhaa kwa bidhaa ambazo ziko kwenye kichwa 22.08 yameongezeka kwa asilimia 30 ambayo ni mara sita ya kiwango cha mfumuko wa bei. Mathalani, kwa vinywaji vikali vinavyotengenezwa kwa zabibu vimetoka shilingi 450/= hadi shilingi 585/= kwa lita. Ongezeko hili ni sawa saw ana asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kiwango kingebadilika kwa kuzingatia kiwango cha mfumuko wa bei kama sheria inavyotaka, kiwango hicho kingetakiwa kuongezeka kutoka shilingi 450 hadi shilingi 472.5. Hatua hii inaweza kuathiri mauzo ya zabibu na hivyo kupunguza uzalishaji wa zao hilo hapa nchini jambo ambalo siyo nia ya Serikali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko ya viwango vya tozo kwa kuzingatia Kifungu cha 124(2) cha Sheria ili mabadiliko yafanyike kwa

kuzingatia mfumuko wa bei unaotarajiwa. Serikali ilikubaliana na pendekezo hilo la Kamati na kufanya mabadiliko katika viwango vya ushuru wa bidhaa kwa asilimia 20 badala ya asilimia 30 iliyokuwa imependekezwa na Serikali awali. Kiwango hiki kimezingatia viashiria vingine vya uchumi. Hata, hivyo kiwango hiki bado ni kikubwa kuliko mfumuko wa bei unaotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134; Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 13A cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali kwa kuruhusu Serikali kutoa dhamana sawa na kiasi cha hisa ambazo Serikali inamiliki kwenye kampuni. Awali, Kamati ilikuwa na wasiwasi na pendekezo hili kwani linaweza kuongeza mzigo wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya mashauriano ya kina na Serikali, Kamati, inakubaliana na mapendekezo hayo yanayolenga kuwezesha kampuni au taasisi inayotekeleza mradi wa kimkakati kama vile ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda mpaka Chongoleani, Tanga, kukopa mkopo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima izingatie viashiria vya deni kabla ya kutoa dhamana hizo kwa sababu endapo kampuni iliyopewa dhamana ikishindwa kulipa deni hilo ni wazi kwamba mzigo wa deni hilo utalipwa na Serikali na hivyo kuongeza deni la Serikali. Aidha, lazima kuwe na usimamizi madhubuti wa dhamana hizo ili zisitumike vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41; Kifungu cha 16 cha Muswada kinahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha. Mapendekezo hayo yanakusudia kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi kutoka asilimia 20 ya sasa hadi asilimia 15 na kuongeza kodi

katika mapato ghafi kutoka asilimia 25 ya sasa hadi asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa, kiasi cha mapato ya Serikali yanayokusudiwa kukusanywa kutokana na marekebisho hayo ya bilioni 14.93 kinaweza kupatikana kwa hatua inayopendekezwa ya kutoza kodi ya asilimia 10 katika michezo ya kutumia kompyuta yaani *virtual games* kwa kuwa michezo hii hadi hivi sasa ilikuwa halitzwi kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano ya kina kuhusu mapendekezo hayo, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kutokuongeza kodi kwenye mapato ghafi kwenye michezo ya *sports betting* kutoka asilimia 25 hadi asilimia 30. Hivyo, kodi ya mapato ghafi itabaki kuwa asilimia 25 na asilimia tano itakatwa ndani ya asilimia 25 na itapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho katika kifungu cha 34(1) ili kuondoa jukumu la Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kupeleka asilimia tano kwenda kwenye Baraza la Michezo na badala yake jukumu hilo lifanywe na TRA kwa sababu ndio wanaokusanya mapato ya michezo ya kubahatisha hivi sasa. Pendekezo ambalo lilikubaliwa na Serikali na limeletwa kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; kuhusu mapendekezo kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato na baada ya mashauriano ya kina na Serikali, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Ibara ya 22 ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yanalenga kuondoa urasimu wa utoaji wa misamaha ya kodi kwa kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi ya mapato isiyozidi bilioni moja katika kipindi chote cha mradi bila kuhitaji ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwenye miradi inayotekelezwa kwa fedha za wabia wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za Kamati kukubaliana na pendekezo hilo ni kurahisisha utoaji wa misamaha inayohusika na kuharakisha utekelezaji wa miradi kwa ufadhili wa wabia wa maendeleo kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 27B ya Muswada ilikuwa na lengo la kuanzisha kodi ya mapato ya asilimia tatu ya thamani ya mauzo ya madini pindi mchimbaji anapoenda kuuza madini yake katika masoko ya madini. Baada ya Serikali kutoa ufafanuzi kwamba walengwa wa kodi hiyo ni wachimbaji wadogo wasio rasmi yaani *artisanal miners* na sio wachimbaji wadogo wanaofanya shughuli zao kwa vibali na leseni wanaowajibika kulipa mrabaha wa asilimia sita na tozo nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliishauri Serikali kuondoa pendekezo hili kwa kuwa linaweza kupunguza kasi ya matumizi ya masoko ya madini na kuongeza kasi ya utorohaji wa madini nje ya nchi na hivyo kuikosesha Serikali manufaa ambayo yameanza kupatikana katika sekta hii. Kamati inaipongeza Serikali kukubali kuliiondoa pendekezo hili kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati inakubaliana na mapendekezo katika Kifungu cha 25 cha Muswada baada ya kupata ufafanuzi wa kina wa Serikali kuhusu watakaohusika na kodi ya zuio katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na umuhimu wa mapato yatakayopatikana kutokana na kodi hiyo. Serikali iliiieleza kamati kuwa mapendekezo haya hayawahusu wakulima wala vyama vya ushirika bali yanawalenga mawakala wa makampuni makubwa yanayojihusisha na biashara ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia vizuri utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kuondoa uwezekano au mianya ya kodi hiyo kutozwa moja kwa moja kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuangalia

namna bora ya uandishi wa Kifungu hicho ili iwalinde wakulima wadogo watakaouza mazao yao kwa makampuni moja kwa moja badala ya kupitia kwa mawakala ama vyama vya ushirika. Kifungu kilivyoandikwa hivi sasa hakitoi msamaha kwa wakulima hao wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289; kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Majengo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuongeza viwango vya kodi ya majengo. Hata hivyo, Kamati ilionesha wasiwasi juu ya utaratibu unaopendekezwa kukusanya kodi hiyo kwa hoja zifuatazo, kwamba ni:-

(i) Jinsi gani Serikali itahakikisha watu wenye msamaha wa kulipa kodi ya majengo chini ya kifungu cha 7 cha Sheria hiyo hawataathirika na ukusanyaji wa kodi hiyo kwa njia ya LUKU;

(ii) Jinsi gani Serikali itatoza kodi hiyo kwa majengo yenye LUKU zaidi ya moja;

(iii) Namna gani Serikali itakusanya kodi hiyo kwenye majengo ambayo hayatumii umeme wa *TANESCO* kwa njia ya LUKU; na

(iv) Namna gani Serikali itatofautisha LUKU za maeneo yanayotakiwa kutozwa kodi ya majengo na yale ambayo hayana sifa za kulipa kodi hiyo hususan maeneo ya vijijini wanaotumia umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja hizo kwa kueleza kwamba Serikali imeandaa utaratibu kwa kutumia *TEHAMA* ambapo mfumo uliopo kwa watumiaji wa LUKU unaweza kutumika bila kuathiri masharti ya Sheria ya utozaji wa Kodi ya Majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, hakuna mtu aliyesamehewa kulipa kodi hiyo wala majengo yaliyo nje ya maeneo yanayotakiwa kutozwa kodi ya majengo, yatatozwa kodi hiyo kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ilieleza kuwa njia ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa njia ya LUKU itatumika sambamba na njia nyingine za kawaida ili kukusanya kodi ya majengo kwa watu ambao hawatumi LUKU na pale ambapo itajitokeza changamoto ya ukusanyaji wa kodi hiyo kwa njia ya LUKU utaratibu wa kawaida utatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Ibara ya 34 inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Serikali katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa. Mapendekezo hayo yanakusudia kuondoa sharti la wazalishaji wanaomiliki mashamba katika halmashauri ambayo kuna viwanda vya kuyaongeza thamani mazao kutolipa ushuru wa mazao yaani *Crop Cess* na badala yake walipe ushuru wa huduma pekee yaani *Service Levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kwamba endapo mabadiliko hayo yatafanyika yatakuwa na athari hasi za kimapato kwa halmashauri zilizokusudiwa ili hali halmashauri hizo zilikwishaweka mapato hayo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na Serikali haikuwa na mpango wa kufidia mapato yatakayopotea. Serikali ilikubaliana na Kamati kuondoa mapendekezo ya Kifungu cha 34 cha Muswada kwa lengo la kwenda kujipanga na kuja na mapendekezo ambayo hayataathiri mapato ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 189; Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Wageni, Sura 436; Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82; na Sheria ya Rufaa za Kodi; Kamati inakubaliana na mapendekezo yote ambayo yametolewa na Serikali kuhusiana na mabadiliko ya sheria hizi kwa sababu zina lengo la kurahisisha ulipaji wa kodi na kurahisisha mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini.

Aidha, zinatoa mwanya kwa mlipakodi kufanya makubaliano nje ya mahakama ili kupunguza mlundikano wa kesi katika Bodi za Rufani ya Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati ilishauri Serikali kufanya maboresho katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia Wageni ili mapendekezo hayo yajumuishe waajiri wanaochelewa kuwasilisha taarifa pamoja na wale ambao hawawasilishi taarifa kabisa. Pendekezo hilo ambalo Serikali lilikubali nalo na imeleta marekebisho katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kukubaliana na pendekezo la Kamati kwa kuweka katazo kwa Bodi ya Mikopo kutoza *rentention fee* au tozo yoyote kupitia kanuni mpaka zitakaporidhiwa na Waziri mwenye dhamana ya Elimu kwa kushauriana na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutoa fursa kwa Serikali kuwasilisha majibu kuhusiana na Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye Kikao cha Bunge kinachofuata mara baada ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Taarifa yake Bungeni. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na utaratibu ambao Serikali ilitaka kuanzisha wa kumpa mamlaka Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukagua kampuni au makampuni ambayo Serikali ina hisa kiasi chochote kisichozi asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati ilishauri Serikali kubadili kifungu hiki na kumruhusu CAG kuendelea kukagua tu hesabu za makampuni ambayo Serikali ina hisa kwa zaidi ya asilimia 50 kwa sababu makampuni ambayo Serikali ina umiliki chini ya asilimia 50 uamuzi wa nani akague ni wa Bodi za Makampuni hayo na siyo wa Serikali. Pendekezo hili lilikubaliwa na Serikali na marekebisho yamefanyika kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220; Kamati inakubaliana na mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali ili kupanua wigo wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya

Barabara Vijijini. Hata hivyo, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kuanzisha Mfuko Maalum wa *TARURA* ili fedha zitakazokusanywa ziende kwenye Mfuko huo moja kwa moja na sio kupitia Serikali Kuu kama inavyopendekezwa kwa sababu utaratibu wa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali unaweza kuleta changamoto katika utolewaji wa fedha; na

(ii) Kuongeza Kipengele cha 4(1)(c) ili kuweka sharti kwamba endapo bei za mafuta zinashuka kwenye soko la dunia na kusababisha bei za mafuta kushuka nchini, asilimia 50 ya kushuka kwa bei ikusanywe na kupelekwa kwenye Mfuko wa *TARURA*. Kifungu hicho kiandikwe kama kinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kifungu hiki kitakuwa na manufaa makubwa sana pindi bei zinaposhuka na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafarijika kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekubalina na ushauri wa Kamati na kuahidi kuufanyia kazi kwa kurekebisha kasoro iliyobainishwa. Aidha, Serikali imepokea wazo la kuanzisha Mamlaka ya Barabara za Vijijini na kuahidi kulifanyia kazi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa *TARURA* ikiwezekana kuanzisha Mfuko Maalum wa Barabara za Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38; Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuanzisha Kamati ya Ushauri kwa Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji yaani *National Investment Steering Committee*. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kwamba Wajumbe wa Kamati hii ni vigumu kupatikana na kufanya vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kumpata Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato na

Naibu Gavana wa Benki Kuu kwa wakati mmoja itakuwa vigumu. Hivyo, Serikali ilikubaliana na pendekezo la Kamati la kuondoa Sehemu ya 18 ya Muswada ili kutengeneza Kamati ambayo inaweza kukutana kwa wakati na kufanya kazi ya ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Bandari, Sura ya 166 na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano, Sura 172; Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu utaratibu mpya wa makusanyo yote ya Mamlaka ya Bandari pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania. Lengo la mapendekezo haya ni kudhibiti matumizi katika mamlaka hizi. Hata hivyo, kuna mkanganyiko wa kisheria ambao inabidi utafutiwe ufumbuzi ili jambo hili litekelezwe kwa ufanisi. Mabadiliko yafanyike katika majukumu ya Bodi za Mashirika haya ili masuala yanayohusu bajeti yasikinzane na maamuzi ya bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utaratibu uliopendekezwa kwa TANAPA wa kuwapa fedha za miezi miwili mwanzoni mwa mwaka wa fedha, utumike pia kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuhakikisha huduma za bandari haziteteleki hasa ukizingatia bandari ni kiungo muhimu katika biashara ya usafiri na usafirishaji na upatikanaji wa mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafarijika kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imepokea na kukubali ushauri wa Kamati wa kuipatia Mamlaka ya Bandari fedha za miezi miwili mwanzoni mwa mwaka wa fedha ili kukubaliana na changamoto za uendeshaji wa Mamlaka ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutaka makusanyo yote ya Shirika la Uwakala wa Meli yawekwe katika akaunti maalum Benki Kuu ya Tanzania na matumizi yatakuwa yanahakikiwa na kupitishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo la hatua hii ni kudhibiti matumizi na kuongeza ufanisi katika shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli kati ya *TASAC* na Mawakala wa Meli, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 7 cha Sheria hii na kuondoa maneno *live animal* na maneno *any other goods as the Minister may by order published in the Gazette prescribe*.

Mheshimiwa Mwenyekiti maneno hayo yanatoa fursa kwa *TASAC* kuongeza wigo wa mizigo ambayo inatakiwa kufanyiwa uondoshaji. Aidha, kwa sasa *TASAC* imekuwa ikiondoshwa hadi wanyama wengine kama ng'ombe, mbuzi na kondoo ambapo wanyama hao hawakuwa malengo ya Serikali ambayo ilikuwa ni kushughulikia nyara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza Kifungu hicho cha 7 kirekebishwe na kiandikwe kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; mabadiliko yanayofanyika katika sheria hii pamoja na mambo mengine yanalenga masuala yafuatayo:-

(i) Kuweka masharti ya uwezo wa ujuzi wa Msuluhishi wa Migogoro ya Kodi yaani *Tax Ombudsman*;

(ii) Kutenganisha mamlaka ya Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Kodi na yale ya Bodi za Rufaa;

(iii) Kupanua wigo wa malalamiko ya kodi kwa watu wote na sio kwa wale wanaolipa kodi peke yao;

(iv) Kuweka utaratibu wa kuwa na *primary server* za kutunzia kumbukumbu za kidijiti nchini; na

(v) Utaratibu wa kutoa tafsiri rasmi ya kumbukumbu kwa zile ambazo hazitunzwi kwa lugha rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imekubaliana na mapendekezo hayo ya Serikali. Hata hivyo, inaitaka Serikali

kukamilisha mapema iwezekanavyo uanzishaji wa Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Kodi ili ofisi hiyo ianzishwe rasmi hasa ukizingatia kwamba ofisi hii ina umuhimu mkubwa sana katika kupokea malalamiko ya walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399; Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu mapendekezo ya Serikali ya kuweka sharti kwa Waziri wa Fedha na Mipango anapoteua Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato yaani *TRA* kwa kuweka uwiano wa bodi kulingana na muundo wa Wizara ambao kwa sasa umegawanyika kwa kuwa na Sehemu ya Mipango na Sehemu ya Fedha. Hivyo, kumtaka anapofanya uteuzi azingatie mgawanyo wa wajumbe kutoka Sehemu ya Mipango na Sehemu ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye sheria hii ambayo yanalenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa misamaha ya kodi kwa miradi ya Serikali na wahisani wenye Mkataba ambao unajumuisha msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imetoa misamaha kwa vifaa mbalimbali vya kilimo ili kuchochea uzalishaji, utunzaji na usafirishaji wa bidhaa za kilimo na mifugo. Pamoja na kwamba kuna changamoto nyingi za kikodi kwenye sekta ya kilimo, Kamati imeona ni vyema hatua za kusamehe ziende hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na vyanzo vya kufidia mapato yanayopungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko ili kuondoa sharti la waagizaji wa vifungashio vya madawa, kuleta vifungashio vikiwa na nembo ya mzalishaji kwa sababu sharti hilo lilikuwa lilienda kinyume na utaratibu wa kimataifa wa ufungashaji wa dawa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya mabadiliko hayo kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla ya Kamati; suala la *TARURA* kukusanya ushuru wa maegesho wa magari; licha ya kuunga mkono pendekezo hili, Kamati inaishauri Serikali kwamba, kwa kuwa halmashauri karibu zote nchini ushuru wa kuegesha magari unakusanywa na *TARURA* na kwa kuwa lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha *TARURA* kimapato, ni vema iongezwe ibara mpya katika Muswada huu ili kuipa mamlaka kisheria *TARURA* kukusanya ushuru wa kuegesha magari. Kamati inapendekeza isomeke kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya takwimu sahihi katika mabadiliko ya Sheria ya Fedha na Ukadiraji wa Mapato ya Serikali; Kamati imebaini kwamba Serikali inapokuwa ikibuni vyanzo vipya vya mapato, takwimu zinazotumiwa kwa baadhi ya maeneo zinakuwa si sahihi na hivyo kusababisha maamuzi kutokuwa sahihi. Kwa Mfano, Mamlaka ya Mapato imekuwa haifikii malengo ya ukusanyaji wa mapato karibu kila mwaka kutokana na ukweli kwamba takwimu zinazotumika kufanya makadirio sio sahihi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia takwimu sahihi wakati inafanya makisio ya makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mabadiliko ya kodi kutosomana na mapendekezo ya Wizara Mama; Kamati ya Bajeti imebaini kwamba kuna utofauti kati ya mapendekezo yanayokuwa yanawasilishwa na Wizara Mama na yale yanayotolewa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha. Madhara ya mkanganyiko huu ni kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuleta mapendekezo ya Muswada ambayo hayazingatii malengo au mawazo ya Wizara Mama. Hivyo, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kuhakikisha kabla ya kuleta mapendekezo Bungeni iwe inahakikisha mapendekezo ya Wizara Mama yanazingatiwa ili kuilea sekta husika na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka utaratibu wa muda maalumu katika kubadilisha Sheria za Kodi; moja ya jambo ambalo linaharibu mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara nchini ni kutotabirika kwa sheria za kodi. Kamati

inaishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa *Tax Calendar* ambapo mabadiliko yatakuwa na kipindi maalum isipokuwa tu endapo mabadiliko yaliyofanyika yanakuwa na madhara makubwa kwa uchumi na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba kutumia fursa hii kwanza kwa kukushukuru wewe kunipa nafasi hii, lakini kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri kwa Bunge letu na pia kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika kwa ushirikiano wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa sana kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Emmanuel Tutuba, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala ya kodi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Omari Kigua, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii Bajeti kwa umakini mkubwa, umahiri wao mkubwa na uvumilivu wao wakati wa kipindi chote cha Bajeti hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge yaani *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Bi Nenelewa Mwihambi, Katibu wa Bunge; Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndugu Michael Kadebe; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Mathew Kileo; Makatibu wa Kamati Ndugu Godfrey Godwin, Ndugu Emmanuel Rhobi, Ndugu Lilian Masabala na Ndugu Wilfred Akasi na Wanasheria wa Bunge Ndugu Mossy Lukuvi na Ndugu Stephano Seba Mbutu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo vyote katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2021 (THE FINANCE BILL, 2021)

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (The Finance Bill, 2021).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na amedhihirisha uongozi wake kwa kutuletea muswada wa Sheria ya Fedha ambao unaenda kutatua changamoto za wananchi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango kwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais, Vilevile Kamati inampongeza, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuendelea kusimamia shughuli zote za Serikali kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Juni, 2021, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi na kiutawala zitakazochukuliwa na Serikali kwa mwaka huo wa fedha. Hatua husika zina lengo la kuchochea uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi kama vile:

i. Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara Nchini yaani *"Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Bussiness Enviroment"*

ii. Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa vyanzo vilivyopo na kuongeza vyanzo vipya vya mapato;

iii. Kurahisisha ulipaji kodi pamoja na usimamizi wake;

iv. Kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio sawa ili viweze kushindana na uzalishaji kwa ufanisi na tija;

v. Kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata mapato yake stahiki; pamoja na

vi. Utaratibu wa kushughulikia misamaha ya kodi kwa miradi ya Serikali na ile ya wahisani.

Mheshimiwa Spika, aidha, kufuatia hatua hiyo tarehe 15 Juni, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha Na. 5 wa mwaka 2021 kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Kwanza. Baada ya hatua hiyo na kwa mujibu wa **Kanuni ya 97(1)** ya Kanuni za Bunge, ulielekeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuujadili Muswada na kutoa maoni kuhusu mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huo.

1.1. Uchambuzi wa Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilifanya vikao mbalimbali kwa ajili ya kuufanyia kazi Muswada huu ikiwa ni pamoja na kupokea maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu

maudhui, madhumuni na malengo ya Muswada huu. Pia, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na masuala mengine ya kikodi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wadau waliofika mbele ya Kamati ni pamoja na: -

- (a) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF);
- (b) Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI);
- (c) Chama cha Wamiliki na Waendeshaji wa Mitandao ya Simu (TAMNOA);
- (d) Baraza la Kilimo Tanzania (Agricultural Council of Tanzania);
- (e) Umoja wa Wawindaji Nchini (TAHOA);
- (f) Taasisi ya Wajibu;
- (g) Umoja wa Wazalishaji wa Vinywaji Vikali (*Tanzania Liquor Manufacturers Association-TALMA*);
- (h) Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini (FEMATA),
- (i) Wazalishaji wa Kahawa;
- (j) Chama cha Mawakala wa Forodha (*Tanzania Freight Forwarders Association*);
- (k) Tanzania Sport Betting Association
- (l) Muungano wa Watengenezaji wa Matela Tanzania (*Tanzania Trailer Manufacturers Union*); na
- (m) Wataalamu wa madini na uchimbaji wa madini wakiongozwa na Dkt. Dalaly Peter Kafumu Mbunge Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maoni ya wadau, Kamati ilichambua maoni hayo na kuupitia Muswada kifungu kwa kifungu, kwa madhumuni ya kujiridhisha na ubora, tija na athari za kiuchumi zitakazopatikana kutokana na utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye Muswada huu. Hatua hii iliwezesha Kamati kubaini maeneo yanayohitaji marekebisho katika Muswada kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali bila kuathiri mwenendo wa kiuchumi na kuvutia zaidi uwekezaji na uzalishaji mali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, siku ya Jumapili tarehe 20 Juni, 2021 Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango na kufanya majadiliano ya kina kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Ishirini na tano (25) zilizopo kwenye Muswada huu. Aidha, majadiliano hayo yalikusisha pia Wizara na Taasisi zote za Serikali ambazo zimeguswa na Muswada huu ikiwa ni pamoja na: -

- i. Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;
- ii. Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
- iii. Wizara ya Viwanda na Biashara;
- iv. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
- v. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- vi. Wizara ya Madini;
- vii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority-TRA*);
- viii. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*Business Registration and Licencing Authority-BRELA*);
- ix. Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA);

x. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); na

xi. Wakala wa Meli Tanzania (TASAC).

2.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2021.

Mheshimiwa Spika, kutokana uchambuzi uliofanywa na Kamati na baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:

2.1. Sheria ya Makampuni, Sura 212 (*The Companies Act, Cap.212*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufuta utaratibu wa kutoa hisa fiche- (*share warrant*) kwa madhumuni ya kuongeza uwazi (*transparency*) kwenye umiliki wa hisa za kampuni. Aidha, Serikali imeeleza kuwa lengo la pendekezo hili ni kukabiliana na vitendo vya kihalifu kama vile utakatishaji fedha na ufadhili wa shughuli za kigaidi. Vievile mapendekezo hayo ni kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa *Global Forum on Transparency and Exchange of Information for Tax Purposes* hivyo anatakiwa kutekeleza masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa pendekezo la usajili wa hisa fiche liliwasilishwa na Serikali katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 ambapo lilifanyiwa mabadiliko na kuwekwa kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020. Aidha, kwa wakati huo Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati ya kuweka utaratibu wa kusajili hisa fiche na kuzuia utoaji na uhamishaji wa hisa fiche bila idhini ya Msajili wa Makampuni.

Katika utekelezaji wa Mabadiliko ya mwaka 2020 Serikali imeishauri kamati kukubali mapendekezo ya muswada huu kama yalivyokuwa yamewasilishwa mwaka 2020 na kamati imeridhia mapendekezo hayo hayo kutokana na changamoto zilizojitokeza kwenye mapendekezo ya Kamati ya mwaka 2020.

2.2. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura 306

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali juu ya mapendekezo ya kuanzisha ushuru utakaotozwa kwenye muda wa maongezi pamoja na miamala ya kutuma na kutolea fedha kwa njia ya simu. Ushuru huu utaongeza mapato ya Serikali na kupanua wigo wa kodi. Kamati ilishauri Serikali kuweka ukomo wa chini na kiwango cha juu kama ilivyokuwa imebainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya kutoka **shilingi 10** hadi **shilingi 10,000**. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kamati kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho, ikumbukwe Pendekezo hili litaongeza mapato ya Serikali kwa **Shilingi trilioni 1.254**.

2.3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 124 (2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kinatoa fursa kwa Serikali kufanya mabadiliko kwenye viwango vya ushuru wa bidhaa kwa kuangalia matarajio ya mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi. Takwa hili lina lengo la kulinda thamani ya shilingi dhidi ya mfumuko wa bei na kuongeza mapato ya Serikali. Ukisoma kitabu cha hali ya uchumi utaona kwamba mfumuko wa bei uko kati ya asilimia 3 hadi 5. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba mabadiliko katika ushuru wa bidhaa kwa bidhaa ambazo ziko kwenye kichwa **22.08 (Heading 22.08)** yameongezeka kwa **asilimia 30** ambayo ni mara 6 ya kiwango cha mfumuko wa bei. Mathalani, kwa vinywaji vikali vinavyotengenezwa kwa zabibu vimetoka **shilingi 450** hadi **shilingi 585** kwa lita ongezeko hili ni **asilimia 30**, endapo kiwango kingebadilika kwa kuzingatia kiwango cha mfumuko wa bei kama sheria inavyotaka, kiwango hicho kingetakiwa kuongezeka kutoka **shilingi 450** hadi **shilingi 472.5**. Hatua hii inaweza kuathiri mauzo ya zabibu na hivyo kupunguza uzalishaji wa zao hilo hapa nchini jambo ambalo si nia ya Serikali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kufanya mabadiliko ya viwango vya tozo kwa kuzingatia Kifungu cha 124(2) cha Sheria ili mabadiliko yafanyike kwa kuzingatia mfumuko wa

bei unaotarajiwa. Serikali ilikubaliana na pendekezo hilo la kamati na kufanya mabadiliko katika viwango vya ushuru wa bidhaa kwa **asilimia 20** badala ya **asilimia 30** iliyokuwa imependekezwa na Serikali awali kiwango hiki kimezingatia viashiria vingine vya uchumi. Hata, hivyo kiwango hiki bado ni kikubwa kuliko mfumuko wa bei unaotarajiwa.

2.4. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 13A cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali kwa kuruhusu Serikali kutoa dhamana sawa na kiasi cha hisa ambazo Serikali inamiliki kwenye kampuni. Awali, Kamati ilikuwa na wasiwasi na pendekezo hili kwani linaweza kuongeza mzigo wa deni la Serikali. Hata hivyo, Kamati, baada ya mashauriano ya kina na Serikali, inakubaliana na mapendekezo hayo yanayolenga kuwezesha kampuni au taasisi inayotekeleza mradi wa kimkakati kama vile ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani-Tanga, kukopa mkopo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima izingatie viashiria vya deni kabla ya kutoa dhamana hizo kwa sababu endapo kampuni iliyopewa dhamana ikishindwa kulipa deni hilo ni wazi kwamba mzigo wa deni hilo utalipwa na Serikali na hivyo kuongeza Deni la Serikali. Aidha, lazima kuwe na usimamizi madhubuti wa dhamana hizo ili zisitumike vibaya.

2.5. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41

Mheshimiwa Spika, Kifungi cha 16 ya Muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha. Mapendekezo hayo yanakusudia kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi kutoka **asilimia 20** ya sasa hadi **asilimia 15** na kuongeza kodi katika mapato ghafi kutoka **asilimia 25** ya sasa hadi **asilimia 30**. Kamati ina maoni kuwa, kiasi cha mapato ya Serikali yanayokusudiwa

kukusanywa kutokana na marekebisho hayo ya **Bilioni 14.93** kinaweza kupatikana kwa hatua inayopendekezwa ya kutoza kodi ya **asilimia 10** michezo ya kutumia kompyuta yaani *virtual games* kwa kuwa michezo hii hadi hivi sasa ilikuwa haitozwi kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ya kina kuhusu mapendekezo hayo, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kutokuongeza kodi kwenye mapato ghafi kwenye michezo ya *sports betting* kutoka **asilimia 25** hadi **asilimia 30**. Hivyo, kodi ya mapato ghafi itabaki kuwa **asilimia 25** na asilimia tano itakatwa ndani ya **asilimia 25** na itapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho katika kifungu cha 34 (1) ili kuondoa jukumu la Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kupeleka **asilimia 5** kwenda kwenye baraza la michezo na badala yake jukumu hilo lifanyike na TRA kwa sababu ndio wanaokusanya mapato ya michezo ya kubahatisha hivi sasa pendekezo ambalo lilikubaliwa na Serikali na limeletwa kwenye jedwali la marekebisho.

2.6. Sheria ya kodi ya Mapato, Sura ya 332.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, na baada ya mashauriano ya kina na Serikali, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Ibara ya 22 ya Muswada. Mapendekezo hayo yanalenga kuondoa urasimu wa utoaji wa misamaha ya kodi kwa kumpa Waziri wa Fedha mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi ya mapato isiyozidi bilioni moja katika kipindi chote cha mradi bila kuhitaji ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwenye miradi inayotekelezwa kwa fedha za wabia wa maendeleo. Sababu za Kamati kukubaliana na pendekezo hilo ni kurahisisha utoaji wa misamaha inayohusika na kuharakisha utekelezaji wa miradi kwa ufadhili wa wabia wa maendeleo kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27(b) ya Muswada ilikuwa na lengo la kuanzisha kodi ya mapato ya **asilimia 3** ya thamani ya mauzo ya madini pindi mchimbaji anapoenda kuuza

madini yake katika masoko ya madini. Baada ya Serikali kutoa ufafanuzi kwamba walengwa wa kodi hiyo ni wachimbaji wadogo wasio rasmi yaani *artisanal miners* na sio wachimbaji wadogo wanaofanya shughuli zao kwa vibali na leseni wanaowajibika kulipa mrabaha wa **asilimia 6** na tozo nyingine. Kamati iliishauri Serikali kuondoa pendekezo hili kwakuwa linaweza kupunguza kasi ya matumizi ya masoko ya madini na kuongeza kasi ya utorohaji wa madini nje ya nchi na hivyo kuikoshesha Serikali manufaa ambayo yameanza kuonekana katika sekta hii. Kamati inaipongeza Serikali kukubali kuliondoa pendekezo hili kwenye muswada.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati inakubaliana na mapendekezo katika Kifungu cha 25 ya Muswada baada ya kupata ufafanuzi wa kina wa Serikali kuhusu watakaohusika na kodi ya zuio katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na umuhimu wa mapato yatakayopatikana kutokana na kodi hiyo. Serikali iliieleza Kamati kuwa mapendekezo haya hayawahusu wakulima wala vyama vya ushirika bali yanawalenga mawakala wa makampuni makubwa yanayojihusisha na biashara ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia vizuri utekelezaji wa mapendekezo hayo ili kuondoa uwezekano au mianya ya kodi hiyo kutozwa moja kwa moja kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuangalia namna bora ya uandishi wa Kifungu hicho ili kiwalinde wakulima wadogo watakaouza mazao yao kwa makampuni moja kwa moja badala ya kupitia kwa mawakala ama vyama vya ushirika. Kifungu kilivyoandikwa hivi sasa hakitoi msamaha kwa wakulima hao wadogo.

2.7. Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Majengo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuongeza viwango vya kodi ya majengo. Hata hivyo, Kamati ilionesha wasiwasi juu ya utaratibu unaopendekezwa kukusanya kodi hiyo kwa hoja zifuatazo:

(a) Kwamba ni jinsi gani Serikali itahakikisha watu wenye msamaha wa kulipa kodi ya majengo chini ya kifungu cha 7 cha Sheria hiyo hawataathirika na ukusanyaji wa kodi hiyo kwa njia ya LUKU;

(b) Jinsi gani Serikali itatoza kodi hiyo kwa majengo yenye LUKU zaidi ya moja;

(c) Namna gani Serikali itakusanya kodi hiyo kwenye majengo ambayo hayatumii umeme wa TANESCO kwa njia ya LUKU; na

(d) Namna gani Serikali itatofautisha LUKU za maeneo yanayotakiwa kutozwa kodi ya majengo na yale ambayo hayana sifa za kulipa kodi hiyo hususan maeneo ya vijijini wanaotumia umeme wa REA.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja hizo kwa kueleza kwamba Serikali imeandaa utaratibu kwa kutumia TEHAMA ambapo mfumo uliopo kwa watumiaji wa LUKU unaweza kutumika bila kuathiri masharti ya Sheria ya utozaji wa kodi ya majengo. Hivyo, hakuna mtu aliyesamehewa kulipa kodi hiyo wala majengo yaliyo nje ya maeneo yanayotakiwa kutozwa kodi ya majengo, atatozwa kodi hiyo kinyume na Sheria. Aidha, Serikali ilieleza kuwa njia ya ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa njia ya LUKU itatumika sambamba na njia nyingine za kawaida ili kukusanya kodi ya majengo kwa watu ambao hawatumii LUKU na pale ambapo itajitokeza changamoto ya ukusanyaji wa kodi hiyo kwa njia ya LUKU utaratibu wa kawaida utatumika.

2.8. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34 inahusu Mapendekezo ya marekebisho ya Serikali katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa. Mapendekezo hayo yanakusudia kuondoa sharti la wazalishaji wanaomiliki mashamba katika Halmashauri ambayo kuna viwanda vya kuyaongeza thamani mazao kutolipa ushuru wa mazao (*Crop Cess*) na badala yake walipe ushuru wa huduma pekee (*Service Levy*). Hata hivyo, Kamati

ilishauri Serikali kwamba endapo mabadiliko hayo yatafanyika yatakuwa na athari hasi za kimapato kwa Halmashauri zilizokusudiwa ilihali Halmashauri hizo zilikwisha weka mapato hayo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 na Serikali haikuwa na mpango wa kufidia mapato yatakayopotea. Serikali ilikubaliana na Kamati kuondoa mapendekezo ya Kifungu cha 34 cha Muswada kwa lengo la kwenda kujipanga na kuja na mapendekezo ambayo hayataathiri mapato ya Halmashauri zetu.

2.9. Sheria ya Ardhi Sura ya 113, Sheria ya Ushuru wa Stempu Sura 189, Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia wa Kigeni Sura 436, Sheria ya Elimu, Mafunzo ya Ufundi Stadi Sura 82 na Sheria ya Rufaa za Kodi

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mapendekezo yote ambayo yametolewa na Serikali kuhusiana na Mabadiliko ya Sheria hizi kwa sababu zina lengo la kurahisisha ulipaji wa Kodi na kurahisisha mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini. Aidha, zinatoa mwanya kwa mlipakodi kufanya makubaliano nje ya mahakama ili kupunguza mlundikano wa kesi katika Bodi za Rufani ya Kodi. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Ajira kwa Raia wa Kigeni ili mapendekezo hayo yajumuishe waajiri wanaochelewa kuwasilisha taarifa pamoja na wale ambao hawawasilishi kabisa. Pendekezo ambalo Serikali ilikubaliana nalo na imeleta marekebisho katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kukubaliana na pendekezo la Kamati kwa kuweka katazo kwa Bodi ya Mikopo kutoza *rentention fee* au tozo yoyote kupitia kanuni mpaka zitakaporidhiwa na Waziri mwenye dhamana ya Elimu kwa kushauriana na Waziri wa Fedha.

2.10. Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutoa fursa kwa Serikali kuwasilisha majibu

kuhusiana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye Kikao cha Bunge kinachofuata mara baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Taarifa yake Bungeni. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na utaratibu ambao Serikali ilitaka kuanzisha wa kumpa Mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukagua kampuni au makampuni ambayo Serikali ina hisa kiasi chochote kisichozidi asilimia 50. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kubadili Kifungu hiki na kumruhusu CAG kuendelea kukagua tu hesabu za makampuni ambayo Serikali ina hisa kwa **zaidi ya asilimia 50** kwa sababu makampuni ambayo Serikali ina umiliki chini ya **Asilimia 50** uamuzi wa nani akague ni wa Bodi za Makampuni hayo na siyo wa Serikali. Pendekezo hili lilikubaliwa na Serikali na marekebisho yamefanyika kupitia jedwali la marekebisho.

2.11. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali ili kupanua wigo wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Barabara vijijini. Hata hivyo, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:

(a) Kuanzisha Mfuko maalumu wa TARURA ili fedha zitakazokusanywa ziende kwenye mfuko huo moja kwa moja na sio kupitia Serikali Kuu kama inavyopendekezwa kwa sababu utaratibu wa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali unaweza kuleta changamoto katika utolewaji wa fedha;

(b) Kuongeza Kipengele cha 4 (1) (c) ili kuweka sharti kwamba endapo bei za mafuta zinashuka kwenye soko la Dunia na kusababisha bei za mafuta kushuka nchini **asilimia 50** ya kushuka kwa bei ikusanywe na kupelekwa kwenye Mfuko wa TARURA. Kifungu hicho kiandikwe kama ifuatavyo: -

<p><i>Division of road and fuel tolls</i></p>	<p>4A (1) <i>Notwithstanding section 4(3), the moneys collected as roads and fuel tolls on petrol and diesel shall be distributed as follows-</i></p>
	<p><i>(c) where there is a decline in global benchmark for crude oil prices that have effect on oil prices in the United Republic upon review and determination of domestic rate, such rate shall be reduced by 50 percent and the remaining percent shall be collected and allocated to TARURA "</i></p>

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini Kifungu hiki kitakuwa na manufaa makubwa sana pindi bei zinaposhuka na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya TARURA.

Mheshimiwa Spika, tunafarijika kulieleza Bunge lako tukufu kwamba Serikali imekubalina na ushauri wa Kamati na kuaahidi kuufanyia kazi kwa kurekebisha kasoro iliyobainishwa. Aidha, Serikali imepokea wazo la kuanzisha Mamlaka ya Barabara za Vijijini na kuaahidi kulifanyia kazi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa TARURA ikiwezekana kuanzisha Mfuko maalumu wa barabara za vijijini.

2.12. Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuanzisha Kamati ya Ushauri kwa Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji (*National Investment Steering Committee*). Hata hivyo, uzoefu unaonesha kwamba wajumbe wa kamati hii ni vigumu kupatikana na kufanya vikao. Kwa mfano, kumpata Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Kamishna mkuu wa Mamlaka ya Mapato na Naibu Gavana wa Benki Kuu kwa wakati mmoja itakuwa vigumu. Hivyo, Serikali ilikubalina na pendekezo la Kamati la kuondoa sehemu ya XVIII cha Muswada ili kutengeneza Kamati ambayo inaweza kukutana kwa wakati na kufanya kazi ya ushauri.

2.13. Sheria ya Bandari Sura ya 166 na Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Sura 172

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali kuhusu utaratibu mpya wa makusanyo yote ya Mamlaka ya Bandari pamoja na Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania. Lengo la mapendekezo haya ni kudhibiti matumizi katika Mamlaka hizi. Hata hivyo, kuna mkanganyiko wa kisheria ambao inabidi utafutiwe ufumbuzi ili jambo hili litekelezwe kwa ufanisi. Mabadiliko yafanyike katika majukumu ya Bodi za Mashirika haya ili masuala yanayohusu bajeti yasikinzane na maamuzi ya bodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu uliopendekezwa kwa TANAPA wa kuwapa fedha za miezi miwili mwanzoni mwa mwaka wa fedha, utumike pia kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuhakikisha huduma za Bandari hazitereleki hasa ukizingatia bandari ni kiungo muhimu katika biashara ya usafiri na usafirishaji na upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunafarajika kulieleza Bunge lako tukufu kwamba Serikali imepokea na kukubali ushauri wa Kamati wa kuipatia Mamlaka ya Bandari fedha za miezi miwili mwanzoni mwa mwaka wa fedha ili kukabiliana na changamoto za uendeshaji wa Mamlaka ya Bandari.

2.14. Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutaka makusanyo yote ya Shirika la Uwakala wa Meli yawekwe katika akaunti maalumu Benki Kuu na matumizi yatakuwa kuhakikiwa na kupitishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo la hatua hii ni kudhibiti matumizi na kuongeza ufanisi katika Shirika hili. Aidha, kutokana na changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli kati ya TASAC na Mawakala wa meli, Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 7 cha Sheria hii na kuondoa maneno *“live animals”* na maneno *“any other goods as the Minister may by order published in the Gazette prescribe”*. Maneno hayo yanatoa fursa kwa

TASAC kuongeza wigo wa mizigo ambayo inatakiwa kufanyiwa uondoshaji. Aidha, kwa sasa TASAC imekuwa ikiondoshwa hadi wanyama wengine kama ng'ombe, mbuzi na kondoo ambapo wanyama hao hawakuwa malengo ya Serikali ambayo ilikuwa ni kushughulikia nyara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza Kifungu hicho cha 7 kirekebishwe na kiandikwe kama ifuatavyo: -

<i>Exclusive mandate of the Corporation</i>	<i>7.-(1) The Corporation shall have exclusive mandate as to the carrying out of: - (a) clearing and forwarding functions relating to import and export of minerals, mineral concentrates, machineries, equipment, products or extracts related to minerals and petroleum, arms and ammunition and Government trophies.</i>
---	--

2.15. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko yanayofanyika katika sheria hii pamoja na mambo mengine yanalenga masuala yafuatayo: -

- (i) Kuweka masharti ya uwezo wa ujuzi wa Msuluhishi wa Migogoro ya Kodi (*Tax Ombudsman*);
- (ii) Kutenganisha mamlaka ya ofisi ya Mpokea malalamiko ya Kodi na yale ya Bodi za Rufaa;
- (iii) Kupanua wigo wa malalamiko ya Kodi kwa watu wote na sio kwa wale wanaolipa kodi tu;
- (iv) Kuweka utaratibu wa kuwa na *Primary Server* za kutunzia kumbukumbu za kidijiti nchini; na
- (v) Pamoja na utaratibu wa kutoa tafsiri rasmi ya kumbukumbu kwa zile ambazo hazitunzwi kwa lugha rasmi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo hayo ya Serikali hata hivyo, inaitaka Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo uanzishwaji wa Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya kodi ili Ofisi hiyo ianzishwe rasmi hasa ukizingatia kwamba Ofisi hii ina umuhimu mkubwa sana katika kupokea malalamiko ya walipa kodi.

2.16. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu Mapendekezo ya Serikali ya Kuweka sharti kwa Waziri wa Fedha na Mipango anapoteua wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kuweka uwiano wa Bodi kulingana na Muundo wa Wizara ambao kwa sasa umegawanyika kwa kuwa na sehemu ya Mipango na sehemu ya Fedha. Hivyo, kumtaka anapofanya uteuzi azingatie mgawanyo wa wajumbe kutoka sehemu ya Mipango na sehemu ya Fedha.

2.17. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye Sheria hii ambayo yanalenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa misamaha ya kodi kwa miradi ya Serikali na wahisani wenye Mkataba ambao unajumuisha msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Aidha, Serikali imetoa misamaha kwa vifaa mbalimbali vya kilimo ili kuchochea uzalishaji, utunzaji na usafirishaji wa bidhaa za Kilimo na Mifugo. Pamoja na kwamba kuna changamoto nyingi za kikodi kwenye sekta ya kilimo, Kamati imeona ni vyema hatua za kusamehe ziende hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na vyanzo vya kufidia mapato yanayopungua.

Mheshimiwa Spika, Vilevile kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko ili kuondoa sharti la waagizaji wa vifungashio vya madawa kuleta vifungashio vikiwa na nembo ya mzalishaji kwa sababu sharti hilo lilikuwa likienda kinyume na utaratibu wa kimataifa wa ufungashaji wa dawa. Kamati inaipongeza

Serikali kwa kukubali kufanya mabadiliko hayo kupitia jedwali la marekebisho.

3.0. MAONI YA JUMLA YA KAMATI

3.1. Suala la TARURA kukusanya Ushuru wa Maegesho wa Magari

Mheshimiwa Spika, licha ya kuunga mkono pendekezo hili, Kamati inaishauri Serikali kwamba, kwa kuwa Halmashauri karibia zote nchini ushuru wa kuegesha magari unakusanywa na **TARURA**, na kwa kuwa lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha **TARURA** kimapato, ni vema iongezwe ibara mpya katika Muswada huu ili kuipa mamlaka kisheria TARURA kukusanya ushuru wa kuegesha magari. Kamati inapendekeza isomeke kama ifuatavyo:-

XX.	<i>The principal Act is amended by adding immediately after section 31A the following:</i>
<i>TARURA to collect Parking Fee</i>	<p>31B-(1) <i>Notwithstanding the provisions of this Act, the Tanzania Rural and Urban Roads Agency shall have the obligation to:</i></p> <p style="padding-left: 40px;"><i>(a) Establish or designate parking bays for transportation objects on road reserves which are under the management of the Agency; and</i></p> <p style="padding-left: 40px;"><i>(b) Collect parking fees on parking bays established or designated as such.</i></p> <p><i>(2) The Agency Shall use the money collected as parking fees for road development projects.</i></p> <p><i>(3) The Ministry may by:</i></p> <p style="padding-left: 40px;"><i>(a) Regulations, prescribe powers of the Agency relating to management of parking bays and other matters incidental thereto; and</i></p> <p style="padding-left: 40px;"><i>(b) Order, published in the Gazette, prescribe parking fees in Districts and Urban Authority.</i></p>

3.2. Matumizi ya Takwimu Sahihi katika mabadiliko ya Sheria ya Fedha na Ukadiriaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Serikali inapokuwa ikibuni vyanzo vipya vya mapato takwimu zinazotumiwa kwa baadhi ya maeneo zinakuwa si sahihi na hivyo kusababisha maamuzi kutokuwa sahihi. Kwa Mfano, Mamlaka ya mapato imekuwa haifikii malengo ya ukusanyaji

karibia kila mwaka kutokana na ukweli kwamba takwimu zinazotumika kufanya makadirio sio sahihi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia takwimu sahihi wakati inafanya makisio ya makusanyo ya mapato.

3.3. Mapendekezo ya Mabadiliko ya Kodi Kutosomana na Mapendekezo ya Wizara Mama

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imebaini kwamba kuna utofauti kati ya Mapendekezo yanayokuwa yanawasilishwa na Wizara Mama na yale yanayotolewa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha. Madhara ya mkanganyiko huu ni kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuleta mapendekezo ya Muswada ambayo hayazingatii malengo au mawazo ya Wizara Mama. Hivyo, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kuhakikisha kabla ya kuleta mapendekezo Bungeni iwe inahakikisha mapendekezo ya Wizara mama yanazingatiwa ili kuilea sekta husika na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

3.4. Kuweka utaratibu wa muda maalumu katika kubadilisha Sheria za Kodi

Mheshimiwa Spika, Moja ya jambo ambalo linaharibu mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara nchini ni kutotabirika kwa sheria za kodi (*Unpredictability of Tax Laws*). Kamati inaishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa *Tax Calender* ambapo mabadiliko yatakuwa na kipindi maalumu isipokuwa tu endapo mabadiliko yaliyofanyika yanakuwa na madhara makubwa kwa uchumi na jamii.

4.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri kwa bunge letu na pia kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa

Fedha na Mipango, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Emmanuel Tutuba, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala ya kodi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Omari Kigua (Mb), Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa kamati ya Bajeti kwa umakini, umahiri na uvumilivu wao wakati wa kipindi chote cha Bajeti hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard)**

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe

22. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb Mjumbe
23. Mariam Nassoro Kisangi Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Bi Nanelwa Mwihambi Katibu wa Bunge, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo, Makatibu wa Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Wilfred Akasi na Wanasheria wa Bunge Ndg. Mossy Lukuvi na Ndg. Stephano Seba Mbutu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

MWENYEKITI: Sasa Mwenyekiti umewashukuru watu wote mbona wenyeviti hukuwashukuru, hukuwashukuru Wenyeviti wa Bunge. Basi inatosha nenda bwana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia, tunaanza na Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua, ajiandae Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae. Mheshimiwa Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia *Finance Bill* ambayo iko mbele ya meza yako. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijalia leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, bila ya yeye pengine tusingesimama au tusingekuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan. Niseme kwa maneno machache kabisa ameanza na mguu mzuri. Haya yote ambayo tunayapongeza, tunayaona hapa, ni fikra pana na hekima kubwa ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha. Niseme ushirikiano ambao wameutoa kwenye Kamati yetu ya Bajeti ni ushirikiano wa hali ya juu sana. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu wake wanatosha kwenye nafasi hiyo. Wameonyesha kwamba wana uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Mheshimiwa Waziri jana wakati anahitimisha ametumia lugha nyepesi sana, hakutaka kutumia lugha ya kiuchumi, na nina uhakika Watanzania wamekuelewa; kwamba maendeleo ya nchi hii yataletwa na Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mjomba, hatuna baba, tuchangie hata kwa senti moja kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji, barabara na afya katika nchi yetu. Mimi nikupongeze sana katika hilo. Na ninaahidi, Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na Watanzania wamekusikia, wataku-*support* kwa ajili ya kuiletea maendeleo nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru wenzetu wa Wizara ya Fedha; Katibu mkuu na *staff* wote. Kwa sababu katika kipindi cha miezi mitatu yote kila tulipowahitaji walikuja bila kusita na hakika wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwenye Kamati yetu ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati na watumishi wote wa Bunge ambao wameipa ushirikiano mkubwa sana Kamati ya Bajeti katika kuhakikisha kwamba

taarifa yetu leo imeweza kusomwa hapa na imeweza kusikilizwa na Wajumbe wote wa Kamati hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yetu ya Kamati ya Bajeti nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, nenda kayafanyie kazi, haya yote ambayo yamesemwa hapa. Kikubwa twende tukasimamie *fiscal policy*. Tukasimamie utekelezaji. Mifumo hiyo tuliyozungumza bila kuisimamia haya matarajio ya mabilion na mabilion hayawezi kupatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye maeneo machache ambayo ninapenda kutoa ushauri wangu mahususi. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kukubali ushauri wetu, hususan wa kukupa ridhaa wewe Waziri wa Fedha kwa kuruhusu kutoa msamaha kwenye GN.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa palikuwa pana changamoto kubwa sana. miradi mingi katika halmashauri, katika majiji, ilikuwa inachelewa kwa sababu fedha au misamaha hii ilikuwa inasubiri mlolongo mpaka Baraza la Mawaziri. Leo hii tumempa dhamana Mheshimiwa Waziri, na nina uhakika ataitumia vizuri; miradi yetu katika vijiji na halmashauri itakwenda vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Serikali na nipongeze Kamati yangu hususan kwa kurekebisha, Serikali kwa kuona kwamba eneo la bandari fedha zile zinakwenda kuwekwa kwenye akaunti maalum; fedha za TCRA, fedha za TASAC. Bandari ni kiungo kikubwa sana, ndipo ambapo Serikali ikisimamia kwa dhati kabisa hii miradi mingi ya kimkakati na miradi mingine ya maendeleo inaweza kukamilishwa kwa kuisimamia bandari yetu ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ninayoiona, bandari wana changamoto ya vifaa chakavu vya kupakua mizigo pale, lakini wana tatizo la mifumo ya kukusanya mapato. Kwa mfano, kuna mfumo wa TEHAMA unaitwa *Electronic Data Interchange* ambao unamfanya mwenye meli ajue ni lini mzigo wake umefika na meli itaondoka lini pale. Mfumo ule pale haupo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Waziri mwenye dhamana, hakikisha kwamba tunanunua vifaa vya kutosha, lakini hakikisha kwamba mfumo huu unawekwa ili uweze kusaidia utendaji wa kazi katika bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mifumo kwa ujumla; katika halmashauri zetu fedha nyingi za mapato zinapotea. Twende tukaimarishe mifumo yetu ya mapato isomane. Maeneo ya halmashauri mapato bado yanapotea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Umy, Waziri wa TAMISEMI, tuhakikishe tunaimarisha mifumo ya mapato katika halmashauri zetu ili fedha zile ambazo zinakusanywa na halmashauri zetu ziweze kusaidia kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Kandege, jia ndae Mheshimiwa Sware.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa fursa kwa siku ya leo niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na kuniwezesha kuwepo leo kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais. Hakika, naomba niungane na Wabunge wote ambao wamesema bajeti ya safari hii ni bajeti ya mfano, na hiki ambacho Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wamewasilisha, ndiyo maana hata Kamati ya Bajeti hatukupata kazi kubwa kwa sababu walikuwa *flexible* sana; nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo matatu. La kwanza; inawezekana hili tatizo limetokana na kanuni zetu na mfumo wetu, ifike wakati twende turekebishe kwa ajili ya manufaa makubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shuhuda; kila kipindi inapofika maandalizi ya bajeti tunapata wadau wengi kwenye *public hearing*. Lakini cha kusikitisha ni kodi zile za *East African Customs* ambazo maamuzi yake yanakwenda kufanyika huko na yanakuja kutekelezwa ambapo yanakuwa na athari kwa wafanyabiashara wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kama Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi tunakosa *room* ya kuwasaidia hawa Watanzania wafanyabiashara ambao wanakuja na mawazo mazuri. Lakini kwa sababu tayari maamuzi yanakuwa yalishafanyika *East Africa* pamoja na madhara ambayo wafanyabiashara wetu wanapata, tunakosa *room* kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasemea na kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali kama ni suala la kanuni tutazame *room* hii inapatikana wakati gani ili pale wanapokuja kuleta malalamiko yao kuhusiana na biashara wapi wanakwama, isije ikawa kama vile wanaleta tu hakuna utatuzi ambao unafanyika. Iko haja ya kulitazama kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe una wafanyabiashara wengi sana kutoka katika jimbo lako. Wewe ni shuhuda jinsi ambavyo umekuwa ukipata malalamiko, lakini Bunge linafanya nini, tunashindwa kwa sababu ya utaratibu ulivyo. Ifike mahali tuone namna nzuri ya kuwasaidia wafanyabiashara kwa sababu wanakuja na *cases* ambazo ni *genuine* lakini tunashindwa kuwasaidia; la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla. Na Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia wamesema kwa

nguvu kubwa kuhusiana na kuiwezesha *TARURA*. Na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha ametoa maelezo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna sehemu moja ambayo ni vizuri atazame kwa jicho la pekee. Amesema kwamba pamoja na hii pesa ambayo imeongezeka ambayo sisi sote tunajua kwamba inauma lakini inakwenda kutatua tatizo, na hasa changamoto kwa *TARURA*, lakini mgawanyo wake bado ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema hakuna haja ya kwenda kuanzisha mifuko mingine. Naomba unisikilize; uki-refer Sheria ya *Roads and Fuel Tolls Act Sub Section Two* inasema *all moneys collected as roads and fuel tolls shall be deposited in the account of the Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mfuko gani huu ambao unasemwa; huu ni Mfuko wa *Road Fund* ambao *control* yake haiko kwenye *TARURA*. Na wewe ni shuhuda; hivi karibuni *TARURA* wamekuwa wakihangaika katika kukusanya *parking fees*, lakini katika kukusanya hiyo *parking fees* hawaruhusiwi kutumia hata senti tano kwa sababu pesa hizo zinakwenda kwenye mfuko huo ambao wao hawana *control*. Sasa haitakuwa na maana kama tunasema inaongezeka shilingi 150 kwenda *TARURA* lakini hawana *control*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri tu Mheshimiwa Waziri – na bahati nzuri ni msikivu sana – aende *Section 4(a)* kama ambavyo tulianzisha Mfuko wa Maji, sasa aongeze (c) iwe *specifically* kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa *TARURA* ili haya makubwa ambayo tunatarajia kama Taifa yaweze kutendeka. Lakini vinginevyo sisi sote ni mahuhuda, kwamba pesa zikiingia kwenye Mfuko Mkuu hazina rangi, kwamba hii ilikuwa *meant specifically* kwa ajili hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ili mambo yote yafanyike, ni kwa mujibu wa sheria. Sasa Mheshimiwa Waziri usije ukasema kwamba mtatengeneza utaratibu ambao hautakuwa umepitishwa na Bunge hili, utakuwa ni *null and*

void. Kwa hiyo ni vizuri tukatoka kisheria tukajua sasa *TARURA* tunaiwezesha kama tulivyo iwezesha *TANROADS*, kusema kwao kote, nguvu yao yote, ni kwa sababu ni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba nirudi sehemu nyingine ambayo hakika juu ya utendaji na ufuatiliaji wa fedha. Hapo zamani tulikuwa na utaratibu ambao Serikali ilikuwa inaleta taarifa yake kila *quarter*, lakini tukaja tukabadilisha, pamoja na digitali ilivyo, sasa Serikali inaleta baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini; kama tumekosea tunasubiri mpaka mwisho tulishaingia chaka wote. Naomba Mheshimiwa Waziri ufikirie kwa mara nyingine utaratibu wa kuleta taarifa kila *quarter* ndiyo utumike ili kama kuna sehemu tunaona kwamba chanzo ambacho Mheshimiwa Waziri tumeanzisha, haki-*perform* vizuri, *then* kuwe na *mid-year review* ili tufanye marekebisho. Tusisubiri mpaka mwisho, tulishaenda kugonga pua halafu ndiyo tunasema tulikuwa tumepania hivi lakini katika makusanyo hatupati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nikiamini kwamba haya yamechukuli kwa uzito mkubwa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Sasa kuna dharura ya Mheshimiwa subiri, Mheshimiwa Oran, kwa hiyo Mheshimiwa Swalle, subiri Mheshimiwa Oran kwanza achange halafu utachangia. (*Makofi*)

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha ambao ni muhimu sana kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti hii ambayo imepitishwa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikumbuka ni kwamba baada ya kupitishwa bajeti, uhalali wa makusanyo ya aina yoyote ya kodi inabidi uzingatie Ibara ya 138 ya Katiba yetu

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo zoezi la leo ni zoezi muhimu sana kwa Bunge lako na inabidi tuzingatie sana na kuangalia ni kiasi gani haya yaliyomo kwenye huu muswada yana maudhui yaleyale kama ilivyokuwa imeandikwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. Lakini najua hayo yote ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, alivyofanya ukusanyaji wa kodi kuwa rahisi sana kwa kipindi hiki na mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yako, kwa kweli bajeti, hata huu muswada wenyewe umeandikwa vizuri sana. ndiyo sababu hata wewe yale mapendekezo ya Kamati ya Bajeti umeyachukua. Lakini ukiangalia hata Kamati ya Bajeti nayo kwenye taarifa yake imekubali karibu mapendekezo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii taarifa ya Kamati ya Bajeti pamoja na kukubali ina maelekezo ambayo Wabunge wjaribu kuyaangalia. Inatoa tahadhari kubwa. Tahadhari kubwa iko kwenye uandishi wa huu muswada. Hauko vizuri katika maeneo kadhaa ambayo Kamati ya Bajeti imeyaelezea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ya kwamba arejee Ibara ya 138 ya Katiba yetu ili iendane na huu muswada ambao ameupendekeza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kufurahisha zaidi ni kwamba huu muswada unajaribu kuboresha mazingira ya uwezeshaji, ya ufanyaji kazi hapa kwetu ya *blueprint* pamoja na kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi, lakini vilevile kulinda viwanda vyetu. Lakini ili hilo litimizwe inabidi uandishi uwe mahususi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Sura ya 147 ya huu muswada ambayo inazungumzia kuhusu

uongezeko la kwenye vinywaji, hasa vinywaji vikali. Silisemei hilo kwa sababu labda nataka niwatetee watu wanaokunywa vinywaji vikali, lakini ni kuwatetea labda wakulima wa zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ongezeko hili, pamoja na kupunguza kuwa asilimia 30, lakini ongezeko la asilimia 20 bado ni kubwa mno, linaweza kuleta athari kwa wakulima wetu ambao malighafi zao ndiyo zinatumika kwenye uzalishaji wa hizi pombe kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninamuomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia, kama ilivyo kwenye maudhui kuwa ongezeko lisiwe nje sana ya *inflation rate*. *Inflation rate* ya sasa hivi iko kati ya asilimia 3 mpaka 4, sasa kukiwa na ongezeko mpaka asilimia 20, hiyo ni kubwa sana. kwa hiyo ajaribu kuangalia kwa sababu hizi biashara zetu nazo tunaangalia na wenzetu, mataifa yanayotuzunguka, wanafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kuboresha hii Sura ya 134 ambayo ni Sheria ya Mikopo na Misaada. Ni muhimu kwa kweli ukiangalia kwa mazingira ya sasa hivi, ya kwamba inawezekana labda hii imelenga hasa kuwasaidia hii kampuni yetu ambayo ipo kwenye ujenzi wa bomba la mafuta kati yetu na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *guarantee* au hizi dhamana ambazo Serikali itazitoa, kiuhalisia inakuwa ni *contingent liability* au wanasema *off-balance sheet*. Lakini kwa wale watu ambao wanaangalia deni letu la Serikali, hizi zitaongezwa kwenye deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa uzoefu. Ya kwamba wewe unaposema hii ni *off-balance sheet*, wenzako wanapokwenda kule wanafanya *adjustment* ya *balance sheet* yako na wanaileta kwenye *on-balance sheet*, hizo dhamana zote. Kwa hiyo, kuweka na misingi ambayo tunasema deni letu liwe himilivu hii inaweza kuongeza deni letu lisiwe himilivu tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya 332 ambayo ni kodi ya zuio. Hii kodi ya zuio, hasa kwenye mazao ya kilimo, asilimia mbili, inaonekana nzuri lakini ni mbaya sana kwa wakulima. Sheria inasema hii asilimia mbili ya zuio haitawagusa wakulima wadogo – ndiyo sababu nimetoa tahadhari ya uandishi wa hizi sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitamgusa vipi mkulima mdogo hii asilimia mbili? Kwa sababu yule anayekusanya anakusanya kwa niaba ya mkulima. Kwa hiyo, italeta presha kubwa sana kwenye bei yetu ya mazao, siyo nafaka tu, lakini mazao hata kama kahawa, pareto n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri aende aliangalie vizuri hilo. Sasa hivi kilimo kinahitaji *transformation*. Kilimo siyo mahali kwa kwenda kurundika kodi. Tumepunguza kodi kwenye kilimo, siyo vizuri ukaongeza kodi kwenye kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeridhika sana kwai le *three percent* waliyoondoa kwenye kampuni za *FEMATA* ambao ni wachimbaji wadogowadogo wa madini. Kwa kweli hiyo ni hatua nzuri. Ie ingetuletea athari sana, kungekuwa na utorohaji mkubwa sana wa madini yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura ya 418 ya *CAG*, vilevile hatua nzuri iliyochukuliwa na Serikali ya kwamba *CAG* akague mashirika tu yale ambayo ina asilimia zaidi ya 50 ya uwekezaji, hiyo ni hatua nzuri. Lakini nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri, kinachotakiwa hapa ni kuimarisha misingi ya *internal controls* za mashirika yetu, siyo ukaguzi. Ukaguzi *postmortem*, tutampa lawama bure *CAG*, *CAG* kazi yake siyo kwenda kuimarisha mashirika. *CAG* ni kutupa taarifa sisi, kuangalia kama haya mashirika yetu mahesabu yake yametengenezwa namna gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri aimarishe Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar*), huyo ndiye atasaidia kuyawezesha mashirika yetu yasimamiwe vizuri, siyo *CAG*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye ile sura nyingine ambayo inasema mapato yote ya Mamlaka ya Bandari, *TCRA*, yaende Serikali Kuu. Nia ni nzuri, lakini kinachotakiwa pale ni kuhakikisha kuwa haya mashirika yanakuwa na uongozi mzuri, bodi nzuri, *management* nzuri, hata ukihamisha hizo pesa inawezekana ukaleta matatizo hata hayo makusanyo tunayokusanya sasa hivi yakawa madogo kwa vile watajiona hawa watu ya kwamba wao inawezekana hawaaminiki. Sasa hiyo inaweza kutupeleka mahali ambapo siyo pazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa pendekezo la kwamba kunapokuwa na punguzo la bei ya mafuta duniani, lile punguzo badala ya kupunguza bei za rejareja, ile tofauti ikienda kwenye Mfuko wa Barabara. Kwa kweli itaongezea mfuko wetu pesa nyingi ambazo zitanufaisha Watanzania kwa kiasi kikubwa. Lakini kwa kiasi kikubwa inawezekana hizi pesa walikuwa wanafaidi wachache tu wenye makampuni hayo ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kweli niendeleo tu kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu hii sheria ni nzuri sana. Tunaomba aangalie kwenye uandishi, unakumbuka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante na muda wako umekwisha.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie wasilisho la Waziri kwenye hii *Finance Bill*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitumie nafasi hii tena kump ongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo amejielekeza kuhakikisha kwamba anapanua wigo mkubwa wa walipa kodi.

Mimi niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lupembe *spirit* ya kuhamasisha Watanzania kulipa kodi ni jambo la msingi sana. Kwa kweli Waziri katika eneo ambalo amelifanya vizuri ni kutoa hamasa kubwa kwa wananchi kuona kulipa kodi ni fahari na kulipa kodi ya nchi ni kujiletea maendeleo wenyewe. Mheshimiwa Waziri alisema kwenye hotuba yake kwamba ni bora kuwa *unpopular*, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwa mipango hii mizuri ya kutanua wigo wa kodi wananchi watakavyoona mafanikio makubwa kwenye sekta mbalimbali atakuwa *popular* badala ya kuwa *unpopular*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninalo jambo moja ambalo napenda kuchangia kwenye Muswada huu. Tumezungumza ndani ya Bunge hili kwamba kati ya sekta ambayo nchi yetu haifanyi vizuri ni sekta ya kilimo. Sekta hii ya kilimo kwa muda mrefu imekuwa ikitengewa bajeti kidogo sana na hata katika mipango ya Serikali tulisema ndani ya Bunge hili kwamba pengine katika miaka hii mitano tujaribu kuiinua na kuikuza zaidi sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika hii *Finance Bill* ninayo *concern* moja kwenye *issue* inayohusu *Withholding Tax* kwenye mazao ya kilimo. Sisi kule Jimbo la Lupembe kwa mfano tunao wakulima wadogo wadogo kwa asilimia 95, wengi wanalima mazao ya chai, maharagwe, mihogo, matunda na miti ya mbao na wanauza mazao haya kwa watu binafsi kwa maana mtu mmoja mmoja na wananchi wengi wa aina hii hawapo kwenye *AMCOS*. *Withholding Tax* kwa ufahamu wangu hii ni *Income Tax* ni kodi, lakini tu *mode* ya kuikusanya inakusanywa kama *Withholding Tax* kwamba

amishna wa *TRA* anamwambia *agent* kwamba kusanya kodi kwa niaba yangu kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache ya kuzungumza, jambo la kwanza, ukisoma kwenye mapendekezo haya bila shaka huyu *withholding agent* atahitaji kupeleka *TRA statement* inayoonyesha jina na *TIN* la huyu ambaye anatakiwa kukatwa hii *Withholding Tax*, wananchi wa kule vijijini hawana *TIN Number* za biashara. Nikisoma huu Muswada sioni namna ambavyo Wizara imejipanga kwamba ni kwa namna gani wakulima wadogo wote watakuwa *identified* kwenye *TIN Number* ili watambulike kwamba wamekatwa *Withholding Tax*, hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, kwa mujibu wa taratibu zetu za kodi zilivyo mtu anayepaswa kulipa *Income Tax* ni lazima awe na *turnover* ya *four million per year*. Wakulima wadogo wadogo walio wengi hawawezi kufika *turnover* hiyo kwa mwaka, maana yake walipaswa kwenda ku-recover pesa ambayo walikatwa kwenye *Withholding Tax*, Kamishna wa *TRA* atawa-*identify* vipi kwamba kodi hii ilikatwa kwa fulani na siyo kwa fulani. Kwa hiyo, kwenye jambo hili la *Withholding Tax* naona kama kuna ukakasi mkubwa sana jinsi ya kwenda kulitekeleza na litakwenda kuleta matatizo makubwa kwa wakulima wetu wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka niishauri Serikali na kwa sababu bajeti hii inaanza kutekelezwa mwezi Julai, kwa vyovyote vile *TRA* sina uhakika kama wamendaa mazingira mazuri ya kutekeleza jambo hili kwa ufanisi unaotakiwa. Pamoja na nia njema ya kutanua wigo wa kodi kwamba watu wengi wachangie kwenye mapato ya Serikali kwenye mazao haya ya kilimo hasa kwa wakulima wadogo ambao wengi wao hawana *TIN Number* na kwa kweli wanauza mazao kwa kubangaiza, naomba sana kwenye utaratibu huu wa kutanua wigo wa kodi wasiwemo au la wadau mbalimbali wapewe muda wa kutoa maoni yao ili Serikali itafute njia bora zaidi ya kusimamia hawa *withholding agent* ni jinsi gani kodi hii itaweza ikakusanywa.

Hofu yangu mimi ni kwamba inawezekana *withholding agent* wakaenda kwa wakulima waka-*withhold* hii *tax*, lakini wasiweze ku-*remit TRA* kwa sababu mazingira ya kuwa-*monitor* na ku-*verify* kodi hii wamemkata nani na ataidai vipi yakawa ni magumu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango wangu huo naiomba sana Serikali kwa kuwa tumekusudia kuinua mazao ya kilimo na kuinua kilimo nchini hebu tujikite zaidi kuboresha kilimo chenyewe badala ya kuanza ku-*impose* kodi kwa wakulima wetu hawa wadogo. Nina uhakika wananchi wadogo kama kule kwangu wakulima wa chai, mahindi na mbao kodi hii itakwenda kuwaathiri sana kwa sababu ni wakulima wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, nasema ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jerry Silaa wajiandae Mheshimiwa Mgalu, Mheshimiwa Mpembenwe na Mheshimiwa Neema Lugangira.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye *Finance Bill* ya Mwaka 2021. Kama muda utaruhusu nitachangia kwenye maeneo manne; *Part VIII, The Amendment of Income Tax Act, Chapter 332* ambayo nitachangia kwa pamoja na *Part XXI, Amendment of the Tax Administration Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Income Tax* ndiyo inakusanya kodi na *Tax Administration Act* ndiyo inatoa utaratibu wa kukusanya kodi pamoja na adhabu. Ukisoma bajeti, ukurasa wa 52 kuna maneno ya kufanya marekebisho kwenye *Regulation* ama the *Transfer Pricing Regulation* za Mwaka 2014 kuondoa adhabu ya asilimia 100 kwa wale watakaobainika kufanya vitendo hivi vya *Transfer Pricing*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo makubwa yanayopoteza kodi ya nchi yetu hasa kwenye makampuni

makubwa ni *Transfer Pricing*. Ukisoma ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, *Audit on Transfer Pricing*, kwenye *Executive Summary Part XVI*, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ametoa mapendekezo kwa Wizara kui-*support* Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza nguvu kwenye suala la kusimamia Kitengo cha *International Tax Unit* katika kuhakikisha tunaondosha utoroshwaji wa fedha nchini kupitia *Transfer Pricing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, naamini taarifa hii tutaijadili Bunge linalofuata, Wizara ya Fedha badala ya kutengeneza utaratibu wa kutoa *support* inaleta mabadiliko ya kwenda kuondoa adhabu kwenye jambo ambalo ni kosa kisheria. Ukurasa wa 23 wa Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonyesha Kitengo hiki cha *ITU* kwa miaka zaidi ya mitatu kimefanya ukaguzi kwenye asilimia 33 tu ya makampuni ambayo yameainishwa kama *the most risk companies* kwenye *Transfer Pricing*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe na niliombe Bunge hili na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa lugha ya mjini tunasema hii umechomekewa, usisaini kanuni hii, ukisaini unaenda kuipa Serikali hasara kubwa ambapo siku za nyuma tulikuwa tumeshaondoka. Niseme tu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuwa anafahamu, ipo kesi, *The Civil Appeal Case No. 144* ya Mwaka 2018 ambayo imetolewa hukumu tarehe 20 Agosti, 2020 na *panel* ya Majaji watatu wa Mahakama ya Rufaa ikiongozwa na Jaji Mkuu Ibrahimu Juma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi hii imeenda kutoa hukumu ya kodi ya zaidi ya dola za Kimarekani milioni 900 kwa kampuni ya *African Barrick* ambayo kwa miaka mitatu mfululizo ili-*declare loss* hapa Tanzania, lakini iligawa *dividends* kwa wanahisa wake kule Uingereza. Kampuni ile haina mali yoyote duniani zaidi ya ile migodi mitatu na ukitaka kujua fedha hizi ziliondokaje nchini ziliondoka kwa *Transfer Pricing*. Sasa mnapoenda kusema mnataka kufuta kanuni hii ya adhabu kwa kigezo cha kusema eti unaenda kuhamasisha uwekezaji, aliyeandika hili Mungu anamuona, ameandika akijua wazi haendi kukuza uwekezaji.

T A A R I F A

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwenye kesi hiyo ambayo anaizungumzia hapa ni kwamba pia hawa *Barrick* wali-*declare* kwenye kesi ile kwamba walitumia kiasi cha asilimia 2 kama fedha za *CSR* katika ujenzi wa miradi mbalimbali katika Jimbo langu la Msalala, Kata ya Bulyankulu. Hata hivyo, mpaka hivi tunavyozungumza zile asilimia 2 ambazo walizi-*declare* kule mahakamani zile nyumba ambazo walijenga kwa fedha hizohizo za *CSR* walienda kuziua tena kwa wafanyakazi na sasa hatujui hizo fedha ziko wapi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jerry.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba masuala haya ya *Transfer Pricing* siyo mambo ya kujifungia sisi wenyewe. Kuna mkutano ulifanyika Addis Ababa unaitwa *The Addis Ababa Action Agenda* ulifanyika tarehe 15 Julai, 2015. Mkutano huu labda kwa sababu muda tu ni mfupi ulieleza mambo mengi sana kuhusiana na *Transfer Pricing*, ilieleza ni jinsi gani fedha nyingi zinatoka Africa kila mwaka katika utaratibu huu. Niliombe Bunge hili lakini nimuombe Waziri kwamba jambo hili likienda kufanyika tunaenda kutengeneza hasara kubwa sana kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, ile ni adhabu kwa yule anayebainika amekwepa kodi ile siyo kodi. Tumetoa hapa ada ya faini za barabarani kwa bodaboda toka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000, lakini adhabu bado ipo, unaenda kuondosha adhabu maana yake unaenda kuhalalisha kosa, unaenda kumfanya mtu sasa afanye kosa kwa amani kwamba hata akikamatwa hakuna adhabu.

Ningetegemea labda adhabu hii itoke asilimia 100 iende zaidi ya hapo ili kutengeneza uwoga kwa makampuni haya makubwa ambayo kwa miaka mingi yanalipa kodi ndogo kuliko Watanzania wazawa wanaofanya biashara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafanyabishara wa Tanzania wa kawaida kabisa wana adhabu ukichelewesha *returns* una adhabu...

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anazungumza *point* nzuri sana, muhimu sana, tuna vijana takribani asilimia 50 ya idadi ya watu wa Tanzania. Nampa taarifa kwamba tunavyopunguza adhabu ya pikipiki na kufanya shilingi 10,000 ni lazima tujue taarifa ni ajali ngapi zilikuwepo wakati faini ni shilingi 30,000 na faini ikiwa shilingi 10,000 kutakuwa na ajali ngapi? Hii ni taarifa sisi kama Bunge na msemaji lazima aizingatie wakati anachangia ili kuokoa watu wasikatwe miguu kwenye ajali za pikipiki, nampa taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry, taarifa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naamini dakika zangu unazilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa na mengi sana ya kuchangia hata dakika zikiniishia kwenye hili la *Transfer Pricing* nitasimamia na nimuombe Waziri asijaribu kuingia kwenye historia hiyo. Kama hilo litafanyika na wewe utaingia kwenye historia kwamba uli-*chair* kikao ambacho kimeenda kufanya jambo hilo la kuweza kudhulumu haki za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili nataka kuchangia ni *Part IX ya Amendment ya Local Government Authorities (Rating) Act, Chapter 289*. Kodi ya Majengo ina historia yake, inapata historia kwenye karne ya 17. Kule Ugereza Malkia Elizabeth I mwaka 1601 walipitisha sheria inayoitwa *The Poor Relief Act* iliyokuwa inatoa mamlaka kwa mamlaka za *Local Government* kukusanya kodi kwenye majengo ili kuwatengenezea huduma wakazi wakazi wa maeneo yale, *The Property Tax. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *Part IX*, Serikali imeleta mabadiliko inataka kuongeza *section 31A* inayotaka fedha hizi na wewe uko pale llala unafahamu majengo pale wapiga kura wako wanavyotaka huduma kupitia *Property Tax* zao, kifungu hiki cha 31A kinakwenda kupeleka pesa hizi kwenye *Consolidated Fund* na inarudishwa asilimia 15 si kwenye mamlaka husika zinarudi TAMISEMI zigawiwe nchi nzima. Labda watafute jina lingine la kodi hii na mimi nitaunga mkono kama ni Kodi ya Maendeleo au Kodi ya Miradi, naomba nilindie dakika zangu, hizo ni kumi zile za mwanzo bila taarifa. Kama tunataka kuipa jina lingine tuipe kodi jina lingine, lakini kama itaitwa *The Property Tax* msingi wake ni Kodi ya Majengo na wenye majengo yao kwenye mamlaka zile za Serikali za Mitaa wanasubiri huduma, wanasubiri barabara na mitaro, niombe Serikali ilianganalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho kwa dakika moja naomba nichangie *Part XIII*. Serikali inataka kurekebisha *The Non-Citizen Employment Regulation* na kutengeneza faini ya shilingi laki tano kwa wafanyakazi wageni. Tarehe 6 Aprili, mmemsikia Mheshimiwa Rais akitoa wito kwa wenzetu wa vibali vya kazi kutaka kuondoa urasimu kuwasaidia wawekezaji kupata vibali vya kazi. Kibali *Class A* ni dola 3,050, kibali *Class B* ni dola 2,050 bado *Labour* wanachukua dola 1,000 na *unreturn fees ya application*, halafu unataka umdai mwekezaji huyu shilingi laki tano eti hajaleta *return* ya watumishi wake. Tunaenda kukwamisha uwekezaji kwenye nchi hii, kila mwezi mnaenda kuwagongea milango yao. Hatuwezi tukawa tuna nchi ambayo mtu anakuja *serious investor* anaomba *serious permit* analipa *three thousand*

dollars halafu kuna mtu anataka kwenda kumgongea mlango wake kila mwezi amdai laki tano kwa sababu hajaleta *return* ya watumishi wake, mnaenda kukwamisha uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huku kwenye *Transfer Pricing* mnaenda kupoteza mabilion mna sema mnakuza uwekezaji mnakuja huku mnachukua shilingi laki tano kwa mwezi. Naomba Waziri wa Fedha hii *Amendment* ya Part XIII aiondoshe, hatuwezi kuwa na nchi ya aina hii ya kwenda kusumbua watu wanaokuja na mitaji yao. Tutakuwa ni nchi ya kipekee duniani ambayo tuna tamaa na fedha za watu na tutakwamisha uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mgalu, wajiandae Mheshimiwa Mpembenwe na Mheshimiwa Neema Lugangira.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo kuchangia Muswada wa Fedha wa Mwaka 2020/2021. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake yote ya Wizara ya Fedha pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Masauni kwa kazi nzuri na ushirikiano mzuri ndani ya kamati yetu. Naunga mkono hoja hii, lakini naishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa kutumia muda mwingi wenye nia njema kujadiliana na Serikali na mapendekezo yote ambayo yameainishwa kwenye taarifa yetu yote nayaunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni machache, kwanza katika *Amendment* ya *VAT*, *section* 81 naipongeza Serikali kwa kutambua bidhaa za mtaji zinazotambulika kwa

Sura 84, 85 na 90 ya Kitabu cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo hizi zitastahili kupewa vivutio vya hairisho la kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Pamoja na hatua hii ambayo itapunguza gharama za uwekezaji na kuchochea uwekezaji nchini, naomba Mheshimiwa Waziri na timu yake ikajielekeze kwenye masharti ya kupata vivutio vya hairisho hili kwenye Sheria ya VAT hasa *section* 11(2)(b) ambayo imesema angalau asilimia 90 ya bidhaa ama huduma zinazozalishwa au zitakazozalishwa ziwe zile ambazo hutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini natoa pendekezo hili? Mheshimiwa Spika alielekeza Bunge hili la Kumi na Mbili liwe Bunge ambalo litaleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Sasa ukiangalia *section* hii masharti ya kutoa ahirisho la kulipa VAT, wapo wawekezaji kwa mfano wa sekta nzima ya ujenzi wa viwanda vya mbolea, ambapo mbolea inayoingizwa ndani ya nchi inatozwa ushuru wa *zero rate* na pia inapata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Kwa hiyo, maana yake kama viwanda vya ndani vitazalisha mbolea, inaweza ikakosa fursa hii ya kupata uahirisho wa kodi la ongezeko la thamani. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu ikaliangalie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa naomba pia, pamoja na mapendekezo ya Kamati yetu kwenye Sheria ya Wakala wa Meli, sura ya 414, pamoja na nia njema ya kuunda TASAC na kazi zinazoendelea vizuri, lakini naomba Serikali ikatazame kile kifungu Na. 7 na ikatazame Sheria nzima hii, kutokana na maoni ya wadau mbalimbali waliokuja kwenye Kamati ya kuona mwingiliano wa majukumu ya kudhibiti hii sekta na kutenda shughuli zinazohusiana na masuala mazima ya TASAC. Kwa hiyo, naomba Serikali iwaskilize vizuri kwa sababu, wana nia njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ningepomba pia niipongeze Serikali; kwa pamoja tumekubaliana kwenye mashauriano wakafanye marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji

ya Tanzania, Sura ya 38 pamoja na kwamba kwa sasa wamefuta ili kufanya marekebisho ya sheria hii kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa *spirit* ile ile ambayo Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, kupitia bajeti hii na Serikali yake, ameonyesha kupunguza urasimu. Mkatazame uwekezano wa kumpa mamlaka Waziri wa Fedha katika kutoa idhini ya vivutio vinavyoidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya kutoa vivutio, mara nyingi pana kukwama. Kamati ya Kitaifa inatoa vivutio, lakini inapokuja kwenye sheria za kikodi mamlaka ya Waziri wa Fedha yalikuwa bado hajapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ambavyo mmetoa sasa, mamlaka ya Kamishina wa *TRA* na wewe Waziri wa Fedha, kwenye miradi ambayo inatekelezwa na wafadhili, imekupa fursa hiyo ambayo itawezesha kuondoa urasimu na miradi yetu kutekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilipongeze Bunge lako Tukufu, jana limefanya mapinduzi. Nimehudumu Bunge la Kumi, nimehudumu Bunge la Kumi na Moja na leo Bunge la Kumi na Mbili, sijapata kuona bajeti ambayo imepitishwa bila kupigiwa kura ya hapana hata moja. Jana tumepiga kura 94%, lakini 6% wao hawakuwa na msimamo popote. Nini tafsiri yake? Ni kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2021/2022, kwa kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri inayofanywa na Baraza lake la Mawaziri, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bunge tumeridhika kwa kiwango cha juu. Tumeridhika na yale maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa mara ya kwanza zimeongezwa fedha hapa juu kwa juu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha katikati ataleta *supplementary budget* ili yale aliyosema, ongezeko la shilingi bilioni 322 kwa Mfuko wa Barabara, ongezeko la shilingi bilioni 70 kwenye Bodi ya Mikopo, ongezeko la shilingi bilioni 50 kwenye madawa na

ongezeko la shilingi bilioni 121 kwenye maji. Yote hayo yatawezekana Bunge tena tukifanya mapinduzi kama jana ya kuipitisha sheria hii ya fedha, ambayo imeweka utaratibu sasa wa kuweza kukusanya na kupeleka kwenye mafungu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, licha ya kwamba imeboresha sheria mbalimbali, lakini kazi inaendelea. Naishukuru kwa sababu zaidi ya Watumishi wa Umma 70,000 washapandishwa vyeo na shilingi bilioni 300 zimetoka. Hongera Mheshimiwa Mchengerwa kwa kazi nzuri hii kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Hata punguzo la kodi la 8% kutoka 9% kwenye Muswada wa Fedha huu, lengo ni kumsaidia mfanyakazi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, jambo lingine ambalo limempa *credit* mama yetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Ile punguzo la miaka kutoka 12 mpaka miaka sita, ili askari huyu aweze kupata *pension*, aweze kuchangiwa; na tunatambua licha ya mambo mazuri, mipango, uwekezaji ambao unahimizwa na Serikali yetu, bila ya ulinzi na usalama mambo haya hayawezekani.

Kwa hiyo, hatua hii ya Serikali ya kuwawezesha vyombo vyetu kupunguza hii miaka ya mkataba, ninaiunga mkono na ninaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais alipokuwa Mwanza wakati wa Sherehe za Wafanyakazi, alitoa maelekezo kwamba Bima ya Watoto ambayo ilikuwa inaishia miaka 18 iende mpaka miaka 21. Hili sijaliona katika sheria hii, naomba nalo mlishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, ninampongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa hata marekebisho ya sura ya 178 ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, kwamba ongezeko lolote lipate idhini ya mashauriano baina ya Waziri mhusika na Waziri wa Fedha,

lenye nia ya kulinda utozaji holela, nalo pia lina msaada mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali kwa kuridhia kutoa mikopo kwenye taasisi zake zinazomiliki zaidi ya asilimia 50, katika marekebisho ambayo yamefanywa ya Ibara ya 13, Taasisi za Umma zinachangia mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Nampongeza Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha kwa kiwango cha mapato yanayopelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kumekuwa na ongezeko kubwa.

Kwa mfano, mwaka, 2019/2020 shilingi bilioni 983 zilipelekwa ukilinganisha na shilingi bilioni 161 mwaka 2014/2015. Ni wazi Serikali kwa kutoa fursa hii, itawezesha makampuni, kwa mfano *TPDC* kuingia mikopo ili kuweza kusambaza gesi na hivyo kuwezesha wanawake kuacha matumizi ya kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niendeleo kutoa pongezi, niwatakie kila la heri Waheshimiwa Mawaziri wote, najua baada ya bajeti hii mnapata kitendea kazi. Niendeleo kuwahimiza Watanzania kulipa kodi kwa hiari. Sheria zilizowekwa hapa Mheshimiwa Waziri amefafanua vizuri, tozo itakusanywa; inaenda kufanya nini? Imeweka mikakati ya kuziba mianya ya upotevu, pia imeweka mikakati ya kuongeza vyanzo vya kodi; na kana kwamba haitoshi, imeweka mkakati wa utekelezaji wa *blueprint* na kuhamasisha shughuli mbalimbali za uwekezaji. Haya yote yanayofanywa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, naunga mkono hoja. Nawapongezeni sana na kwamba mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Halima Mdee jiandae.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii *Finance Bill*. Kabla sijaanza kuchangia, nilikuwa naomba tu nichangie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa bajeti ambayo jana tumeipitisha kihistoria kabisa.

Vilevile, niwapongeze Mawaziri; Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake, nawapongeza pia Wabunge wenzangu ambao wapo katika Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameweza kuifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kuhakikisha kwamba bajeti hii inapitishwa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina nukta nne tu za kuchangia katika hii *Finance Bill*. Nukta ya kwanza yenyewe inahusiana na suala zima la tozo la asilimia 10 kwa zile *motorcycle* zinazoingizwa zenye umri zaidi ya miaka mitatu. Tukiangalia katika hii *Finance Bill*, hii *Amendment of the Excise and Management and Tariff* ipo kwenye *Cap. 147*, yenyewe inazungumzia kwamba kutakuwa na tozo ya asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la busara, lakini nami nilikuwa naomba kidogo nikazie hapa. Tafsiri yake pana ni kwamba, tunakwenda kuvilinda viwanda vyetu vya ndani. Nami nizungumze Kitaifa, lakini vilevile kwa *interest* kubwa sana ya Mkoa wa Pwani ambapo kuna viwanda vingi sana vina *assemble* pikipiki hizi. Nafikiri hii tozo ya asilimia 10 ingeongezwa kidogo, ingeenda mpaka asilimia 20. Kwa sababu, tafsiri halisi ni kwamba unapozungumzia *life span* ya *motorcycle*, haiwezi ikazidi miaka mitano. Kwa sababu mtu anaitoa pikipiki kutoka huko, anaileta hapo, tutakuwa *tunawa-discourage* sana wale wawekezaji ambao tunao tayari ndani ya nchi na hii itakwenda kuathiri sana katika zile kodi ambazo, tunakusudia kuzikusanya sisi kama Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri, ikiwezekana basi Mheshimiwa Waziri liangalieni hilo, wakati mnakuja kufanya majumuisho ikiwapendeza hii asilimia 10 twende juu kidogo, maana yake hapa tunajaribu *ku-discourage* kufanya nchi yetu kuwa kama ni *dumping*. Kwa hiyo, twende katika asilimia 20 ili tufanye *total discouragement* ya namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilikuwa naomba nilichangie, hili ni kuhusiana na suala zima la mabadiliko pale *PTA*. Hii ipo katika ukurasa wa 17, tunapojaribu kuangalia suala zima la *Amendment of the Ports Act* na hii inajumuisha vile vile, katika ukurasa wa 33 na ukurasa wa 34 tunapoigusa *TASAC* na wakati huo huo tunapoigusa *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya, tunakwenda kuchukua mapato yote yale yanapelekwa kwenye *account* maalum ambayo itaenda kufunguliwa pale Benki Kuu. Sasa mimi sielewi na sijui kama hii ndiyo ile inayoitwa *Treasurer Single Accounting System* au ni kitu kingine kidogo kipo tofauti. Kwa sababu tunachokifanya hapa, tusipokuwa makini sana kama Serikali, maeneo haya yako *very strategic*. Unapozungumzia *TPA*, ipo *very strategic* katika masuala ya kiuchumi. Unavyozungumzia suala zima la *TASAC*, ni *very strategic* vile vile katika masuala mazima ya kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo haitoshi, mpaka *TCRA* tumeona hapa, tumeweza kuwekeza tozo zile tunazoenda kuzikusanya zitakazoweza kutusaidia ili tuweze kwenda kufanya shughuli za kimaendeleo kwenye maeneo mengine. Sasa, tunavyoweza kwenda kuziweka zile fedha pale, *Pay Master General* ndio anakwenda kule *ku-approve* zile *expenditure*.

Mimi naona hii tunaenda kuweka *unnecessary bureaucracy*. Kwa hiyo, nafikiria ikipendeza, tuache tu *system* iendelee. Unajua Waingereza wana msembo wao, wanasema: "*don't fix it if it is not broken.*" (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mazingira yalikuwa yanaendelea kama kawaida, *why do we need to fix it again?* Tuache tu ili sasa tuweze kuona, taasisi hizi zinakwenda kufanya kazi kama ipasavyo. Tusipokuwa makini Serikali tunaweza tukaenda *ku-paralyze* taasisi hizi. Kama yale yaliyokuwa yameshatokea kule TANAPA, mazingira yalikuwa siyo rafiki mpaka Serikali ikaamua kuingia kati na kuanza kupeleka mashambulizi ya fedha kule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna *solution* mliyokuja nayo ambayo inasema kwamba mnakwenda kupeleka fedha za OC za miezi miwili, lakini tujue tu, hizi taasisi ziko *very sensitive*. Kuna mambo ambayo yanapaswa yafanyike kwa haraka haraka, sasa *decision making processes* zetu kidogo zinaweza zikawa zina shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nafikiria ambacho mnapaswa mkifanye ni kwenda kufanya *proper control* katika taasisi hizi *rather than* kwenda tena katika mfumo, kule katika *Central Bank*, kufungua akaunti, fedha zikaenda kule, wale wakiwa wanahitaji fedha, sasa wafanye *request. It makes no any difference* kama vile wanavyofanya kule katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo katika Halmashauri huwa hayaendi kwa wakati kwa sababu ya hizi *bureaucracy* hapa katikati. Makaratasi yanakusanywa pamoja, sijui yanapelekwa Benki Kuu yawe *authorized*, halafu ndiyo malipo yaweze kufanyika. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri eneo hilo tuweze kuliangalia kwa karibu zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilikuwa naomba nilichangie ni eneo linalohusiana na masuala mazima ya malipo. Hapa tunakwenda kufanya *amendment* inayohusiana na *Amendment of the National Payment System Acts*. Hii *amendment* tunayoenda kuifanya, tunaipa mamlaka sekta husika au Wizara husika kwamba sasa wanakwenda kutengeneza *regulation* ili sasa ziweze kutumika ili tuone ni jinsi gani yale makato ya simu yanayoenda kufanyika kule yaweze kwenda kama ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nitoe tahadhari hapa. Sisi tunayo hapa Kamati ya Sheria Ndogo, nafikiri ingekuwa ni busara zaidi, hizi kanuni ambazo zinakwenda kuandaliwa sasa na Wizara, kabla hazijaenda *kuwa implemented* ziletwe hapa Bungeni. Tunaye Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, ana umahiri mkubwa sana na Wabunge wenzetu. Ziletwe zile kanuni wazipitie. Watakapoweza kujiridhisha, basi tafsiri yake ni kwamba tunakwenda *kuzi-implement*. Kinyume na hapo nachelea kusema kwamba, yasije yakatokea kama yale yaliyotokea kwenye vikokotoo. Hii nafikiri inaweza ikawa ni tafsiri pana sana na hii tusipokuwa makini linaweza likawa ni tatizo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, niweze kuchangia katika eneo hilo, tuweze kuona tunavyoenda kumpa *freedom* moja kwa moja Waziri husika na taasisi ile kwenda kuandaa kanuni zile, hii inaweza ikaja ikaleta shida. Lazima hizo kanuni zije Bungeni, wale watu wa Kamati ya Sheria Ndogo wapo, wazipitie. Wao kwa niaba yetu watakapoweza *kuzi-authorize* zile, basi ziweze kutumika. Hii tunaweza tukaenda kuchukua *control measure* ya hali ya juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa naomba vile vile nilichangie, ni kuhusiana na hii *amendment* ambayo ilikuwa imeenda kufanyika, *Amendment of the Road and Fuel Tolls Act*, tumeenda kuongeza shilingi moja kule. Hili ni jambo la busara sana. Naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa ujumla wao kwa kuweza kuja na ubunifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nachelea kusema kitu kimoja tu, sijaona hapa, labda Mzee Mpembenwe wakati ananipeleka shule, hii lugha ni ya wenzetu labda sielewi vizuri. Sijaona kama hizi fedha zinazoenda kupelekwa kule katika huo mfuko zimeenda kuzungushiwa ili sasa kuweza kuwa na uhalisia kwamba

zinakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko ule wa *TARURA* tunaokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, labda kama ni tatizo la lugha, naomba tu ieleweke hivyo, basi Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atatuambia. Kinyume na hapo, kutokana na tafsiri ya maelezo haya ambayo yamezungumzwa hapa, sijaona kama kuna kipengele kinachosema kwamba fedha hizo zitakuwa *per-se* kwa ajili ya suala zima la *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Neema atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Juma Hamad Omar jiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye hii *Finance Bill*. Kwanza kabisa napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na bajeti ya kimkakati ambayo inalenga kwenda kuinua uchumi wetu na hata uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kuchangia kwenye eneo la *Part 24 Amendments ya Value Added Tax Act ya 2014 Cap. 148*, ambapo kwenye ukurasa wa 42 Serikali imeridhia ombi ambalo mimi binafsi nilitoa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ya kuacha msamaha wa *VAT* kwenye bidhaa za taa zinazotumia nishati ya jua kwa maana ya *solar lights*. Jambo hili litakwenda kuwasaidia sana wananchi wetu hususani wananchi wa vijijini, ili waweze kuendelea na shughuli zao za kujiinua kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapa, napenda kupendekeza kwa Serikali kwamba kwa kuwa bado

upatikanaji wa maji haujasambaa maeneo yote nchini, basi Serikali iweze pia kutoa msamaha wa kodi kwenye *pump* za maji zinazotumia *solar* (*solar water pumps*). Hii itasaidia sana: moja, kufanikisha ile kampeni ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani na pia itasaidia kulinda watoto wetu ambao wengi wanapata changamoto mbalimbali wanapokwenda visimani kuchota maji; na tatu, itasaidia katika kilimo cha mboga mboga, matunda na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili hili katika ukurasa wa 43 chini ya kipengele hiki cha *Part 24*, Serikali pia imesikia kilio cha wadau wengi wa mazao haya ya mboga mboga, matunda na maua ambapo imeweka msamaha wa kodi wa *cold rooms*. Hili ni jambo jema sana ambalo litakwenda kuimarisha biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kupendekeza Serikali katika eneo hili, iongeze pia zile *cold trucks*, kwa sababu hivi sasa kuna changamoto kubwa ya kusafirisha haya mazao.

Nikitoa tu mfano mdogo wa samaki, unakuta mara nyingi hata ukiwa Mkoa wa Dar es Salaam unakuta sSamaki zimerushwa nyuma ya *pickup*, zinapigwa jua yaani haziko katika mazingira salama, zinakaa kwenye foleni muda mrefu na changamoto kubwa unakuta *cold trucks* bado kodi yake ipo juu. Kwa hiyo, kwa muktadha ule ule ambao Serikali imeweka msamaha wa kodi kwenye *cold rooms*, basi naiomba Serikali pia ifanye hivyo kwenye hizi *cold trucks*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, naomba niende kwenye *Part 10* ya *Amendments* ya *Local Government Finance Act Cap. 290* kwenye ukurasa wa 15. Hapa Serikali imependekeza kwamba, makampuni yalipe *Service Levy* peke yake na yasilipe *produce cess*. Hili ni jambo jema sana, lakini kuna athari kwamba linaweza likapunguza mapato ya Halmashauri, hususan pale ambapo *produce cess* ni kiwango cha juu zaidi ya *Service Levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa tu kuikumbusha Serikali kwamba chini ya sheria hii kuna takwa la kisheria ambalo linasema kwamba kila Halmashauri inatakiwa ifanye *re-investment* kwenye sekta ya kilimo, sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi kulingana na yale mapato yake ya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri, Halmashauri inatakiwa *i-reinvest* asilimia 20 kwenye sekta ya kilimo, asilimia 15 kwenye sekta ya mifugo na asilimia 5 kwenye sekta ya uvuvi. Jambo hili toka sheria hii ilivyotungwa, yaani toka takwa hili lilivyowekwa kwenye sheria hii, halijawahi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo kwa haraka, Halmashauri ya Mufindi mapato yake ya ndani ni shilingi bilioni tatu kati ya hizo bilioni tatu shilingi bilioni 2.4 zinatokana na sekta ya kilimo, lakini halmashauri hii ina *re-invest* kwenye kilimo asilimia mbili tu ambayo ni milioni 60 wakati ilitakiwa ili-*invest* asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo tukija kwenye Halmashauri ya Njombe mapato yake ya ndani ni bilioni 1.5. Kati ya hiyo milioni 600 zinatokana na sekta ya kilimo lakini ina *re-invest* asilimia mbili tu ambayo ni milioni 12 wakati sheria hii inataka kwamba *re-invest* asilimia 20. Kwa hiyo kwa kuwa Serikali imeamua kwamba makampuni yasilipe *produce cess* yalipe tu *service levy*. Basi niombe Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba halmashauri zinatenga fedha za *re-investment* kama ambavyo sheria hii imeagiza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la faini za bodaboda na bajaji. Serikali kwa nia njema imepunguza faini kutoka elfu 30 mpaka elfu 10. Malengo makuu ya hizi faini huwa ni matatu; la kwanza ni kumfanya aliyefanya kosa ajifunze; kufanya wengine wasifanye kosa; kuzuia mtu asifanye kosa. Sasa kwa kupunguza kutoka elfu 30 mpaka elfu 10 tunafisha haya malengo ya faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupendekeza kuwa, Serikali ije na mfumo wa kuweka *point system* kwenye hizi leseni. Kwamba humu mwendesha bodaboda au bajaji akifanya kosa la kwanza atalipa elfu 10 sawa; akifanya kosa la pili alipe elfu 10 sawa; akifanya kosa la tatu kulingana na ile *point system*, basi leseni yake ifungiwe. Kwa sababu kwa kufanya hivyo ndiyo tutaendelea pia kulinda ile dhana nzima ya zile faini na kulinda watumiaji wa zile pikipiki na bajaji, lakini hata na maisha ya wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana; tusiache hii faini ya elfu 10,000 peke yake, Serikali ije na *point system* ambayo itasaidia kuhakikisha kwamba huyu dereva wa bodaboda au bajaji, akishalipa faini zake mara tatu basi akae akijua kwamba leseni yake imefungiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, nakiri na natambua nia njema ya Serikali ya kuimarisha vyanzo vyake vya mapato kupitia sekta ya kilimo. Hata hivyo, napenda kuishauri Serikali kwamba mwaka wa fedha ujao, hebu Serikali ije na vyanzo vipya vya mapato ili tusiendeleo kukamua kundi lile lile badala yake tuangalie makundi mengine ambayo hivi sasa hayatozwi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda kurejea ushauri ambao niliutoa. Naiomba sana Serikali ije na utaratibu wa kutoza kodi ya huduma za kidigitali yaani *digital service tax*. Kwa sababu kwa kufanya hivyo Serikali itaweza kupanua wigo wa walipa kodi badala ya kuendelea kutoza kodi nyingi zaidi kwenye kundi lile lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee jiaandae Mheshimiwa Juma Omar na ajiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono alichokizungumza Mheshimiwa

Jerry Silaa kuhusiana na *transfer price*. Sitataka kukirudia kwa sababu amekizungumza vizuri na kwa kina. Natumaini Waziri atakuja na majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa sheria hii maana yake ni kwamba itakuwa ni marufuku sasa hivi kwa Bodi ya Mikopo kuweka tozo mbalimbali zinazotokana na Mikopo ya Elimu ya Juu na kwa kweli ni ushindi kwa wote waliopigania kero ya asilimia sita ya *retention fee* na vile vile asilimia 10 ya *penalty* ambayo ilikuwa inatozwa kwa watu ambao wamevuka miwili ile ya muda ambao walikuwa wamepewa wa kuweza kulipa deni. Kwa hiyo nitambue kazi ambayo imefanya na vijana huko nje lakini hapa nitambue kelele nzuri sana zilizopigwa na Mheshimiwa Matiko kuhusiana na vijana hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitazungumza hoja ambayo imekuwa *raise* na Kamati, lakini ambayo vile vile imezungumzwa na Mheshimiwa Njeza ambaye ni Mjumbe wa Kamati, kuhusiana na ushuru wa bidhaa; yale marekebisha ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambayo yanahusu vinywaji vikali. Hii inawahusu wote ambao wanatumia *whisky*, wanapiga ma-*Gin*, wanapiga ma-*Vodka*. Malengo ya kuweka ushuru ambao haukuwa mkali sana kwa vinywaji ambavyo vinazalishwa nyumbani lililenga ku-*encourage* watu wetu watoke kwenye vinywaji ambavyo havijachujwa. Vinywaji ambavyo havijapita kwenye mnyororo wa kuhakikiwa ili wasiweze kupata maradhi na vitu vingine. Kwa lugha za gongo na mapombe mengine yanayofanania hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumza hivi kwa sababu tumepata nafasi ya kukutana na wadau ambao ndio walipa kodi wa nchi hii na wameonesha *concern* zao kuhusia na hili. Kubwa zaidi hili ni jambo la kisheria; sababu Sheria ya Ushuru wa Bidhaa imezungumza masuala mawili makubwa; kwamba bei ama ushuru utaongezwa kutokana na mfumuko wa bei tarajiwa ama shughuli zingine za kiuchumi. Sasa sisi tunatumia taarifa zetu kutokana na taarifa za Serikali ambazo inatupa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ambayo imesomwa na Waziri wa Fedha, mfumuko wa bei kwa kipindi kilichopita ilikuwa asilimia tatu na mfumuko wa bei tarajiwa ni asilimia tano kwa mwaka ujao wa fedha. Sasa leo wanatuletea ushuru wameongeza kwa *level* ya asilimia 30 na wamepunguza sasa hivi baada ya Kamati kwenda asilimia 20. Sasa unajiuliza kwa mwaka ujao wa fedha, unaoanza kesho kutwa; hivi mfumuko wa bei tarajiwa ni asilimia tano ambayo wameisema ama ni asilimia 20 ambayo wametumia kutoza ushuru wa bidhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa Serikali ikalijibu hili kwa sababu wazalishaji wa bidhaa hii na taarifa na tafiti zinaonesha kwamba kwanza kuna utitiri mkubwa wa bidhaa haramu zinaitwa, bidhaa ambazo hazikidhi vigezo. Vile vile tunaambiwa asilimia 51 ya Watanzania ama ya bidhaa za pombe kali mitaani; kuna asilimia 51 za bidhaa za pombe kali haramu ambazo *TRA* wameshindwa kuzi-*track*, hivyo basi hazilipi kodi. Sasa kutokana na kutengeneza mazingira magumu ya kikodi, tutapelekea sasa, Watanzania watatoka kwenye bidhaa ambazo zipo kwenye mfumo rasmi watakwenda kwenye bidhaa ambazo haziko kwenye mfumo rasmi; wao wataathirika lakini zaidi Serikali itakosa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia Serikali yenyewe inatuambia uchumi wetu kwa kipindi kilichopita tulitarajia ungekua kwa asilimia saba, lakini ume-*drop* kwa asilimia tano. Tunaambiwa pato la Taifa ambalo ndio mkusanyiko wa shughuli mbalimbali za kiuchumi za Taifa, tulitarajia lingekua kwa asilimia saba, limekua kwa asilimia 4.8. Sasa shughuli za kiuchumi zime-*drop*, sasa inakuwaje leo tunatunga sheria ambayo inakwenda kinyume na sheria yenyewe. Mosi, nimesema mfumuko wa bei uko chini, lakini Wizara wame-*estimate very high*. Pili, shughuli za kiuchumi zime-*drop* kwa sababu pato la Taifa lime-*drop drastically* sasa hivi vitu mbona havi-*relate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mosi nilizungumze hili, kwa sababu wadau wamesema Serikali itakosa mapato.

Mfano tu mmoja wa mdau mmoja wa *Mega* ambaye anazilisha *K-Vant* na najua huku wapenzi wa *K-Vant* mko wengi kweli kweli, amesema kutokana na tozo hii mpya maana yake ni kwamba wao wenyewe kikodi watapunguza bilioni 19, yaani kwa hiyo hiyo kampuni moja tu. Kutokana na *introduction* ya huu ushuru mpya maana yake Serikali itakosa bilioni 19. Kwa hiyo, natarajia vilevile Serikali ije itupe majibu mazuri na yenye tija ili tuweze kuangalia, lakini zaidi kama Kamati ilivyosema ni busara na Serikali inatakiwa itunge Sheria ama ileta mapendekezo mapya ya kodi kutokana na sheria siyo kinyume na sheria inavyosema. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la sekta ya huduma ya fedha. Kwa mujibu wa mapendekezo ni kwamba, kutakuwa kuna tozo kati ya Sh.10 mpaka Sh.10,000. Sasa nina taarifa ya mjumuiko wa wamiliki wa makampuni ya simu, wanaoitwa *TAMNOs* wametoa uchambuzi ufuatao, kwa *transaction* za chini kabisa na *transaction* za juu. Watanisahihisha na watatoa mwongozo sahihi ili Taifa liweze kusikia kwa namna gani wataathirika na hili jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema kwa sasa kwa mfano; mtu akituma Sh.10,000 kwa mtu mwingine anatozwa Sh.350, mtu akipokea Sh.10,000, anatozwa Sh.1,450, anapokea 8,550 kwa hali ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kwa tozo mpya; Halima nikimtumia pesa mtu mwingine, kwa mfano Sh.10,000 nitatozwa 550, nikipokea ile fedha nitatozwa Sh.1,650 ambayo inajumlisha *levy* ya Sh.200 kutokana na huo mchanganuo walioutoa, nitapokea Sh.8,050. Kwa hiyo natumiwa Sh.10,000, napokea Sh.8,050. Sasa tulianzisha huduma za simu ili kuweza kusaidia watu ambao hawawezi kufikia mabanki waweze kupata fedha kwa gharama nafuu. Sasa kwa utaratibu huu nadhani inaleta tatizo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia akasema kwa watu wanaotuma fedha nyingi kwa mfano, akimtumia A, akimtumia B Sh.3,000,000 kwa sasa anatozwa Sh.5,000; B akipokea anatozwa Sh.10,000; maana yake akipelekwa

Sh.3,000,000 anapata katika hatua ya mwisho 2,990,000 kwa sasa. Baada ya *levy* pamoja na tozo zote, naenda kwa *summary* sasa, mtu katika Sh.3,000,000 anapata 2,980,000 yaani 20,000 yote hii ni kwa mujibu wa TAMNOs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hivi ni sahihi, nadhani kuna sehemu tunakosea, maana yake dhamira yote ambayo ilifanya Tanzania tukasifika kama watu ambao tumeweza ku-*simplify* huduma ya fedha, mwananchi wa kawaida kule akaweza akapata, inakuwa *defeated* na mabadiliko haya. Kwa hiyo, naomba Waziri na Serikali ikija ifanye uchambuzi wa kina ili tujue *implication* ya hii gharama kwa sababu sasa hivi mzigo ni mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ambalo nitatoa dogo kama ushauri kuhusiana na kodi ya majengo. Kwa mabadiliko hayo, nusu dakika nimalizie. Kwa mabadiliko haya wamelazimisha mtu awe analipa kwa mwezi, kwa mabadiliko haya, yaani ama Shilingi elfu tano, tano, kama kwa mwaka ni Sh.60,000 ama shilingi elfu moja, moja kama kwa mwaka ni Sh.12,000. Nashauri, kama mtu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi iwe kama mtu anataka kulipa kwa pamoja waweke *provision*, kama anataka kulipa Sh.60,000 yote alipe yote, msilazimishe kulipa...

MWENYEKITI: Mengine andika kwa Waziri. Mheshimiwa Juma Hamadi Omar, jiandae Dkt. Charles Kimei na tutakuwa na nafasi ataingia Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia

Suluhu Hassan, kwa uono wake wa kuleta bajeti ambayo ni ya kimapinduzi. Nimekaa kwenye Bunge lako hili vipindi vinne na nikiwa Waziri katika Serikali hii; lakini sijapata kuona bajeti ambayo ya viwango kama bajeti ya Mama Samia Suluhu, kwa hiyo nimpongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha ni msikivu sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, kama kuna Waziri ambayo ameskiliza maoni yetu basi ni Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba. Kwa kweli tulitofautiana lakini baadaye tukaja ku-*make a consensus*, kwa hivyo tunamshukuru sana; kaelewa matakwa yetu na yeye katupa fikra zake, lakini mwisho wa siku tumefikia malengo mamoja. Nasema nampongeza kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kidogo kuhusu Ndugu yangu Mheshimiwa aliyetangulia. Mheshimiwa aliyetangulia alisema kwamba; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, hasa kwa vinywaji vikali; inatakiwa kwa mujibu wa kifungu 124(2) cha Sheria hii, kwamba vinywaji hivi vikali vitozwe *excise duty* kulinga na *interest rate*, lakini siyo kulingana na *interest rate* na viashiria vingine vya uchumi. Sasa nataka nimwambie ndugu yangu huyu kwamba lengo kubwa la kutoza *excise duty* ni ku-*deter* madhumuni ambayo yalikuwa yanaleta athari au mambo ambayo yaliyokuwa yanaleta athari kwa maisha ya binadamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pombe kali pia ni moja ya jambo linaloleta athari katika maisha ya binadamu, nafikiri atakubaliana na mimi. Kuna wengine wanakunywa pombe, mimi sinywi pombe na wala sijapata kunywa katika maisha yangu; lakini basi angalau unywe pombe hizi bia bia. Unakwenda kuchezea *G/N*, unakwenda kuchezea gongo na kadhalika. Hiyo inaleta athari katika mwili wako ndio maana imekuwa *imposed* hiyo *excise duty of 30%*. Bahati nzuri Serikali imependelea imerejesha to 20%. Kwa hiyo, nafikiri Serikali ingeiacha vilevile 30% ili iwe *deterrent* kwa wale watumiaji wa pombe kali kama hii.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamad ni rafiki yangu sana, lakini hoja yangu; halafu asiwe anajibu, hoja yangu ilikuwa *based* kwenye Sheria ya *Excise Duty* yenyewe anayoizungumza Kifungu 124(2) ambacho kimeelezea mazingira ambayo Serikali inatakiwa izingatie wakati inatoza *excise duty*. Sheria inasema inatakiwa iangalie mazingira mawili; iangalie mfumuko wa bei na iangalie shughuli zingine za kiuchumi. Nataka aelewe mimi *argument* yangu...

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Halima, unachangia au unatoa taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa kwamba Mzee hii ni sheria sio mimi. Sheria iliyoletwa na Serikali na sheria ambayo...

MWENYEKITI: Haya ahsante, Mheshimiwa Hamadi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaweza ukaipokea au ukaipotezea tu kama ilivyo utamaduni.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimefahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema sheria hii imezingatia suala la mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi; na kwa kweli lengo kubwa la kutoza *excise duty* ni ku-*deter* yale mambo ambayo yana athari kwa maisha ya binadamu, hilo ndilo lengo kubwa, namtaka Mwanasheria aende akasome atakuta hiyo. Sasa pombe kali ni hatari kwa maisha ya binadamu *and that's why* ikatozwa *excise duty to that tune*; lakini bado Serikali imekuwa *generous* imepunguza *from 30% to 20%*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nasema hivi, nataka niipongeze Serikali. Kwanza juzi alipokuwa ana-*windup* Mheshimiwa jana au juzi, alipokuwa ana-*windup* Waziri wa Fedha alisema wameongeza fedha za ziada, akataja kwa mfano Elimu ya Juu *to the tune of 70 billion*, ununuzi wa vifaa vya afya *50 million*, TARURA *around 322, 121 billion* miradi ya maji na kadhalika. Hiyo yote ukijumlisha utakuta kwa mfano *563 billion*, lakini *chunk* kubwa inakwenda kwenye TARURA, lakini TARURA tayari kuna vyanzo vyake vya fedha; ambavyo tumeviweka katika bajeti au vimeelezwa katika *Finance Bill* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba; kwanza nampongeza sana kwa kiasi hicho, lakini kinyume na Mjumbe alivyosema kwa sababu *Appropriation Act* tumeshaipitisha, haiwezekani tena kufanyika *supplementary budget*, lakini hapa kitakuja kitu kinaitwa *reallocation within the boards*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kitu kimoja, kwa sababu hii ni pesa nyingi inakwenda TARURA, naomba, naomba, kwamba hii fedha iwekwe kwenye Mfuko Maalum na Mfuko huu ujadiliwe kwenye Bunge kama hizi sheria zinavyotaka na Mfuko huu uwe *ring fenced*; isije ikatokea kutumika katika matumizi mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *finance bill* inapendekeza kwamba zile bidhaa ambazo kuwa zinakuja kwa ajili ya *horticulture* hasa haya mabarafu, kwamba zipunguziwe ushuru au zisamehewe. Nilidhani jambo sahihi kwa sababu *horticulture* ni mapinduzi makubwa sana katika kilimo, nafikiri wenzetu Wakenya sasa hivi wanapata karibu *two billion dollars per annum* kwa *horticulture* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri sisi nafikiri tukwenda kwenue *chain* nzima ya *hotculture* sio hivi majokofu tu madogo madogo na hata hizi *containerized structure* ambazo huwa ni za baridi zile au suala la *greenhouse* pia zingesamehewa kwa sababu kuzihuisha hii sekta ya *horticulture*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama tuna *manage* kupata *two billion dollars* hiyo ni *all most our half of our foreign change raging*, kwa hiyo nadhani Serikali ingekazia sana kuboresha hii *horticulture*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba bajeti hii imeweka mkazo kwenye kilimo, pamoja na kwamba mchango katika bajeti katika kilimo ni mdogo sana lakini *the fact* kwamba imekubalika kupunguza au kusamehe ushuru katika sekta hii basi ni ishira ya kwamba tunaelekea kuzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hivyo, nataka nipendekeza mambo maili, kwanza katika hili kilimo nadhani hii ni mapendekezo haimo kwenye *finance bill*. ni vizuri tukaboresha utafiti sasa hivi Tanzania utafiti wa mbegu bora, utafiti wa mitamba, utafiti wa zana bora za kilimo, sasa hivi Tanzania tuna *issue* za utafiti kama 10, na bajeti ya utafiti, *research and development*, nafikiri ni pesa kidogo sana, ni *around 3.3 trillion* hii ni pesa kidogo sana, kwa hiyo, ni vizuri katika bajeti zinazokuja tuboteshe kuweka fedha nyingi katika utafiti na utafiti unasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo China na Malesia wanatumia *around 3.4 percent of the GDP* kwa utafiti. Kenya wenzetu wanakaribia *one*, sisi hatujafika *one percent of the GDP*. Ujerumani na Korea walitumia *more than five of the GDP* na ndio maana yake Ujerumani leo katika sekta ya magani, *all most cars* katika Dunia zinapatikana Ujerumani *masadis bens*, BMW, Odi. Korea ninahakika ilo si la kubishana lakini wanatoa simu hizi za Samsung ambazo ni *the best in the world*, kwa hiyo utafiti unasaidia, nadhani tu-*concentrate* katika bajeti inayokuja katika utafiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kilimo, tuhimize matumizi ya bwana shamba, *agriculture extension officers*, sisi hapa tuna mabwana shamba wanaofika 7,000 na mahitaji 22,000. Na ni jambo la kushangaza tukilinganisha na wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya *in terms of coffee production* imelima *less hectarage* compere to Tanzania but, Kenya the *yield per hector* ni kubwa kuliko sisi, inamaana Kenya wanatoa kahawa nyingi kuliko Tanzania, *despite the fact* kwamba sisi Tanzania tuna *hectarage* ndogo, kwa hivyo na yote kwa nini, kwa sababu ya bwana shamba, wenzetu wa Kenya wanawatumiwa mabwana shamba wao vizuri sana, wanakwenda mkulima kwa mkulima, mti kwa mti kinyume na sisi, mabwana shamba wetu hawa tulionao 7,000 wanakaa maofisini. Sasa nadhani imefika wakati saivi kwa mabwana shamba wetu wasikae ofisini badala yake waende kwenye mashamba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wao wanakwenda shamba kwa shamba, mti kwa mti, Kijiji kwa Kijiji kitu kama hicho. Sasa na sisi ni muhimu *we should make use our agriculture extension officers*, nasema hivi tukifanya hivi mimi ninahakika *yield per hectare* itaongezeka kwa mazao yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi kwamba nataka niunge mkono kwa dhati, *finance beld* ya Waziri wa fedha, na ninawaomba waheshimiwa wabunge wote tuunge mkono hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kimei, jandae Mheshimuwa Kwagilwa Reuben.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, nianze kwa kumshukuru na kumsifu na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa msikivu na kuelekeza baraza lake la mawaziri vizuri.

Nimpongeze pia Makamo wa Rais nimpongeze Waziri Mkuu, nipongeze baraza zima la Mawaziri, pia nimpongeze sana kipekee kabisa Mheshimiwa Dkt. Nchemba kwa hotuba nzuri aliyotoa jana, na kwa kuwa ni msikivu sana, la tatu nisema kwamba ametendea *Ph.D* yake haki jana, allitoe

mada yake alitoa hoja yake vizuri na ninaamini ndio sababu wengi wanapenda kuchangia kwenye jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ukiangalia mswada ambao umeletwa Mbele yetu, ni mswada ambao unakidhi mataakwa ya kufikia malengo ambayo ni makubwa kwa bajeti yetu ya 2021/2022 pamoja na mpango wetu wa maendeleo ambao nitasema kwamba ni ile miradi ya kielelezo ambayo tunajua itapata fedha, kuendeleza miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii, kujenga mazingira Rafiki kwa wawekezaji, *blue prints* na hasa jana tukasikia Mheshimiwa Waziri anasema nini, kwamba hata *areas* au yale madeni ambayo *privet sector wa contactors* hawajalipwa yanaweza yakalipwa pia kutokana na fedha hii ambayo itapatikana ya ziada, kutokana na ubunifu ambao imejitokeza kwenye kuangalia na kubuni vyanzo vya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ukijumlisha zile fedha ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha jana alizielezea kwamba ni za ziada na zitapelekwa kwenye maeneo mbali mbali, unaona kwamba sasa tunaweza tukakusanya kitu kama tilion 26, ndio mapato ambayo yanayijitokeza kwa hesabu za haraka haraka, hii inamaana kwamba tunakusanya mapato ambayo ni asilimia 17.5 ya pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakuwa tumefanya *tax effort* kubwa sana, kwa hiyo tatizo kubwa letu kwenye hii bajeti na kuhakikisha kwamba tunatekeleza tukae mpango wa kukusanya vizuri, inamaana gani? Inamaana kila mtu Serikalini hata sisi wabunge tuhakikishe kwamba ile elimu kwa walipa kodi inakwenda na kwamba tunafanya kila kinachowezekana ili Serikali ipate pato lake na ili hii miradi iweze kutekelezeka na sera yetu na bajeti yetu iwe na muoleleo huo ambayo sasa unaona kwamba itaendelea kupunguza *in-quality* katika mapato ya watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapotumia fedha nyingi kwenye huduma za kijamii, na kutumia fedha nyingi

kwenye miundombinu ya kiuchumi inamaana kwamba inapunguzia mtanzania, inampunguzia mwananchi wa kawaida mzigo wa kulipa kwa sababu anakuwa amepata bure kama kapata bima ya bure inaama unakwenda kutibiwa bure, inamaana fedha haikuvingia mfukoni mwako lakini imekusaidia wewe sasa kuongeza kipato kwa njia ambayo ni *in direct*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi kwamba nafikiri katika yote yanayo zungumzwa, jambo muhimu ni kutengeneza ile *guideline* au mwongozo wa kutekeleza hizi kodi mpya zilizokuja. Kodi ya luku, kodi ya majengo kupitia luku, kama ile *program* ambayo alikuwa ametueleza Waziri hapa jana, *program* ambayo inatengenezwa kuweza kukusanya kupitia luku. Kama haijakamilika upesi tutacheleweshwa, na inatarajiwa kwamba wakati huu kodi hii ya mapato imebuniwa kutoa au imekadiriwa kutoa fedha nyingi sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kodi inayotozwa kwenye fedha za *mobile money* na *airtime*. Sasa niseme kuna wakati ule tulivyolingiza *extra duty on financial transition*, TRA iliwachukua muda mwingi sana kuja na *guideline* ya kwamba itatozwa namna gani. Nawaomba watu wa TRA wapo hapa wafanye haraka ili kuwa muongozo uende kwa wale wanaohusika wale wadau wetu ambao ni makampuni ya simu na mabenki waweze kujua kwamba wana-*adjust* mifumo yao pia kuweza kukusanya hiyo fedha *electronic*, hiyo ni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni *issue* hii ya uwezo wa *Tanzania Revenue Authority* mamlaka ya mapato, kusema kweli unaambiwa kwamba kwenye majimbo au halmashauri waajiriwa wa TRA ni wachache sana. Sasa kama TRA haitajipanga haitaongezewa rasilimali watu na rasilimali fedha naamini kwamba hatutafika. Kitu kikubwa katika utengezaji wa sheria hii ambayo itakuja kutufinya sisi wenyewe kwa vile tutakuja shindwa kitekeleza na tutashindwa kusimamia Serikali, kikuwa ni kwamba uwezo wa kukusanya hayo mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ni mengi na inaonekana kwamba vianzio ni bunifu sana, naamini kwamba tukikusanya tutafika pazuri na tunaweza kutekeleza malengo yetu ya bajeti na malengo wa mpango wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme hivi kuna mambo ambayo tunaona kwamba yangeweza yakaongeza *revenue base* yetu au *taxi base* yetu, moja ni kufanya Dar es Salaam iwe a *logistic hub* kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa hivyo *unfortunately* Inakuwa na vikwazo vingi lakini moja wapo ni *East African Customs Management Act*, inakuwaje hivi, kwa sababu huku kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki *axle load* inayokubalika ni *maximum thirty tonnes* huku ambako ziko mizigo mingi inakwenda mizigo inapita sasa hivi Dar es Salaam sasa hivi mingi inaenda *SADC*, sisi pia ni watu wa *SADC* ni jumuiya ya *SADC*. Sasa hatuwezi kubeba mzigo iende Kongo inazidi au iende Zambia au iende huko kusini kwetu Mbeya inazidi tani 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utakuta kwamba watu wengi na tunaambiwa na watu wa *TPA* kwamba meli nyingi hasa zinaenda Beira kwa sababu kule wanaruhusu *axle load ya 50 tonnes*. Sasa mimi nataka niseme hivi tujaribu nataka pale wenzetu kwenye jumuiya ya wenzetu *partners* wajue kwamba sisi iyo inatuzuia maendeleo, hiyo ya kuzuia mzigo mkubwa wa *tonne 50* kupita kwenye barabara zetu ni jambo ambalo haliwezi ku-*facilitate industrialization* kwetu kwenye *zone* ya kusini au hata kuwasaidia wenzetu kupitisha mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri hiyo ikitokea inaweza kuwa njia pekee au njia kubwa ya kutupa mapato siku za Mbele. Sasa niseme pia kwamba hili la ushuru wa bidhaa ya pombe tamtam hizi kali, nafikiri hivi ukweli ni kwamba miaka mitatu au zaidi huku nyuma bei hazikuwa zinaongezwa kwa kasi ya mfumuko wa bei, sasa ukichukua *compound rate ya three point of inflation* kwa miaka mitatu tu inakuja 3x3x3 ni 27, kwa hiyo wazee wa fedha inakuja na

30 *it was within*. Sisi tukasema hapana kuja kwenye Kamati ya Bajeti ikasema hapana punguza kidogo ikashushwa ikawa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba hawakuwa nje ya sheria, wako ndani ya Sheria hasa baada ya kushuka kwenda 20. Kwa hiyo, napenda kinywaji changu lakini hiyo hainitishi sana laizima tulipie mfuko wa Serikali ili Serikali ipate mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme kuna suala la hizi fedha ambazo zimeongezewa kwenye maeneo mbali mbali. Sasa kuna pendekezo la bajeti *escalating* inasema kwamba ile wakati bei za mafuta zina *fluctuate*, zikishuka ile asilimia 50...

MWENYEKITI: Ahsante, Dkt Kimei mda wako umekwisha.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: ...kutokana na hiyo inakwenda kwenye kilimo, kwa hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mchangiaji wetu wa mwisho leo atakuwa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia mswada wa sheria ya fedha 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme naunga hoja iliopo Mbele yetu naiunga mkono, baada ya kuiunga hoja mkono nijielekeze kuchangia kwenye huu Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Handeni sehemu ambapo ni Wilaya yenye madini mengi sana, na Muswada huu uliokuwa umeletwa Serikali ilionyesha ni ya kuigusa sekta ya madini kwa maana ya kuongeza kodi. Na hata vifungu ambavyo ame *withdraw*, wamesema wanakwenda kujipanga ili siku za usoni waweze kuanalia namna nzuri ya kutoza kodi kwenye sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwenye *amendment* zilizoguswa ilikuwa ni ile *part 3 amendment of the income tax Act cap 332*, na ile *part 25 amendment of the vocational education and training Act cap 82*. Hii ilikuwa inawataka wachimbaji walipe 0.4 kama *levy* kwa maana ya *SDL*, na ile nyengine ilikuwa inawataka wachumbaji wadogo walipe asilimia 3 kama *income tax*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii nimshukuru sana sana Mheshimiwa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa msikivu sana, kwa kuwa msikivu sana na kuelekeza kwa Waziri wa Fedha wa *withdraw* hizi kwa ajili ya kuwalinda wachimbaji wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa Serikali ime-*withdraw*, na kwa kuwa bado wanafikiria kutoza kodi zaidi siku za usoni, kwa wachimbaji wadogo maana mpaka sasa mchimbaji mdogo analipa asilimia 6 kama mrabaha, analipa asilimia moja kwa ajili ya ukaguzi na analipa 0.3 kama sehemu ya *services levy*, inamaana kodi yake yote mpaka sasa mchumbaji ni asilimia 7.3. Sasa kabla ya Serikali kufikiria kuwatoza zaidi wachumbaji wadogo, ninashauri mambo yafuatayo yafanyike:- (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kumekuwa na taarifa tofauti tofauti za sensa za idadi ya wachimbaji wadogo, hivi tunavyo zungumza si Serikali, si wachimbaji wadogo wenyewe wenye takwimu sahihi za wachimbaji wadogo, kwa hiyo tunaishauri Serikali, sensa hii inayokuja ya Tanzania nzima ikatusaidie kutupa idadi ya wachumbaji wadogo nchi nzima, huwezi kutoza kodi kwenye sekta ambayo hujui idadi ya wahusika, hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tulitunga sheria hapa mwaka 2017, Sheria ya *The Natural Wealth and Resources, Permanent Sovereignty Act 2017*, ambayo iliwawezesha watanzania kumili madini kisheria rasilimali zile, madini kisheria. Sasa watanzania wameshamiliki madini kisheria, Watanzania wanamiliki *PML* Watanzania wanamiliki migodi, lakini

hatujawawezesha Watanzania kuyachimba haya madini, hatujawawezesha watanzania kuchimba haya madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia ile *Mining Act cap 123* ambayo imtungiwa *Regulations Section* ya 129, inasema *The Mining Act Mineral Value Addition Guidelines* ambayo imetolewa kwenye tangazo la Serikali namba 60, tuiipitie upya kanuni hii, tumewamilikisha madini na tumewanyang'anya fursa ya kuyatumia madini haya, kwa sababu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *regulation* hii ilitungwa na wizara inazuia wachumbaji kusafirisha madini ghafi, sikatai kwamba kuna umuhimu sana wa kuyaongeza madini yetu thamani kabla hatujayasafirisha, sio kila madini tunauwezo nayo leo ya kuyaongeza thamani. Kwa mfano wanaposchimba chuma, ukiongelea *valued edition* kwenye chuma unaongelea kufunga *plant* kiwanda cha zaidi ya dola milioni moja, mchimbaji gani mdogo ataweza ku-*afford* kuongeza *value addition* ya chuma hapa, tumewafilisi wachimbaji wa kopa kwa hii na tumeshindwa kuyatumia maadini kama vile *manganese* na zile *pressures mentalis*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba wizara yenye zamana ikapitie upya kanuni hii, tujaribu kuangalia kwa yale madini ambayo tunaweza kuyaongeza thamani kama ilivyo *gold*, kama ilivyo *tanzanite* tuendelee nayo, na kwa madini ambayo bado hatujajipanga tuwaruhusu watu wayachimbe na wayasafirisha yakiwa ghafi. Tukifanya hivyo tutapata kodi nyingi sana zaidi ya hata ambayo mlikuwa mnakadiria kuipata kwa kutoza asilimia tatu, huo ni ushauri wangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nawashukuru sana benki ya *CRDB* kwa kuanza kuwaamini wachimbaji na kuwakopesha, lakini wenzeatu wa Serikali naomba niwaeleze jambo moja, hata kama *CRDB* wameanza kuwakopesha wachimbaji, wanawakopesha kwenye *commercial rate*,

uchimbaji ni *investment* huwezi kumkopesha mtu kwa *commercial rate* afanye uchimbaji, lazima tuangalie namna gani wachimbaji wetu watakopeshwa kwama kufanya *investment*, kwa kuzingatia kwamba *pay back period* ya miradi yao ni ndefu sana na hata *break event point* yao ni ndefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe tu hata hizi kodi tunazowatoza sasa hivi wachimbaji, kuna wengine tunawatoza kutoka kwenye mitaji yao kwa sababu inamchukua mchimbaji muda mrefu sana kutengeneza faida.

Kwa hiyo, anapokuwa amekwenda kuuza madini yake aliyoyapata wewe ukitoza ile 7.3 haimaanishi kwamba yeye atengeneza faida, anaweza kuwa ame-*invest* amepata jiwe ambalo halifanani na thamani ya *investment* yake kwa sasa, lakini wanaendelea kulipa kodi kizalendo sana, kwa sababu wanalipa kodi kwenye *investment* zao, kwenye *capital*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *industry* ni lazima tui-*trite with conscious*, tusiwe tunakuja tu hapa tunataka kutoza kodi, lazima hii *industry* tuilee na lazima tufungue milango kwa sababu hawa wachimbaji hatujawa na uwezo wa kuwawezesha kama Serikali, basi tuwalee ili wao wenyewe waendeleo kujijenga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushuru sana nafikiri nimetumia muda wangu vizuri, ahsante sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu umekwisha, jioni tutakuwa na wachangiaji wa nane tu, sababu tutamaliza saa 12.30, na tutaanza na Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Kigwangalla, Mheshimiwa Mzava, Mheshimiwa Mtemvu, Mheshimiwa Tadayo, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King. Nasitisha shughuli za bunge mpaka saa kumi na moja.

(Saa 07.00 Mchana Bunge lllisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na uchangiaji na mchana nilishamtaja Mheshimiwa Kakunda, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Mnzava.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitoe pongezi tatu. Pongezi ya kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji mzuri. Uwasilishaji wenu tumeuelewa, mlikuwa *very eloquent* lakini *brief to the point*. Hongereni sana, tumewaelewa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za pili, naomba niipongeze nchi yangu Tanzania kwamba kama tulivyomsikiliza Mheshimiwa Mkuchika pale alipopewa nafasi siku ile alivyokuja mara ya kwanza Bungeni baada ya kuumwa alituambia kwamba akiwa India na baada ya kusikia habari ya ile *transfer of power* ambayo ilifanyika hapa Tanzania akapata furaha na amani kwamba sisi Tanzania tuna Katiba nzuri sana ambayo imetuvusha kwenye mawimbi makali. Tumepata msiba ambao Tanzania hapa haujawahi kutokea tangu uhuru wa kufiwa na Rais ambaye yuko madarakani lakini tumevuka salama kwa sababu tuna Katiba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumepitisha bajeti hapa ambayo kwa kazi zake za awali za maandalizi ilisimamiwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa takriban asilimia 70. Baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais kuapishwa kuwa Rais alichukua kijiti kile kwa umakini mkubwa akaendeleza pale ambapo Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliishia na hakutaka kubadilisha vipaumbele bali akaja na

kaulimbiu ya Kazi lendelee kumaanisha kwamba anaendelea na vipaumbele vilevile ambavyo vilikuwa vya Rais, Hayati Dkt. Magufuli. Jambo hilo ni la kujipongeza sana kama nchi, sio nchi zote zinaweza kufikia hatua kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za tatu, nimpongeze Waziri wa Fedha na timu yake yote ya Serikali chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wamekuwa wasikivu kwa hoja za Wabunge humu Bungeni lakini wamekuwa wasikivu kwa Kamati ya Bajeti na wadau mbalimbali ambao walikuja kuwafuata na kujadliana nao. Hii ni hatua muhimu sana na ndiyo maana upitishaji wa bajeti wa jana umevunja rekodi ya miaka 25 iliyopita. Tangu mwaka 1995 Uchaguzi Mkuu wa vyama vingi haijawahi kutokea bajeti ya nchi ikapita humu Bungeni bila kura ya 'Hapana' hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kwa ajili ya Sheria ya Bajeti na sheria hii ndiyo ambayo itahakikisha kwamba tunapata zile shilingi trilioni 36.3 kwamba tutazipata baada ya sheria hii kupita na itumike kuhakikisha kwamba tunapata hayo mapato ambayo tulilenga. Bila sheria hii kupata shilingi trilioni 36.3 itakuwa ndoto. Vipaumbele alivyotaja Mheshimiwa Waziri, elimu, afya, maji, barabara vijijini, miradi mikubwa na uendeshaji wa Serikali. Ni jambo ambalo inatakiwa tutafakari sana tunapozungumzia sheria hii kwa sababu tunahitaji kuzipata hizi shilingi trilioni 36.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana lugha ambayo Mheshimiwa Waziri alitumia katika baadhi ya maeneo kwenye hotuba yake alizungumzia kuhusu kufunga mikanda. Lugha hii imetumika kututayarisha Watanzania kuwa Serikali inakuja na mbinu mbalimbali ambazo zitahakikisha kwamba tunatimiza matarajio yao ambayo walituchagua mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbinu kadhaa ambazo zimeainishwa kwenye sheria hiyo. Mbinu ya kwanza kwa mfano kodi mpya kwenye baadhi ya maeneo, mfano, kodi ya kwenye muda wa maongezi, ukosaji wa kodi za

majengo kupitia malipo ya umeme wa LUKU na maeneo mengine Serikali imeamua kutoa msamaha wa kodi kwa mfano, kuingiza simu janja kutoka nje, hili ni eneo ambalo limesamehewa kodi. Vilevile kuna baadhi ya maeneo kwenye sheria yamewekwa ili kuimarisha ukusanyaji na uhibitwa wa mapato. Mfano, mapato ya bandari, *TCRA* na taasisi nyingine kama hizo kukusanywa kupitia akaunti moja, akaunti kuu. Hii itaongeza uhibitwa wa mapato, hongera sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati na mbinu hizo, naomba niishauri Serikali katika maeneo machache yafuatayo. Kwanza, fedha zote ambazo zitapangwa kwa ajili ya miradi ya kipaumbele, hiyo ya barabara vijijini, barabara za mitaa ambako hakuna barabara, maji na miradi ya afya na elimu ile ambayo iliongezwa, kama haitakuwa *ring fenced* itatumika kwa kazi nyingine. Hata kama fedha itaingizwa kwenye Mfuko wa Barabara maana hakuna sheria nyingine, ziende zikiwa *ring fenced* ili zisitumike kwa matumizi mengine bali kwa yale yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili kwa sababu Serikali iliahidi jana maeneo yanayokaribia shilingi trilioni moja na Mheshimiwa Waziri akasema tunawaongezea sekta. Mimi najua ni mchumi, mtaalam wa bajeti kabisa, kama Serikali haina mpango wa kuleta *mini budget* mwezi Desemba au Januari mwakani, maana yake ni kwamba kutakuwa na *re-allocation* ya kupunguza kwenye baadhi ya mafungu kupeleka kule ambako Mheshimiwa Waziri alitaja kama ni vipaumbele. Kwa hiyo, ni vyema Bunge lako Tukufu likapata angalau *hint* kwamba ni mafungu gani ambayo yatapunguziwa hizo fedha ili ziende kwenye yale ambayo Serikali sasa imekuja na zile ahadi ambazo Mheshimiwa Waziri jana alizitamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli mimi baada ya kusema hayo, nisingependa niongeze maneno mengi yanaweza yakachafua utaratibu. Kwa hiyo, niseme

tu naunga mkono hoja ya Waziri kuipitisha sheria hii, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nami naomba nitoe mchango wangu kidogo kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza utahusiana na Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220 hususan yale mapendekezo yanayowekwa kwenye kifungu cha nyongeza cha 4A(a). Kimsingi hapa nakubaliana sana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti yote kwa ujumla wake lakini napenda tu kuweka msisitizo kwamba pengine imefika wakati sasa Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa barabara za vijijini kiuchumi na kijamii ikafanya maamuzi mahsusi na ya haraka kabisa ya kuanzisha Mfuko wa Barabara Vijijini. Naamini hili litakuwa ni kiini cha kuleta mabadiliko makubwa katika namna ambavyo *TARURA* itafanya kazi yake kwa tija na kwa ufanisi kwenye kujenga barabara za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halihitaji kusisitizwa sana kwa sababu umuhimu wa barabara unajulikana kiuchumi lakini pia kijamii. *TARURA* uwezo wake umeonekana kuwa mdogo sana sana kifedha lakini pia hata kiufanisi kutokana na kwamba bado ni taasisi mpya, changa na inahitaji Serikali iwekeze nguvu zake kwa kiasi kikubwa ili iweze kutufikisha kwenye malengo tuliyokusudia wakati tunaanzisha *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuanzisha Mfuko maalum wa Barabara Vijijini itasaidia hivi vyanzo vyote mbalimbali vya mapato ambavyo ni kwa malengo ya kuboresha ujenzi wa barabara vijijini basi pesa hizi ziende kule moja kwa moja badala ya kuingia kwenye Mfuko Mkuu Hazina ambapo tuna mashaka pengine kunaweza kukawa na ucheleweshwaji lakini pia kunaweza kukawa na urasimu

mkubwa. Tunaona ni vyema tuungane na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwamba uanzishwe Mfuko Maalum wa Barabara Vijijini na hili liwe ni jambo la kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Marehemu Benjamin Mkapa Mungu amrehemu alianzisha huu Mfuko wa Barabara ambao leo hii umetuletea faida kubwa sana katika ujenzi wa barabara hapa nchini. Mimi napenda na Mama yetu naye Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aanzishe Mfuko wa Barabara Vijijini na hii iende ikawe *legacy* yake kwa sababu nchi inasonga mbele sio kwamba inarudi nyuma ama inabaki pale pale, hatuwezi kubaki na mambo yale yale machache ambayo yalifanywa na viongozi waliotangulia. Ni wakati kwa sisi kama Bunge kusimama kwa nia ya dhati kabisa kumshauri Mheshimiwa Rais wetu naye aweke *legacy* yake kwenye eneo la ujenzi wa barabara vijijini jambo ambalo sisi Wabunge na wananchi linatugusa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuchangia ni kuhusiana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kuhusiana na mabadiliko ambayo yalikuwa yameletwa na Serikali kwenye Muswada ambapo *produce cess* ingepaswa kuondolewa halafu mapato yake ikawa kama shirika ama kampuni imelipa *service levy* basi hiyo itoshe kuwa ndiyo kodi pekee ambayo ingetozwa kwa shirika husika. Hili ni jambo lenye hatari kubwa sana hususan kwa zile Halmashauri ambazo zinategemea kupokea mapato yake kutokana na mazao zaidi kuliko kitu kingine chochote kile. Halmashauri zenye mazao ya pamba, tumbaku, korosho, chai na kahawa kwa kiasi kikubwa sana zinategemea *produce cess* kama chanzo kikuu cha mapato ya kuendeshea shughuli zake. Hivyo, naomba jambo hili kwa kweli lisitishwe na lisipite kama ambavyo nimeona pia Kamati ya Bajeti wamependekeza kwamba Serikali isite kwa sasa basi na mimi naungana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nalopenda kuchangia linahusu Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289 ambapo Serikali imekuja na mapendekezo mazuri sana ambayo yanaelekea kuanza kutoza Kodi ya Majengo kwa

kutumia LUKU za umeme. Hili ni jambo zuri lakini jambo hili bado halijaeleweka vizuri, lina mashaka na wasiwasi mkubwa kutoka miongoni mwetu Waheshimiwa Wabunge lakini pia hata kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama msamaha ambao unawekwa na Sheria ya Majengo kwenye kifungu chake cha 7 kuna baadhi ya makundi ambayo yanapewa *exemption* ya kutotozwa *Property Tax*. Pia kuna vijiji na maeneo mengine vinapewa msamaha wa kutotozwa *Property Tax*. Tutakapoanza kutoza kwenye LUKU inaweza ikaleta tafrani namna ambavyo itakuwa inatozwa kwa sababu baadhi ya nyumba ambazo zina LUKU na ukizingatia mafanikio makubwa ambayo tumepata kwenye umeme wa vijijini maana yake watu wengi wamepata *access to electricity* na kwa maana hiyo wameweka umeme kwenye nyumba zao na hivyo, wote hawa tukisema tunawatoza tutajikuta tunapata changamoto kwenye namna ya kuwabagua wale wa vijijini hususan vijiji ambavyo vinapewa msamaha na Sheria ya Majengo lakini pia yale makundi mbalimbali kama wazee wenye umri wa miaka zaidi ya 60 ambao pia wanapewa msamaha kwenye Sheria hiyo ya Majengo kwenye kifungu cha 7, kutakuwa na changamoto kubwa sana ni namna gani tutawabagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ifanye utaratibu wa kurekebisha Mfumo wa LUKU hususan mfumo wa TEHAMA ili uweze kubaini na kutambua makundi pamoja na maeneo ambayo yanapewa msamaha. Vinginevyo hili jambo litatuletea *political catastrophe* kwenye majimbo yetu ambapo wazee na watu wa vijijini wanaweza wakajikuta wanatozwa kodi kinyuma kabisa cha sheria na ikaleta usumbufu mkubwa. Kwa hivyo, kabla ya kuanza kuitekeleza, Serikali wawe makini sana kwenye kurekebisha mfumo wake wa ki-*electronic* hususan unaohusiana na LUKU. Ni jambo zuri lakini lazima tuliendee kwa tahadhari kidogo ili lisituletee changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba kwenye sheria nimeona

kuna mapendekezo ambapo Serikali ingependelea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aende akakague mashirika na kampuni ambapo Serikali ina hisa hata ambazo ziko chini ya asilimia 50. Hili pia naona kama ni jambo ambalo haliendani kabisa na mifumo ya uendeshaji wa makampuni (*corporate governance systems*) kwa sababu kwenye *corporate governance* wenye mamlaka ya kuamuru nani akakague wapi ni Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni husika. Bodi ya Wakurugenzi inakuwa *formulated* kwa kiasi kikubwa kutokana na wabia ambao wana nguvu kubwa kwenye hiyo kampuni kwa maana ya kuwa na *shareholding power* kubwa kuliko wale ambao ni *minority shareholders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama Serikali ni *minority shareholder* kwenye kampuni haiwezi kuelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akaenda kukagua kwenye kampuni ambako kuna *majority shareholders* ambao ndiyo wanaunda Bodi ya Wakurugenzi na ndiyo ambao wanaimiliki na kuiendesha kampuni husika. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo pia napenda kupendekeza Serikali ikaridhia likaondolewa kwenye sheria ili kutoleta tafrani lakini pia kutokuathiri utendaji wa kiutawala bora ambao tunaenda nao katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano nalopenda kuzungumzia linahusu Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 hususan kwenye yale mapendekezo ya Serikali ya kutoza asilimia 2 kwenye mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kwenye ile sheria wanasema kama ni kampuni au ni shirika litatozwa asilimia 2 ya mazao ambayo itanunua lakini kama ni *AMCOS* ama ni Ushirika haitatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoza kupitia kampuni hata kama kampuni hailipi moja kwa moja tozo hii itamfikia yule muuzaji kule mwisho kwa maana ya mkulima ama Chama cha Ushirika. Hata tunapoamua kwamba tusitoze kwa *AMCOS* tukiamini kwamba ni wakulima wetu ama kwa *cooperative union*, bado tunapotoza kwenye kampuni *automatically* tumetoza hadi kule kwa mkulima. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linapaswa pia kutazamwa. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, muda wako umekwisha. *(Makofi)*

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajandae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu wa Sheria muhimu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru na kumpongeza sana mtoa hoja kwa maana ya Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri na usikivu mzuri waliokuwa nao kusikiliza na kukubali na kuthamini maoni na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kipekee sana niipongeze sana Kamati yetu ya Bajeti imefanya kazi nzuri na kwa hakika imefanya kazi kubwa kwa niaba ya Bunge lako hili. Tunawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hii nzuri waliyoifanya nimeona nichangie kwenye maeneo tu machache; na sehemu kubwa ni pongezi kwa sababu kazi kubwa imefanyika ya kurekebisha Muswada huu tofauti na vile ambavyo ulikuwa umesomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwani kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Simu, marekebisho yaliyofanyika, na haswa ule ushauri wa Kamati wa kuweka ukomo wa vile viwango, ni jambo kubwa sana na inatusaidia hata wananchi wetu wanaona ni namna gani ambavyo pamoja na kwamba tunazihitaji kodi kwa ajili ya maendeleo, lakini wakati huo pia tunaendelea kuzingatia

namna ya kupunguza huu mzigo kwa wananchi wetu. Niwapongeze sana kwa jambo hilo zuri ambalo tumelifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwenye mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220, amesema hapa Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kigwangala; Mheshimiwa Waziri jana amesema hapa kwamba hela hizi hazitaguswa, zitakwenda moja kwa moja. Ili jambo hili liwe na tija ambayo inakusudiwa ni lazima tuliwekee utaratibu ambao uko wazi zaidi tofauti na ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubaliane Mfuko wa Barabara umefanya kazi kubwa na unafanya kazi nzuri, lakini kwa kuwa tuna chanzo cha fedha cha kueleweka kwa ajili ya shughuli za *TARURA*, ni lazima tufikirie na tukubaliane kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya barabara za vijijini. Tukianzisha mfuko huu maalum maana yake ni kwamba, fedha hizi zikipatikana; huko zinakopatikana na huko zinakokatwa, zitakwenda moja kwa moja kwenye mfuko huu kufanya kazi ambayo imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linaweza kuja kuwa jambo la baadaye huko tunakokwenda, lakini kwa sasa tukiwa bado hatujaenda kufanya mabadiliko ya sheria kwenda kuanzisha mfuko huo, Mheshimiwa Waziri kwanza tukaangalie kwenye zile kanuni, tukaziboreshe ili kwa sasa pia kanuni zile ziseme wazi kuhusu mapato haya na mgawanyo wake tunaokwenda kuongeza kwenye ule mfuko wetu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nizungumze kuhusu marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Nilichangia hapa na nimesema nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa usikivu, nimeona mmesema mmeamua kuondoa mapendekezo ya marekebisho mliyokuwa mmeyaleta yale, tunawashukuru sana, ni jambo zuri, mnakwenda kutusaidia, lakini tutakuwa hatujafika mwisho wa jambo letu, lazima huko mbele ya safari tuangalie

namna ya kufikisha jambo hili kwenye hatua ya mwisho.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokuwa tunakisema hapa, kabla ya 2014 Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Kifungu cha 16 (7), kilikuwa kinasema tu kwamba *Service Levy* inayolipwa, italipwa hivyo hivyo kwa kiwango hicho hicho, kwa wenye viwanda ndiyo utakuwa ushuru wa viwanda. Mwaka 2014 yakafanyika marekebisho tukaongeza pale kwamba, *cooperate entity* ambayo imelipa *Service Levy* haitalipa *produce cess*. Tukawa na mgongano hapo kidogo, sisi wengine tukaenda kutengeneza sheria ndogo ili itusaidie kuweza kukusanya. Yalipokuwa yanakuja marekebisho haya ambayo yalikuwa yanapendekezwa mwanzoni, yangefanya zile sheria ndogo zisiweze kufanya kazi, tungeweza kuzifunga mikono. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa kuondoa yale mapendekezo, tumebaki tulivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate suluhu ya mwisho ya jambo hili mbele ya safari huko tukakirebishe hiki kifungu cha 16 (7). Tuynakirekebisha kwa sababu gani? Wenzetu wa Wizara ya Kilimo ndiyo wanasema sana hoja hii kwamba, hawa wenzetu wasilipe tozo mbili mbili, kwamba asilipe *Service Levy*, pia akaja akalipa na *Produce Cess*, lakini hizi ni tozo mbili tofauti, zinalipwa na watu wawili tofauti na kwa namna tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria ya Fedha anayelipa *Produce Cess* ni mnunuzi, anayelipa *Service Levy* ni huyu ambaye anafanya shughuli pale kwa huduma anazozifanya. Changamoto ambayo inakuja, wako baadhi ya wazalishaji ambao wanunuzi wao hatutakuja kukaa tuwajue kwa kuwa wanajua wenyewe wanakokwenda kulipata soko; na wanunuzi wengine hawatakuja kuingia kwenye hii nchi, watapelekewa mzigo huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikibaki hivyo, Halmashauri nyingine zitashindwa kupata fedha kwa sababu wanunuzi hawapo. Mmeandoa yale marekebisho, siyo *by law* itakwenda kutekelezeka, lakini ziko Halmashauri ambazo ili

ushuru huu waukusanye, ni lazima wakatengeneze sheria ndogo ambazo zitazuia mazao haya yasitoke kwenye mamlaka ya Halmashauri kabla ya kupewa kibali na Halmashauri na kibali hicho kisitoke kabla ushuru huu wa mazao haujalipwa. Hao watafanya vizuri. Wasipotengeneza hiyo, hakuna watakachokipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa usikivu wake, lakini nashauri ni lazima tunakokwenda mbele ya safari tuone namna ya kukiboresha zaidi kifungu hiki ili kuondoa aina yoyote ile ya utata ambayo inaweza ikajitokeza. Sisi kwa mfano Mkoa wa Tanga sasa hivi itakuwa ni rahisi tu, mabadiliko aliyoyaondoa *by law* yetu itafanya kazi, tutaendelea kukusanya mapato yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Mtoa Hoja, mabadiliko ni mazuri na marekebisha ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mtemvu, jiandae Mheshimiwa Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwijage.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021. Kabla sijachangia, nitumie nafasi hii kwanza nami nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kupiga kazi yenye mfano wa kutukuka kabisa kwenye nchi yetu, Afrika na dunia nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza kwa jinsi ambavyo amefanya uteuzi ulio mzuri. Katika jambo hili tulionalo muda huu, ni uteuzi alioufanya juu ya Daktari Mheshimiwa Mchemba Lameck kuwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa

Mhandisi Masauni na wale Makatibu Wakuu na Makatibu Wakuu Wasaidizi wawili. Kwa kweli wanaisaidia Wizara hii ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *declare* kabisa, ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Natumia nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wetu, kaka yangu Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini akiwa pamoja na Makamu Mwenyekiti wetu CPA Omar Kigua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo machache ambayo nitajaribu kusema. Eneo la kwanza ni sehemu ya tano ya mikopo, dhamana na misaada, Sura ya 134. Hapa marekebisho yamefanyika kwa kuweka kifungu kipyua cha 13(b), lakini marekebisho haya kwenye Muswada yamefanyika ili kuruhusu Serikali kuweza kudhamini kampuni zetu au taasisi za Umma ili ziweze kukopesheka, lakini dhamana yetu tuliyoiweka pale ni katika kiasi cha *share* tunazozimiliki katika kampuni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema. Hata kwenye sheria iliyopita siyo kwamba Serikali ilikuwa haiweki dhamana. Ilikuwa inaweka dhamana kwa kiwango cha asilimia 70 ya mkopo wote ambapo hiyo taasisi au hiyo kampuni inaenda kuchukua. Asilimia 70 tu ya mkopo wake wote, lakini sasa tumebadilisha tunaenda kuweka *share* zetu ambazo tunazo pale ndiyo kiwango ambacho tunakubali kuweka dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme ukweli, kwenye hili CAG kwenye ripoti ya miaka mitatu mfululizo 2018/2019 na 2019/2020, amekuwa akisema juu ya kutokuwa na maadili timilifu, kutokuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha, kutokuwa na nidhamu hata pale tunapokopesheka kusimamia mikopo tuliyopewa au dhamana na Serikali.

Kwa hiyo, nasema hili, kwa sababu pia umekuwa ushauri wa Kamati juu ya kuona jicho letu likae vizuri pale wakati tunatoa dhamana hizi ili zitusaidie tusije tukaenda chaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maangalizo ya msingi kabisa, maangalizo kama *inflation* (mfumuko wa bei), tukishatoa au tunataka kutoa dhamana, tuangalie hilo jambo. Muhimu sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo *issues za international pandemic*. Umeona katika miaka miwili mfululizo tumedhuriwa sana na jambo la *Covid 19*. Kwa hiyo, kuna mambo kama haya lazima macho yetu yawe vizuri ili tusije tukaliingiza Taifa kwenye deni kubwa ambalo likishindwa kulipika linaenda kwenye deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niseme jambo hilo. Jambo la pili la marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo Sura ya 437. Hapa Marekebisho ya Muswada wa Sheria tumefanya katika Kifungu 46 (a) na dhumuni lilikuwa ni kuweka tozo katika kila muamala wa kutuma au kutoa fedha kwa kiasi kinachotofautiana tofautiana. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumeweka wazi kabisa itakuwa ni shilingi 10 mpaka shilingi 10,000. Asubuhi hapa yupo mmoja amejaribu kutoa mfano na niuweke sawa. Alisema, kuna mtumaji na mpokeaji na mfano akaweka shilingi 10; ikitumwa kwa zamani, ina-charge shilingi 360; ikitumwa leo, ina-charge karibu 560. Huyo ni mtumaji; lakini mpokeaji wa leo, kwenye kutuma ile atapokea kwa shilingi 1,450 maana yake kuna hela ya kutolea, lakini kwa leo itakuwa imeongezeka 1,650. Yaani kuna maongezeko ya shilingi 200. Hapa ikawa ni *issue* sana asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, dhumuni letu kwenye hili ni kuongeza wala tusiwe na mashaka juu ya kuongeza shilingi 200, ndiyo lilikuwa dhumuni letu, lakini nini *implication* ya kuongeza? Naomba niseme, sababu ya kuongeza Watanzania na wana-Kibamba wasikie; moja, ilikuwa iweze kutusaidia kwenye elimu ya juu. Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa, katika mwaka 2019/2020 takribani watoto 11,000 wamefaulu na wameshindwa kwenda shule, lakini ametenga takribani shilingi zisizopungua bilioni 70

kuwasaidia watoto wa aina hii na ndio nia yetu sisi Wabunge wote. Tunaona watoto wetu wanafaulu wanashindwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, mimi sio wa zamani sana kwa umri wangu, lakini wakati mimi ninasoma, kufaulu ni kuchaguliwa tu, lakini wako wengi katika watoto 200 wanaenda 18 wengine wote wanaitwa wamefeli, lakini wala Serikali ilikuwa haihangaiki kuongeza madarasa, wala kutafuta hela nyingine za watoto wasome, lakini leo hii Serikali sikivu imesikia hii Awamu ya Sita, inaona jinsi gani kila mtoto anayefaulu apelekwe shuleni. Hii ni pongezi kubwa kwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, lakini pongezi kabisa kwa Waziri mwenye dhamana na timu yake yote kwa jinsi ambavyo wamejipambanua kuona watoto wetu wanaenda shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo eneo hilo tu, imetusaidia hata katika eneo la afya. Takribani shilingi bilioni 123 baada ya haya mambo kukusanywa, shilingi 10/= wakilipa kwa *transfer* au kuhamisha miamala hadi 10,000/= kuna shilingi bilioni 123 upande wa afya. Zinaenda kufanya nini? Watanzania wasikie, wananchi wa Jimbo la Kibamba wasikie. Kuna maboma karibu 10,000 ya vituo vya afya na zahanati, ambayo yamekaa huko hayajaisha. Kila Mbunge atapelekewa maboma 10. Hii ni faida kubwa, haiwezi kutokea bila fedha. Fedha ni lazima ziwe za kwao, zitokee ili waweze kuhudumiwa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliseme hilo, lakini lipo jambo lingine. Kwenye ushuru wa muda wa maongezi, kwa haraka, shilingi 10 hadi shilingi 200 *implication* ni ile ile. Hapa kazi kubwa imefanyika na wananchi wajue, wale wadau tuliowahi kukutananao wengine wanasema kuna hasara, shilingi 500 hadi shilingi 1,000 ni watu zaidi ya asilimia 94. Sisi tunasema sawa. Kama shilingi 500/= hadi shilingi 1,000 ndio wako asilimia 94 ya watumiaji, sisi tunaenda pale pale tukaweke hata shilingi 5. Eeh, shilingi 500 ya muda wa maongezi, hadi 1,000 sisi tunaweka shilingi 5 ili kila Mtanzania aone *pinch* ya kutaka kuona barabara nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesema Jimbo la Kibamba nje ya barabara zetu zile za juu pale kilometa tano, nyingine zote za udongo, watapataje barabara ya *morrum*? Kilometa 3,101; kilometa 319 zote ni za vumbi na udongo. Lazima walipe hata shilingi 5/= kama siyo shilingi 10/= ili tuweze kuyapata haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Sehemu ya Kumi na Nne, Sehemu ya Tisa na Sehemu ya Ishirini ya Sheria ya Bandari, Sura ya 116, Sheria ya Wakala wa Meli, Sura ya 415 na Sheria ya Mawasiliano, Sura ya 172. Ninataka kusema nini? Wengi wamesema hapa, tunayo *TASAC*, tunayo *TCRA* na tunayo *TPA*. Zote hapa, nimefurahi sana, Mheshimiwa Waziri umebeba hizi vizuri. Tumeenda kupeleka fedha zao zote zile mbichi kabla hawajatumia kwenye mfuko maalum pale *BOT*, lakini kuna maangalizo. Jambo ni zuri, tukasema tunawatangulizia miezi miwili halafu baadaye mwezi mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa na nilisema na kule, tujaribu kuwapelekea miezi mitatu mitatu wakajisimamie kutokana na changamoto nyingi walizonazo. Mbili kwenye nyingi ambazo wanazo kwa mfano wa *TPA*, tayari wameingia *MoU* wao na watu wa reli ili waone jinsi gani mashehena yanatoka kwenda kwenye bandari kavu. Sasa tukiwasimamia sana kwenye kufanya *approval* za fedha, zitatuletea shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni usafiri wa Dar es Salaam. Tunaona kuingia na kutoka bandarini ni changamoto sana ya foleni. Wana mipango mizuri kama bandari kuona jinsi gani wanatengeneza barabara zile, sasa hela tunawashikia tuzitoe kwa wakati ikibidi ili waweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kumaliza ni eneo la Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Nimefurahi sana, niliongea hapa wakati nachangia bajeti; na nimsifie sana, nilimwita Baba yangu Mkwe, Mzee Mheshimiwa Lukuvi, amefanya vyema. Tulikuwa tunaongelea *premium* hapa, ilikuwa asilimia 2.5 kuipunguza kwenye upimaji wa kawaida,

lakini 1% kwenda chini kwenye upimaji wa urasimishaji. Zote kaziondoa 2.5% na ile 1% kupeleka 0.5%, pongezi sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii na Naibu wako, ni wasikivu kweli. Ninawashukuru. Maana yake nini? Wananchi sasa wanaenda kupata hati. Hati ambayo ni dhamana ya Serikali, dhamana ya Wizara kutoa Hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile kampuni zilikuwa zinaishia kupima na kuthaminisha tu, ambapo mlipunguza kutoka shilingi 200,000 hadi shilingi 150,000. Nyie sasa mmefanya vyema, mkatoe hati kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja bajeti ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii ni mgeni wake Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni. Amemleta Mtaalam wa kuchora picha, ambaye amechora picha ya Mheshimiwa Spika, Ndugu Edgar Kayange. Karibu sana. Amekuja kumpongeza Spika, kwa umahiri wake na kuliendesha Bunge. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wasanii wa *Bongo Movie* kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Menina Abdulwakil na Ndugu Atik Wakil.

Mheshimiwa Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwijage.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote niungane na wenzangu wote kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa kuweza kuendeleza kwa kasi mambo yote yaliyokuwa yakifanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, lakini pili kama alivyoahidi

mwenyewe, kuleta mambo mengine mapya mazuri kwa ajili ya nchi yetu na mojawapo ya mambo mapya ambayo ameyaleta ni bajeti hii ambayo leo hii tunaendelea kuijadili hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu wake na timu yote kwa kuaminiwa kuleta na baadaye kusimamia bajeti hii ambayo imeamsha matumaini makubwa sana kwa Watanzania katika Nyanja mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo kazi kubwa sasa ambayo inahitaji uzalendo mkubwa sana ya kusimamia haya ambayo tumeyakusudia na kuyapitisha kwenye bajeti hii. Yako mambo ambayo yanahitaji umakini na ushirikiano mkubwa siyo wa TRA au Wizara ya Fedha peke yake, lakini Wizara nyingine pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, yale marekebisho yaliyopendekezwa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438, juu ya kuwataka wale ambao wanaweka kumbukumbu zao ki-*electronic* kuwa na *servers* hapa Tanzania. Kubaini jambo kama hili kwamba ni yupi anayo *server* hapa ndani na yupi hana, linahitaji ushirikiano mkubwa na pia ni uzalendo, kwa sababu watu hawa wanakuja na teknolojia, kama wanakuja kwenye vita ya kiuchumi. Kwa hiyo, tunahitaji umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kodi, kuna kuwa na pande mbili; kuna upande wa Serikali ambayo ndiyo inasimamia kutoza kodi halafu kuna upande wa yule mlipa kodi. Sasa kwa upande wa Serikali, majukumu yake nafikiri yanaeleweka, ambayo tumeyaona sana kwenye bajeti hii yakizingatiwa ya kuweka mazingira wezeshi ya kumwezesha yule mlipa kodi kuzalisha ili aweze kupata kodi ya kulipa, na pia kutoza kodi au kuweka viwango vya kodi ambavyo vinashabihiana na kipato cha yule mlipa kodi; tatu,

kuwa na mifumo rafiki ya ukusanyaji kodi; na la nne, kuweka sheria zisizo na utata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Kodi zinapaswa kuwa sheria ambazo hazina utata, kwa sababu kodi mwisho wa siku inagusa haki ya kikatiba ya mtu ya haki ya kumiliki mali. Kwa hiyo, sheria zake zinapaswa ziwe *precise* na ziwe pia rahisi kueleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano wa sheria moja ambayo utata wake unaleta matatizo kwa watu. Kifungu cha 90 cha Sheria ya Kodi ya Mapato (*Income Tax Act*) kinachozungumzia juu ya masuala ya *Capital Gain Tax*; kifungu kile hakikuwa wazi juu ya suala la mtu anapotoa ardhi yake au mali yake kwa ule mfumo ambao tunasema wa *natural love and affection* kama baba anapompa mtoto au babu anapompa mjukuu. Sheria pale haikuweka wazi kwamba hawa hawatalipa *Capital Gain Tax* kwa sababu *Capital Gain Tax* ni pale ambapo mtu anapata faida inayotokana na kile alicholipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ziko *property* nyingi ambazo zimekaa bila umiliki wake kurasimishwa kwa sababu wale wazee wanaowapa watoto wao au wababa wanaowapa wake zao au akinamama wanaowapa waume zao wanakuwa pengine wakati huo hawawezi kulipa *capital gain tax* na *in fact* hawapaswi kulipa. Kwa hiyo hii ndio inanifanya niseme kwamba sheria ya kodi inapaswa kuwa *precise* na pia iwe rahisi katika kuitafsiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine la Serikali ambalo hasa linakwenda sana kwa walipa kodi wadogo ni kutoa elimu ya mlipakodi. Wakati mwingine watu wanakuwa waoga wa kodi kwa sababu tu ya kukosa elimu ya mlipa kodi. Utakuta mtu mdogo ana-raise *invoice* yake analipwa lakini anakatwa *withholding tax*, lakini kufuatilia apate ile *withholding tax certificate* ili aweze kupata ile *benefit* ya ile kodi, anakuwa hajui hilo. Kwa hiyo mwisho wa siku mtu ana mzigo mkubwa wa kodi, lakini kumbe anazo nafuu nyingine ambazo angeweza akazipata ndani ya mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona marekebisho ya ile Sheria ya Mikopo na Dhamana za Serikali, Sura ya 134 juu ya masuala yale ya *guarantee* ya Serikali. Kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa hili kwa sababu lilikuwa ni moja ya mambo ambayo yalikuwa yanashangaza kidogo pale ambapo tunakataa au tunachelewa bila sababu kwa muda mrefu kutoa hizi dhamana wakati ambapo mtu anataka kufanya biashara. Ilikuwa inaonekana kama vile pengine hatuwaamini wafanyabiashara wetu. Hili ni jambo zuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kile kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ambacho kinampa mamlaka Waziri kutoa msamaha kwa ile miradi ambayo ina wafadhili. Matumaini yangu ni kwamba katika utekelezaji wake Mheshimiwa Waziri atalisimamia kwa karibu kwa sababu kifungu hiki kimekuwa na changamoto, utakuta labda kuna mradi wa wafadhili wa *package* nzima labda ni dola milioni 20, halafu ikagawanyika katika miradi labda 20. Sasa yapo maeneo mengine na nilishuhudia hili kwangu kwamba, unapofika wakati yule mzabuni anatekeleza ule mradi, anakuwa hapati ule msamaha wa kodi mpaka apate barua rasmi kwa ajili ya mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta iko *GN* kwa ajili ya kusamehe miradi yote iliyofadhiliwa na yule mfadhili, lakini bado inatakiwa tena ipatikane barua kwa kila mradi. Sasa usumbufu ule wakati mwingine miradi inatekelezwa mahali ambapo ni mbali kidogo, ni *remote*, imekuwa ikileta shida kubwa kidogo. Naamini Mheshimiwa Waziri kwa umakini wake ambao tunaufahamu, atalisimamia kwa karibu hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la *Tax Ombudsman*, limekuwepo lakini naona utekelezaji wake umekuwa sio wa makini sana. Hata hivyo, kwa jinsi ambavyo limekuja sasa hivi naamini kabisa litatekelezwa. *Tax Ombudsman* itatusaidia sana kwanza kumpa nafuu mlipakodi, kwamba halazimiki kwenda kupitia ile mifumo ambayo ni migumu, lakini pia itaondoa adha ya kodi zetu

nyingi kushikiliwa kwenye hii mifumo ya kikesi kesi ambayo imekuwa mahakamani au kwenye mabaraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba na kukishauri ni kwamba uteuzi wa hii *Tax Ombudsman* uzingatie sana weledi na uwezo. Pia zile kanuni zitakazotengenezwa, zisiwe tena ngumu zikafanya tena watu wakabaki kuchelewa kama ambavyo ilikuwa kwenye mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na kumpongeza na timu yake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwijage.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hii *Finance Bill* ya mwaka 2021. Langu zaidi ni kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi ya jana. Ahsante kwa kupiga kura za ndio nyote kwa sababu takwimu zinaonesha hakuna kura ya hapana zote ni ndio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapochangia Muswada huu na zaidi nikilenga kuongeza mapato Zaidi, kwa sababu hapa biashara ni kuongeza mapato na namna ya kuwakusanya, nirejee mawazo ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Balozi Bashiru aliwahi kusema kwamba, tunapaswa tuwe na *dialog*, tuwe na mijadala, yaani kuna mawazo yanatoka humu mpaka unafurahi unasema na mimi nikachukue *PhD* ya mawazo yanayotoka humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kitu kinaitwa *transfer pricing*; katika Muswada huu na hotuba ya Mheshimiwa Waziri suala la *transfer pricing* sisi Wabunge hata wataalam wa Serikali inaonekana tunakwenda kufanya maamuzi bila kujua madhara yake. Sielewi kwanini tunakwenda kupunguza *transfer pricing*, nini madhara ya *transfer pricing* wakati bidhaa inatoka au inapoinjia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapoingia bidhaa na *transfer pricing*, yule mwenye faida ata-*trigger price whole*, lakini wewe kama mtoza ushuru bidhaa inapotoka, huyu mtu anapotoka, ataweza kukuletea kukwepa kodi. Naona Serikali hii tuna haja ya kukusanya kodi kwa ajili ya kutimiza malengo. Sasa unapokataa kumtishia mtu kum-*scare* yeye asikwepe hiyo kodi, halafu unamwachia bila kumtoza lolote, hapa naishauri Serikali yangu tuache kipengele hiki kilivyo, tuchukue muda zaidi tuweze kukiangalia zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, Sheria ya Wakala wa Meli, Sura 415; hili suala na lenyewe linapaswa kuangaliwa. Kwanza naiangalia *TASAC* katika mambo mawili; inakiuka sheria za mchezo kwa kuendelea kuwa *operator* na kuendelea kuwa *regulator*. Pamoja na kwamba anakiuka sheria za mchezo, sisi pamoja na kutafuta kodi, tuna maslahi mengine ya ajira, utendaji wa *TASAC* unaviza ajira, tunaweza kukusanya kodi lakini kama vijana hawana ajira tutapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuelewa maelezo yote yaliyoelezwa hapa. Pamoja na kuwaunga mkono watu wa Kamati ya Fedha, lakini *TASAC* anapokamatiwa bidhaa anasema *exclusive right* ya ku-*handle* mafuta, *TASAC* mafuta Anaya-*handle* ili yasiweje? Mafuta yameshughulikiwa, vipimo vimewekwa Wakala wa Vipimo na Mizani, ni Serikali, viwango vimewekwa chini ya *TBS*, bei imewekwa chini ya *Bulk Procurement*; hizi zote ni Taasisi za Serikali *TASAC* anakwenda kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho Serikali haikielewi na napenda niwashawishi hawa watu wanaokwenda ku-*handle* watu wengine wanasaidia kuuza haya mafuta. Nimeandika maelezo marefu kwenye mchango wangu wa maandishi, Tanzania inapaswa kuwa kituo cha kuuza mafuta katika Afrika hii na mafuta utakayoyapeleka *transit* au mizigo ya *transit* kupitia hapa ndio yatakupa fedha zile unazochangisha kwenye shilingi. Kwa hiyo uwepo wa *TASAC* wa kutaka kuchukua kila kitu kwenye mafuta sioni uhalali wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *TASAC* atengwe aende kushindana kusudi tuweze kuleta ushindani, tuache kubweteka, *TASAC* anabweteka, analeta *inefficiency*. Naomba suala hilo tulipitie upya, tuweze kumtoa kwenye maeneo mengine. La mafuta nina vielelezo vyote, hakuna anachoweza kufanya na niweze kusema hakuna anachoelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono Kamati kuhusu suala la anguko la mafuta, *the backwardation and contango*; nimemwandikia Mheshimiwa Waziri somo zuri, mtu anaweza akapata *degree* pale. Hata hivyo, niwakosoe Wajumbe wa Kamati si kila mafuta yanapoanguka bei, makampuni ya mafuta hufaidika, si kweli, anguko la bei tatizo lake ni kwamba halimnufaishi mlaji wa mwisho ndio tatizo lake. Tanzania kuanguka kwa bei hakuwezi kuleta manufaa kwa sababu sisi sio soko huru, ni soko lililodhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa maelezo ya kina na Mwenyekiti wa Kamati nimemwahidi tuje tukae Pamoja, hii ni sehemu yangu ya kujidai. Kwa hiyo kuna mambo yanapaswa kufanyika ili tuweze kupata hiyo faida, lakini nakubaliana kwamba lile anguko lichukuliwe liende *TARURA* kusudi kuweza kufungua barabara za kwetu ambazo hazipitiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu *Government loans, grants and guarantee*. Langu katika hili, Serikali ikakope na ikatole *guarantee*, lakini tujiridhishe tunakwenda kuwekeza wapi.

Niliandika kwenye mchango wa Waziri, hata kwenye mchango wangu wa maandishi kuhusu viwanda. *Msiende kuwekeza pale ambapo hapawezi kulipa yaani kuna viwanda vimekufa hata mngedhikiri uchi haviwezi kufufuka.*
[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kuna viwanda vimekufa hata ungefanyaje, nilijaribu nikashindwa, vikanishinda, hawawezi kuvifufua, Waziri aachane navyo.

Kwa hiyo, Waziri wasiweke *guarantee* pale ambapo hawawezi kupita. Kwa hiyo fedha za *guarantee*, tuna mafunzo mabaya na *guarantee*, tusirudi kwenye makosa yale yale, kwa hiyo tuwekeze kwenye maeneo ambayo...

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji hasa aliposema kwamba yeye alijaribu akashindwa nataka nimpe taarifa na mimi nilijaribu nikashindwa Lindi *Industries*, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwijage unakubali taarifa?

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali taarifa ya mjomba wangu. Kwa hiyo tuwekeze pale ambako kuna fursa kubwa, tuwekeze kwenye fursa kubwa, lakini tunapohitaji *guarantee*...

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo mjomba wangu Mheshimiwa Mwijage afute kauli yake katika suala la kudhikiri uchi yaani hapo amekwenda kwingine. Naomba sana kwa sababu itaingia kwenye *Hansard* za Bunge, halafu litaleta taabu hilo neno, naomba alifute, tafadhali. (*Makofi*)

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa sentensi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *guarantee*, *guarantee* ni muhimu, nachelea upande wa kupata kibali cha Baraza la Mawaziri. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri

na mamlaka husika tuwe na kasi kubwa ya kuweza kutoa hizo *guarantee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu, kwenye *Electronic and Postal Communication Act*; nina uhakika kwa watu wote wenye LUKU, mapato ya *property tax* yatakuwa makubwa kuliko maelezo. Ninachoomba kama nilivyosema mwanzo tunapaswa kujiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, wale ambao hawana LUKU, msiwafuate *manually* kama zamani, fedha tutapata za kutosha, lakini naomba basi tuchukue fedha za kutosha kama nilivyosema mwanzoni wa-*electrify* sehemu zilizobaki. Wanaotaka umeme wako wengi, wawape umeme kusudi waweze kupata *property tax*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia kuhusu mambo ya vibali na wale wanaojiri watu kutoka nje, kama walivyosema Waheshimwia Wabunge, mambo ya *filling* unaposoma vizuri *Blue Print Regulatory Reform* moja wapo ya tatizo ni hii kimbia kimbia, kwenda hapa, kwenda hapa, hii *filling* ingefanyika mara moja kwa miezi sita, *filling* ya vibali ingefanyika mara moja baada ya mwaka mzima ili tuache watu watulie wafanye shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mungu pia kwamba tupo hapa, tunajadili mambo haya mazuri. Ni muda mrefu sasa takribani mwezi wa tatu tupo kwenye jambo hili la bajeti, lakini jana imepita vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ambayo nataka kuchangia. Ni wazi kwamba tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan

kwa mambo mazuri ambayo ameona yafanyike kipindi hiki kwa wananchi wake. Nianze na hili la kutokuwepo kodi kwa waajiriwa ambao wanapata Sh.270,000 kwa mwezi au Sh. 3,240,000 isiyozidi hapo kwa mwaka. Watu hawa ni wengi Tanzania hii, lakini watu hao kwa sasa au waajiriwa hao hawatadaiwa kodi hata kidogo. Kwa hiyo fedha hiyo itakwenda sasa kutumika vizuri katika shughuli zao na kipato chao kitakuwa kimetulia. Niwaombe waipokee hii kama tunu kwa sababu wote wanapodaiwa wa juu na chini inakuwa kwamba ile kodi sasa inawapunguzia kipato hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM ni Serikali sikivu na ilipoona kwamba watu wamepanga sasa kufungua viwanda vya dawa imeondoa kodi kwenye vifungashio vya dawa. Sasa niwahamasishie wote ambao wanataka kwenda kufungua viwanda vya dawa, wakafungue viwanda vingi vya dawa ili matibabu yawe rahisi na kila mtu apate matibabu. Taifa lolote linalokwenda vizuri ni taifa ambalo watu wake wana afya nzuri na watu wenye afya nzuri ni watu ambao wanapata matibabu kwa gharama nafuu. Endapo hiyo kodi sasa imeondolewa, ina maana dawa hizo zikishapatikana vile vifungashio havichajiwi kodi, kwa hiyo watu wataweza kupata matibabu kwa gharama ambayo wanaweza wakaipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hayo tu, niseme wazi kwamba Waziri wa Fedha pamoja na timu yake akiwepo Naibu Waziri na Katibu Mkuu walikuwa na Kamati ya Bajeti kila siku wakihakikisha kwamba vifungu hivi vinapitiwa na vikija hapa vinakuwa salama. Hilo limekuwa hivyo na nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa sababu bajeti hii ni bajeti iliyokubalika ndani ya nchi hii dunia nzima imeisikia na Afrika Mashariki imeisikia, tumwombe Mungu wote tuwe salama tuweze kuja kushuhudia matokeo yake kipindi kama hiki mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jambo moja tu, wakati tukijadili bajeti hii, tulikuwa tumefikiria sana jinsi gani wanafunzi wetu watapata chakula kwa urahisi mashuleni. Hapa naona kwamba endapo sasa ile kodi itaondolewa kule

kwenye mahindi yale, basi wazazi wengi wataweza kuchangia mahindi, maharage ili wanafunzi mashuleni waweze kupata chakula chao kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hainiingii akilini mwanafunzi anashinda kutwa nzima hajala chakula lakini naambiwa kwamba mahindi ni ghali kumbe mahindi yamejaa tele kwenye godauni. Kwa hiyo, niseme kwamba alivyozungumza Waziri leo kwamba jambo hilo amelifikiria na itakuwa salama kwenye kilimo, nimpongeze kabisa kwa sababu sasa mahindi hayo yanaenda kutoka katika bei ambayo inakubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, lakini pia tuliona kiwanda kikubwa cha kukamua mafuta ya alizeti kama ilivyo Singida 'C' kimepunguziwa kodi ili mafuta yale yaweze kupatikana kwa urahisi. Naamini kwamba hata vile viwanda vidogo vidogo, atakapohitimisha Mheshimiwa Waziri, atavifikiria viwanda vyote vile vidogo vidogo vinavyokamua mafuta ya alizeti ambayo tunayakuta barabarani wakati tumnasafiri na yenyewe yanaenda kuondolewa kodi na mafuta hayo sasa yanaenda kupatikana kwa bei inayokubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mafuta hayo yatapatikana kwa bei nafuu, hatutakuwa hapa tunasubiri mafuta yaliyo bandarini, mafuta ya majina ambayo ni ya kigeni sana na wote tutakwenda sasa kulima alizeti yetu tukijua kwamba tunakwenda kupata mafuta kwa bei ambayo inakubalika kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba kuna kesi nyingi ambazo zinakuwa zinasubiri mahakama, lakini Waziri ametueleza kwamba Kamishna wa TRA sasa ameweza kupata nafasi na kukaa na wafanyabishara wale wakubwa nje ya mahakama waweze kufanya mashauriano na kesi hizo ziweze kufanyika na kumalizika. Hili ni jambo jema, jambo hili halitakiwi kumsubiri Rais anavyotembelea mahali apokelewe na mabango au aweze kuitisha wafanyabiashara. Kama Waziri wa Fedha ameshatamka kwamba Kamshna wa TRA

anaweza kuongea na watu hao nje ya mahakama, najua kwamba inaenda kupunguza kesi nyingi sana ambazo zimerundikana na watu hao watakuwa sasa hawana tena tatizo.

Sambamba na hilo hata wale wafanyabiashara wadogo ambao walikuwa wanafunga maduka yao kwa hofu ya kufuatwa fuatwa na *TRA*, sasa wanaweza kwenda kuongea na Kamishna na maduka yale hawatafunga wala hawatafunga biashara zao tena.

Kwa hiyo, nina uhakika Kariakoo inaenda kushamiri, wanakwenda sasa kufanya biashara zao vizuri, kwa sababu jinsi ambavyo alilielezea vizuri Waziri wa Fedha ni wazi kwamba watu hawa wamesikia ahueni, wanaenda kufanya kazi kwa nafuu na wanaenda kufurahia biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ambayo ambayo yalikuwa yanahusu Muswada leo, nilete habari njema kwenu wote. Niseme kwa uhakika kabisa Benki ya *CRDB* ina takribani bilioni tisa na ushee zimekaa hazijadaiwa na hizo ni gawio la miaka mingi kwa watu ambao walinunua hisa *CRDB* lakini hawajui kama walinunua hisa wala wababa wengine hawakuwaambia wake zao na wengine wameshatangulia mbele ya haki. Ninapozungumza bilioni tisa, bilioni tisa ukiweka katika *denomination* ya elfu elfu inajaza chumba kizima. Ni fedha nyingi sana ambazo zinaweza zikabadili uchumi wa eneo la Tanzania kwa mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizo zikishakaa kwa muda mrefu huko kwenye benki ya biashara kama *CRDB* basi muda ukifika *BOT* inaziita ina *call* kwa sababu ni *unclaimed form* yaani hazina mdai. Sasa zikienda zikirudi kule tunakuwa tumepoteza. Natoa rai na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, wananchi wenu ambaye anajua kuna mtu alinunua hisa za awali *CRDB* wakati ule ndiyo hisa zinauzwa, awashauri wakachukue gawio lao kwenye benki yao walionunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo nawaomba sana na namuomba sana Mkurugenzi Mkuu Majid atoe kurasa kwenye magazeti ya nchi hii yaandikwe watu wote walionunua hisa, inaniuma kuona kwamba hela zinakwenda kufungiwa zinaitwa *unclaimed for* wakati watu wanashida na hela. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru ahsanteni kwa kunisikiliza. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante wageni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wasanii wa *Bongo movie* kutoka Jiji la Dar es Salaam ndugu Menina Abdul Wakil na ndugu Atik Wakil karibuni Dodoma. Sasa namuita Mheshimiwa Ali Hassan Omar King wa Jangwani huyu.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nashukuru sana kupata hii nafasi ili tuweze kuchangia mawazo katika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na shairi moja ambalo labda litafupisha maudhui wa hii sheria yetu ya fedha. Kuna mshairi mmoja anasema limelia baragumu wameanza kuuliza mlio wake mtamu wengi limewaliwaza wamepayuka kwa hamu wamo wanacheza cheza lakini wapo wasiofahamu bado linawatatiza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti na sheria yetu hii ambayo tunataka kuipitisha ya fedha ni sawasawa na baragumu ambalo limelia na wengi kweli limewaliwaza hakuna mtu ambaye hajasifia kwenye hii bajeti wala hajasifia hii sheria ya fedha. Kwa hiyo, hii ni sawasawa na baragumu lakini kwa wasiofahamu litawachanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kitu kimoja ambacho ni muhimu sana tunaishukuru sana Serikali kwa kupokea mawazo mengi ya Wabunge na kuchukua mengi mazuri kuyafanyia kazi tumeona kwamba mapendekezo yaliyotolewa mengi yameshatengenezewa *schedule of*

amendment na tumeyaona humu. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa kutusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na yote hayo tuna mawazo au nina mawazo ambayo yamesemwa kutokana na hizo sheria ambazo tunataka kuzipitisha hapa. Mawazo yangu ya kwanza katika sheria ya posta na Mawasiliano ya kielektronic sura 306, katika sheria hii Mheshimiwa Waziri ameisema vizuri na jana alitaja mpaka *figure* ambazo zitakazopatikana kutokana na fedha hizi na akatoa na mgao kabisa mle, kwamba huku kitakwenda hiki, hapa kitakwenda hiki, kwenye maji kitakwenda hiki tunashukuru sana. Lakini hii sheria ni sheria ya Muungano utakaposema unawakata watanzania hizi tozo wanakatwa watanzania wote wale wa Bara na wa Visiwani wa Zanzibar wote watakuwa wanakatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo watakapochajiwa na hizi fedha tayari Mheshimiwa Waziri umeshazitangaza zinaenda wapi na wapi kuna pahala pamoja hatujasikia kwamba zitaenda ngapi kwa sababu hatosalimika mpaka yule wa Zanzibar kwamba kama atakuwa hachajiwi wala hawezi kukwepeka na sisi tunajua *regulator* wa haya ni *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufunga utuambie kuna utaratibu gani wa fedha hizi kwenda Zanzibar kwa sababu hujalisema, sasa tunakukumbusha au kama lilikwisha kuwepo basi uje utuambie Mheshimiwa kwa sababu hatosalimika kule kuna tigo, kuna Zantel, kuna Halotel, kuna *Airtel* mitandao yote kule ipo. Kwa hiyo, uje utuambie na pia jambo kama hili tunapenda Zaidi likifanyika lifanyike kwa mashirikiano kwa sababu kama kutakuwa hakuna mashirikiano hata hiyo *formular* ya kusema mnazigawa vipi hizi fedha itakuwa haipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utakaposimama utakuja na wewe ni wa jangwani mwenzangu nafikiri utanipa jawabu zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika sura ya 148 ambayo inazungumzia masuala ya *VAT* naipongeza

kwanza Serikali kwa *VAT refund* na tunaipongeza tena Serikali tulipoishauri kwamba warejesheane *TRA* na *ZRB* wazo letu amelichukua na wamelifanyia kazi na tumeliona katika *schedule of amendment*. Pia katika sura hiyo hiyo ya 148 kuna jedwali namba 7 ambalo linazungumzia *VAT exemptions* tunaishukuru Serikali imepokea kusamehe vifungashio vya madawa na kufuta lile neno kwamba lazima viwe *printed* tunashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo moja ambalo niliseme hapa ambalo ni muhimu sana jambo lenyewe kuna *raw materials* ambazo zinatengeneza vifungashio hizi *raw materials* zinazotengeneza vifungashio bado hizi hazijasamehewa na *raw materials* hizo kwa majina ni *polyoprene grainews* na *petgrainews*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chembechembe hizi zinatengeneza hivi vifungashio vinatumika sasa hivi hizi hazijasamehewa kodi ilikuwa tunamuomba Mheshimiwa Waziri kupitia jedwali hilo hilo namba 7 hebu waweke basi na hizi *raw material* za kutengeneza vifungashio ili tukisema kwamba tumeimarisha sekta ya madawa ionekana kwamba tumeimarisha. Wasiwasi wa Serikali kwamba labda *raw materials* hizi zitakuwa *misused* labda zitatumika vingine kutengenezea bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ndani ya hiyo *schedule* kumetoka *control mechanism* kwamba lazima Waziri wa Afya *approved* kwa kuwa Waziri wa Afya aki-*approve* na hawa kabla hivi vifungashio hawajaviingiza nchini kwanza wanapeleka maombi yao. Wakipeleka maombi yakiwa *approved* wakati bado *materials* ziko nje itakuwa tayari ni *control* moja lakini watakapoingia hapa kuna *TMDA* wanahusika lakini zitakapopeleka viwandani nako zinaenda kukaguliwa lakini pia zinafanyiwa uhakiki baada ya kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tukisema kwamba zitakuwa *misused* hii *control mechanism* tuliyoweka ina maana kwamba itakuwa haiwezi kufanyakazi. Lakini

kwamba hii *control mechanism* iliyokuwepo inao uwezo wa kufanyakazi, kwa hiyo niombe Serikali iruhusu na *raw materials* kwa sababu utaratibu wa kukaguliwa upo kwa hiyo hivi havitokuwa *misuse* na tutoe huo uhakika kwa sababu taratibu zote zitafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo jingine ambalo nilizungumzie linahusiana na masuala la takwimu ambalo hili mara nyingi sana huwa tunalizungumza. Hatuna takwimu sahihi tunapotaka kufanya maamuzi ya kikodi mara nyingi tunakuwa tuna *importers* pengine wa *raw materials* lakini pia tunakuwa tuna viwanda vyetu vya ndani kwa hiyo tuna *base* na takwimu zao pengine mfano labda nitoe kwenye mafuta ya kula wako watu ambao ni *manufacture* na wako wengine ni *importers* ni *suppliers* tu ambao wao wanachukua kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa takwimu zinatupeleka *wrong* wakati mwingine, sasa hivi hakuna mbegu za kuzalisha mafuta na tunajua kwamba huku tumepandisha kodi kwa mafuta ghafi tayari mafuta ya kula ghafi tushapandisha kodi lakini huku mbegu hatuna ina maana kwamba takwimu zimetucheza. Zimetucheza pia kwenye sukari, wazalishaji wa ndani wanaweza wakasema kwamba tunaouwezo wa kulisha sukari katika nchi yetu lakini kumbe tukaweka kodi kubwa kwa sukari ya kutoka nje matokeo yake mzigo wanakuja kuubeba wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali ijaribu kuwa na takwimu sahihi ili kufanya maamuzi haya ya sera za kodi yawe sahihi tusiweke maamuzi haya ya sera za kodi halafu baadaye haya maamuzi hayaji kuwa sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri alilizungumza ambalo alisema katika hotuba yake ya mwanzo na leo napenda nilizungumze kuhusiana na kupunguza miaka kwa Jeshi la Polisi miaka ya awali 12 kufikia hadi miaka 6. Hapa kwanza niipongeze Serikali lakini kingine Serikali ijaribu kuangalia hawa watumishi wetu

kwani haiwezekani kwamba tokea mwaka wa kwanza ameajiriwa huyo askari akaanza kupelekewa pesa zake katika mfuko wa pensheni kwa sababu unapokaa uaskarini kwa miaka 12 halafu baadaye hii pensheni *fund* sheria zao kama hujachangia kwa miaka 15 wewe huwezi kupewa pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa huwezi kupewa pensheni ina maana kwamba miaka yako kama ikiwa haijamalizika na taratibu za ajira za askari tunazielewa. Askari kama hujapewa cheo ukiwa una miaka 48 unatakiwa ustaafu na ukiwa cheo chako kidogo pengine huwezi kufika umri ule mkubwa na huku miaka 12 ambayo ulikuwa umekaa bure bila kuchangia kule inawezekana ukapata kiinua mgongo siyo kikubwa na ukakosa pensheni ya maana na ndiyo maana tunaweza tukaja tukawatesa askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niishauri Serikali wakati tumeamua kwamba askari watakapokuwa wanaajiriwa basi wapelekewe fedha zao katika mfuko wao tokea mwaka wa kwanza ili kuepusha kuja kupata pensheni ambayo pengine askari wengi wanaweza wakaja wakalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa na tatizo hili, jimbo langu ni jimbo ambalo lina askari wengi ndiko kwenye kambi kubwa ya polisi kwa pale Zanzibar ziwani kwa hiyo hili tatizo nimeshughulikia kesi nyingi sana za askari malalamiko yao kutokana na viinua mgongo na pensheni ambazo wanazopewa kutokana na tatizo hilo. Kwa hiyo, niipongeze Serikali lakini wafikirie Zaidi kuwapa pensheni tokea mwaka wa mwanzo ambapo anapoanza.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa King. Waheshimiwa wachangiaji wote wamekwisha niwatangazie kuwa sasa hivi kuna kikao cha *party caucus* kwenye ukumbi wa Msekwa

kwa wanachama wote wa Chama Cha Mapinduzi mnaombwa muelekee huko.

Suala Mheshimiwa Waziri la *transfer pricing* tulikwambia asubuhi Mheshimiwa Jerry, kachangia, Mheshimiwa Mwijage kachangia mnaposema mnatoa kanuni lakini vilevile mtatoza kodi kwenye mauzo halafu unasema *penalty* ni kubwa *we must be very aggressive* kwenye makosa ya kodi *short of that* hawa jamaa wataendelea kunini ukisoma takwimu Afrika ina *lose three billion dollars* kwa siku kwenye masuala ya *industries*.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa hilo mkalifanyie kazi vizuri halafu mnini na ukisema kuwa kodi itatozwa kwa mauzo huyu anayeua hajali kuogopa adhabu sababu anajua adhabu huku ishapunguzwa umenielewa Mheshimiwa Waziri anasema hapa mimi nitauza kwa bei ninayoitaka mkinikamata huku ishapunguka adhabu. Kwa hiyo, sasa *who loses* ina *lose* nchi.

Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.10 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 24 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)